HOJA ZENYE NGUVU KATIKA KUTHIBITISHA KUONEKANA ALLAH *(SUB'HAANA WATA'ALAA)* KWA MACHO HUKO AKHERA

MAJIBU NA MAELEZO.

MARKAZ SHEIKHIL-ISLAMI IBN TAYMIYYAH AL-SALAFIY,
P.O.BOX 398 TANGA,
MOBILE: 0715 615645 / 0784 615645.
BARUA PEPE: kassimmafuta@yahoo.com
PONGWE-TANGA.
TANZANIA.

Abul-Fadhli Kassim Mafuta Kassim

YALIYOMO

MAUDHUI **UKURASA**

بسم الله الرحمن الرحيم

UTANGULIZI

إنّ الحمد لله نحمده ونستعينه ونستغفره ونعوذ بالله من شرور أنفسنا ومن سيئات أعمالنا من يهده الله فلا مضلّ له ومن يضلل فلا هادي له.
وأشهد أن لا إله إلاّ الله وحده لا شريك له وأشهد أنّ محمداً عبده ورسوله أرسله بالهدى ودين الحق ليظهره على الدين كله ولو كره الكافرون.
{يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اتَّقُواْ اللّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلاَ تَمُوتُنَّ إِلاَّ وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ }آل عمران102
{يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُواْ رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُم مِّن نَّفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالاً كَثِيراً وَنِسَاء وَاتَّقُواْ اللّهَ الَّذِي تَسَاءلُونَ بِهِ وَالأَرْحَامَ إِنَّ اللّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيباً }النساء1
{يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلاً سَدِيداً يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَمَن يُطِعْ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزاً عَظِيماً }الأحزاب }الأحزاب70-71

أما بعد: فإنّ أصدق الحديث كلام الله وخير الهدي هدي محمد صلى الله عليه وسلم وشرّ الأمور محدثاتها وكلّ محدثة بدعة وكلّ بدعة ضلالة وكل ضلالةفي النار.

Ama baada ya kumsifia mola wetu kwa sifa njema, sina budi kumswalia Mtukufu Mtume wetu Muhammad –swalla llaahu alayhi wasallam-, na swala na salamu hizo pia ziwafikie Aali zake, wake zake, maswahaba zake na wale wote walioiandama njia yao kwa wema mpaka siku ya malipo.

Kwanza, napenda kusema machache kuhusu kitabu hiki, sababu za kuandikwa kwake na madhumuni yake.
Sababu kuu na asili ya kitabu hiki ni majibu na maelezo dhidi ya kitabu kiitwacho; "HOJA ZENYE NGUVU JUU YA KUTOONEKANA MWENYEZI MUNGU KWA MACHO" cha Ndugu JUMA M. Al-Mazrui.
Maudhui ya kitabu hicho ni kama kinavyojieleza chenyewe katika anwani yake, nayo ni kupinga kuonekana kwa Allah kwa macho huko akhera, na hiyo ndiyo itikadi ya makundi mengi ya batili kama vile: Mu'tazila, Khawariji (Ibadhi), Shia, na wengineo

Ndugu Juma M. Al-Mazrui muandishi wa kitabu hicho hakuleta jambo jipya, bali amejikakamua kwa kiasi kikubwa mno kuitetea itikadi hiyo batili inayopingana na mafundisho sahihi ya Qur'an na Sunna za Mtume wetu Muhammad-swalla llaahu alayhi wasallam-.

Baada ya kukisoma kwa utulivu na umakini kitabu hicho chenye kurasa 339 kutoka mwanzo hadi mwisho, sikuweza kuuvumilia upotashaji alioufanya, ndipo nilipoamua kukirudia tena na tena kwa lengo la kuyadhibiti yale ambayo nimeyaona kuwa ndio mambo ya msingi aliyoyategemea muandishi huyo kwenye kitabu chake hicho kwa lengo la kutaka kuhakiki zaidi.

Baada ya kufanya utafiti wa kielimu ambao lengo lake lilikuwa ni kupata faida, nikaona kuwa ninaowajibu wa kuzitawanya faida hizi ili ziwafikie wengineo katika waislamu ambao wengi wao hawana uwezo wa kufanya utafiti wa kielimu kwa kutumia misingi sahihi mpaka kuufikia ukweli.

Kutokana na majukumu niliyonayo pamoja na ufinyu wa wakati, kazi hii niliiona kuwa ni ngumu mno hivyo nilikata tamaa, kwa sababu shughuli hii si ndogo na inahitaji muda wa kutosha, lakini mambo makuu manne ndiyo yaliyonipa moyo wa kukiandika kitabu hiki:

i) Amri zilizokuja kuhimiza kuibainisha haki, na makatazo yaliyokuja kuharamisha kuinyamazia batili.

ii) Hali ya hatari ambayo inayowakabili waislamu wengi hasa wale wasio na uwezo wa kufanya utafiti wa kielimu; ima kwa sababu ya udhaifu wa kielimu au kwa sababu ya uvivu wa kutafiti au kukosa nyenzo za kufanyia utafiti huo au kwa sababu nyinginezo, hivyo hawataweza kukabiliana kielimu dhidi ya ubabaishaji alioufanya ndugu Juma, na hatima yake wataingia kwenye dimbwi la batili kwa kudhania kuwa upotoshaji alioufanya ndugu Juma Mazrui kuwa ni haki.

iii) Kupambana kwa kalamu dhidi ya watu wa bid'a na wapotoshaji wote ni moja katika amali njema za kumweka mtu karibu na Mola wake kwa sababu ni katika sampuli za Jihadi.

iv) Na kwa kuwa suala hili linafungamana na kuhusiana na mambo ya itikadi, ambayo ndiyo msingi wa dini, bado tuna wajibu wa kuielimisha jamii hata kama hakujitokeza mpotoshaji.

Kwa kuyazingatia yote hayo, nilipata ari na hima ya kulikabili jambo hili kwa umakini, na kwa Tawfeeq ya Allah nikafanikiwa kukikamilisha kitabu hiki kwa salama.

Na zote hizo ni miongoni mwa fadhila nyingi za Mola wangu juu yangu, ninamuomba anijaalie niwe miongoni mwa wenye kumshukuru.

Mwandishi.

Abul-Fadhli Kassim Mafuta Kassim._

كلمة شكر وتقدير

بسم الله الرحمن الرحيم

الحمد لله رب العالمين والصلاة والسلام على أشرف الأنبياء والمرسلين وعلى آله وأصحابه والتابعين لهم بإحسان إلى يوم الدين.

فقد اطلعت على كتاب الأخ الفاضل أبي الفضل قاسم مفوتا قاسم فوجدته كتاباً مفيداً في نوعه فى الرد على الخوارج الإباضية , حيث أتى فيه المؤلف بالحجج الباهرة فى إثبات رؤية الله تعالى فى الآخرة , وكشف فيه عن كذب الأخ جمعة المزروعي وشيوخه وتلبيسهم فى تلك الحجج الظاهرة كالشمس فى رابعة النهار , فجزى الله المؤلف عنا وعن المسلمين خيراً , وبارك الله له فى علمه وفى جهوده الجبارة فى نشر عقيدة السلف والذب عنها.

وصلى الله وسلم على نبينا محمد وعلى آله وصحبه أجمعين

كتبه الفقير إلى رحمة الله :

أبو هاشم عبدالقادر بن هاشم بن عبدالقادر المساوي

13 / جمادى الأولى / 1430 هـ

8 / مايو / 2009 م

PONGEZI NA SHUKRANI (1)

Sifa njema zote ni za Allah Bwana wa viumbe wote, na swala na salamu zimshukie mtukufu wa Manabii na Mitume, na Jamaa zake na Swahaba zake na waliowafuatia hao kwa wema mpaka siku ya malipo.

Ama baada ya yaliyotangulia.

Nimekitalii kitabu cha ndugu mbora Abul-Fadhli Kassim Mafuta Kassim, nikakikuta kuwa ni kitabu kilicho na faida kwa sampuli yake, katika kuwajibu Makhawariji wa Kiibadhi, pale mtunzi alipozileta HOJA ZENYE NGUVU katika kuthibitisha kuonekana Allah huko Akhera kwa macho, na akaufichua uwongo wa ndugu Juma Al-Mazrui na masheikh zake pamoja na ubabaishaji wao kwa hoja za wazi wazi kama vile jua lililokuwa katikati ya mchana.

Allah amlipe mtunzi kheri kwa sababu ya kuwatumikia waislamu, na ambariki katika elimu yake na juhudi zake kubwa katika kuitangaza itikadi ya Salaf na kuitetea.

Na swala na salamu zimshukie Mtume wetu Muhammad na Jamaa zake na Maswahaba zake wote.

Al-Akhi Sheikh Abu Hashim Abdul-Qadir Ibn Hashim Ibn Abdul-Qadir Al-Musawaa
13 /Jumadal-Ulaa /1430 H.
8 /Mei / 2009 M.

Pongezi na Shukrani (2)

Ama baada ya kukipitia kitabu cha ndugu yetu Abul fadhli Kassim Mafuta, kitabu chenye anuani ya kitabu HOJA ZENYE NGUVU katika kuthibitisha kuonekena Allah kwa macho huko akhera, majibu na maelezo, kitabu hiki nimekipitia chote kwa uwangalifu na insaafu, ni kitabu madhubuti kinacholingana na jina lake kwani makusudio yake makubwa ni kutetea itikadi sahihi ya Manabii na Mitume wote, itikadi ya AHLI SUNNATI WAL-JAMAA dhidi ya waandishi wa uwongo, walio dhidi ya itikadi hii safi, kwani kitabu hiki kimebainisha waziwazi kwa hoja sahihi juu ya upotovu wa mtunzi wa kitabu kiitwacho HOJA ZENYE NGUVU JUU YA KUTOONEKANA MWENYEZI MUNGU KWA MACHO cha ndugu JUMA AL-MAZRUI ambae ni miongoni mwa wafuasi wa mapote ya matamanio kwani ndugu Juma ndani ya kitabu chake hicho amemsingizia uwongo Mwenyezi Mungu na Mtume wake kama kawaida ya watu wa matamanio kumsifu Allah sub'haanahu wata'alaa kwa sifa ambazo ametakasika nazo za kutoonekana, ilhali Mwenyezi Mungu Sub'haanahu wata'alaa amejisifu yeye mwenyewe nafsi yake kwa sifa ya kuonekana huko akhera na pia akasifiwa na Mtume wake Muhammad swalla llaahu alaihi wasallam kwa sifa hiyo hiyo ya kuonekana na hii ndio itikadi ya Maswahaba wa Mtume Muhammad swalla llaahu alaihi wasallam na ndio itikadi ya Taabiina na wema waliofuata baada yao itikadi ya Ahli-Sunnat Wal-Jamaa.

Ndugu Juma Al-Mazrui ameandika kitabu hicho ili atetee itikadi yake ya kikhawarij kama ilivyo kawaida ya watu wa matamanio kabla ya kusoma na kufahamu jambo, wao kwanza ni kutetea itikadi zao vyovyote iwavyo kama vile walivyoipokea toka kwa mababu zao, lakini kwa rehema za Mwenyezi Mungu sub'haanahu wata'alaa amejaalia katika umma huu kama anavyosema Mtume katika hadithi sahihi kwamba: HALITAACHA KUWEPO KUNDI KATIKA UMMA WANGU LENYE KUPIGANIA HAKI HAWATADHURIWA NA

WASIOWASAIDIA NA WALA HATADHURIWA NA WANAOWAPINGA MPAKA KITAKAPO SIMAMA KIYAMA na watu hawa ni AHLI-SUNNAT WAL-JAMAA.
Ama ndugu Juma Mazrui mimi namlaumu sana kwa kufanya haraka kuandika kitabu hicho bila ujuzi wa dini, lakini baada ya lawama namuomba Mwenyezi Mungu amuongoze ndugu Juma na ampe maarifa na amtoe katika hali ya itikadi potofu, kwani kubwa la Juma ni kumuamini sana Said Mabruk Al-Qanuubi bila kumuelewa elimu yake na uwadilifu wake kwani inaonyesha bwana Juma hamfahamu bwana huyu Qannubi na ndio maana akampachika majina makubwa ya kielimu ambayo hastahiki jinsi alivyo, kwani Said Qannubi si mwengine zaidi ya kuwa ni mwanakasumba wa kikhawariji si mkweli, angelikuwa ni mkweli asingelifikia hali ya kunukuu hoja hai za ndani ya vitabu vya wanakasumba na watu wa matamanio na yeye kuzifanya hoja za kuwarudi Ahli-Sunnat wal-Jamaa.

Ama marudio anayorudiwa ndugu Juma ndani ya kitabu hiki ni malipo yatokanayo na chumo la mikono yake iliyoandika maandiko ya Qannubi ambaye ni mwanakasumba wa kikhawariji aliyeiajiri mikono yake juu ya kunukuu maneno ya watu wa matamanio wenye chuki dhidi ya wanasunnah, na maimamu wa Ahli-Sunnat.
Miongoni mwa watu anaowaiga Qannubi maandiko yao ni kama Al-kauthari, na Abuu Ghudah na Jamal-din Af'ghani ambaye si Muaf'ghani bali ni Muirani, na Butwi na Al-Maliki katika watu wa hivi karibu na pia miongoni mwao hao ni pote la Muutazilah kwani wao ndio wanaopinga sana kuonekana kwa Mwenyezi Mungu sub'haanahu wata'alaa kwani pote hili elimu yao yote imejengeka juu ya misingi ya mijadala ambayo asili yake ni vipimo vilivyo juu ya kufananisha kisichopo kwa kilicho kuwepo na miongoni mwa maigizo ya Qannubi ni pote la Jahmiyyah, Baatiniyya, Mashia Imamiyyah ndio maana utayakuta maandishi yao yote juu ya kutoonekana Mwenyezi Mungu sub'haanahu wata'alaa wanayanukuu kwa mwana matamanio mkubwa adui wa Mwenyezi Mungu sub'haanahu wata'alaa Abdul

Jabbar al-Muutazili kwenye kitabu chake almughni, hasa katika zile hoja za kiakili alizozitaja Alkhalili kama alivyomnukuu Juma Mazrui katika kitabu chake Al-Haqu Addamigh ukurasa 67, kwamba kuona kwa macho ni kuingia sura ...., na kadhalika amefananisha kuonekana Mwenyezi Mungu sub'haanahu wata'alaa na kuonekana viumbe, ametakasika Mwenyezi Mungu na dhana zao.

Na vilevile Qannubi si mwenye elimu ya vitendea kazi (Qawaid) vya elimu za waislamu kama somo la hadithi na ala zake na usuli na misingi ya fiqhi na lugha ya waarabu, lakini ni shujaa asiye na uwoga wala aibu na ndio maana utakuta mara nyingi hutoa hukumu juu ya hadithi kutokana na ushujaa wake mfano;- anasema kwamba hadithi ambazo zimepokewa zenye kuifasiri aya ya 22 na ya 23 za surat Al-Qiyamah ni dhaifu na za uwongo, na Juma Al-Mazrui akamfuata kiongozi wake Qannubi na ilhali hadithi hizo zote zilizokuja kutafsiri aya hizo ni Mutawatir kwa mujibu wa majio yake na kwa mujibu wa ushuhuda wa wanazuoni wa somo la hadithi, pia Qannubi kutokana na kutoelewa somo hili utakuta anamtia ila (dosari) mpokezi wa hadithi pasi na kuielewa ila ile kwamba haiwi hadithi ya mpokezi yule ni dhaifu, mfano amemwita imamu Zuhri kwamba ni Mudalis ili aidhoofishe hadithi zake bila kubainisha ni tadlis ipi ili muradi atetee matamanio yake.

Haya nimeyataja machache, lakini makosa ya namna hii ni mengi juu ya Qannubi na mfano wa hayo, na yote haya yanatokana na kasumba za kimadhehebu zinazompelekea Qannubi na mfano wake kuandika mambo wasioyajua ili watetee madhehebu yao kwa hali na mali, mfano Juma Mazrui, nikisema kwamba hana ujuzi katika somo la hadithi sitakosea, lakini hebu tumsikilize yeye mwenyewe anavyojieleza katika kitabu chake "Hoja zenye nguvu" katika ukurasa wa 194 anamwita mpokezi wa hadithi kwa jina ambalo sio lake, mpokezi huyu jina lake ni Ibn Halbas yeye akamwita Abu Halbas, mfano mwingine katika kitabu chake hicho katika ukurasa wa

69 amemwita Al-Duuriy, Al-Dauri na haya ni mengi mno kwenye maandiko ya Juma na haya ni kwa kuwa haja wahi kukaa na watu wa elimu hizi, labda aliwahi kukaa na Qannubi kisha akamuiga porojo zake na ndio maana akasema Ibnu-Halbas ni majhulil-ayn bila ya kubainisha ni majhul wa vipi, lakini yeye katika uibadhi wake Imamu wake aitwae Abuu Ubaidah Muslim Ibni Abi Karimah yeye ndiye Majhuli tena ni Majhulil-Ayn, mtu huyu ni kigano, lakini kwa kutojua kwao wanadhania yupo, sitaeleza mengi bali mengi yameshaelezwa ndani ya kitabu hiki na mwenye kutaka haya arudi kuangalia vitabu vya watu wa Sunnah kama kitabu Assunnah, Arrisalatu alhamawiyyatu alkubraa, Al-Aqidatu Atwahawiyah, na Minhaju Assunnah na vinginevyo.

Ama kitabu hiki cha ndugu yetu Abul-Fadhli ni kitabu kilichokusanya faida nyingi sana haswa katika somo azizi la hadithi na pia katika somo la lugha ya waarabu, faida ambazo hazipatikani katika vitabu vingi vilivyokwisha andikwa kwa lugha ya waswahili. Mwenyezi Mungu sub'haanahu wata'alaa amlipe ndugu yetu huyu kheri na amzidishie elimu na uongofu na kulingania dini ya Mwenyezi Mungu sub'hanahu wata'alaa kwa hekima na elimu, kwani Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kutakabali dua za watu wake na rehema na amani zimfikie Mtume wetu Muhammad swalla llaahu alaihi wasallam na Aali zake na Maswahaba zake.

Al-Akhi Sheikh Abuu Saam Seif .S. Al-Ghafriy.

SHUKRANI

Ni Allaah peke yake ndiye wa kuhimidiwa na kushukuriwa, kwa hiyo sina budi kusema:

الحمد لله (Al-Hamdu lillaahi) kwa kuniwezesha kukiandika kitabu hiki na ninamuomba Allaah akijaalie kitabu hiki kiwe ni chenye kheri, faida na manufaa kwa waislamu wote hasa wasomi wa mambo ya dini na wale wenye kuitafuta elimu ya dini na kuyafuatilia mambo ya dini kwa ukaribu na wakawa wako tayari kutoa wakati wao na hali na mali zao kwa ajili ya elimu ya kuutafuta ukweli kupitia elimu ya dini.

Pamoja na hayo, pia ninawashukuru wale wote ambao wametoa juhudi zao kwa njia mbali mbali kwa ajili ya kufanikisha kutoka kwa kitabu hiki, ima kwa kutoa nasaha na ushauri wao, au kwa kuutumia wakati na mali zao.

Pia ninawashukuru ndugu zangu wapenzi:

Sheikh Abu Hashim Abdul-Qadir Hashim Al-Musaawiy Al-Hashimiy.

Na Sheikh Abu Saam Seif .S. Said Al-Ghafriy.

Kwa kazi yao kubwa waliyoifanya ya kukipitia kitabu hiki na kwa nasaha zao na ushauri wao walioutoa. Pia ninamshukuru ndugu yangu mpenzi Sheikh Abu Ar'qam Abdallah Muhsin kwa kunishajiisha na kunipa moyo wa kukichapisha kitabu hiki wakati nilipomuonyesha nuskha ya kitabu hiki kabla ya kukichapa.

Mwisho ninamshukuru Ahli yangu Ummul-Fadhli kwa ustahamilivu wake na uzito alioubeba mpaka nikaweza kukimaliza kitabu hiki.

Abul-Fadhli Kassim Mafuta Kassim

Markaz Sheikhil-Islami Ibn Taymiyyah, Pongwe-Tanga Tanzania

25/SHAABAN/1428 H = 26/08/08 M.

Nimekianza kitabu hiki kwa kumsifia Allah sub'haanahu wata'alaa Mola wetu mkarimu na kumswalia Mtume wetu Muhammad swalla llaahu alaihi wasallam pamoja na Aali zake na Maswahaba zake wote.

Kisha nikalazimika kuzijibu baadhi ya tuhuma za uwongo ambazo amezileta ndugu Juma dhidi ya maulamaa wa kiislamu kama vile Ibnu Taymiyyah, na Ibnul-Qayyim Allah awarehemu kwa lengo la kutaka kuwachafua.

Kisha nikaweka mlango maalumu kwa ajili ya kuelezea kwa muhtasari uchambuzi wa elimu ya hadithi, na kanuni za upokezi wa habari.

Pia tukabainisha sababu za msingi za upotevu wa watu, na kuyabatilisha madai ya uwongo ya ndugu Juma pale alipodai kuwa chanzo na sababu ya upotevu ni kukataa kuwepo kwa majazi ndani ya Qur'ani.

Pia tumelazimika kujadili kielimu tena kwa muhtasari suala la Majazi kuwepo kwake na kutokuwepo na tofauti za maulamaa wa kiislamu juu ya suala hilo.

Kisha ndio tukaanza kuubainisha msimamo sahihi wa AHLI-SUNNA WALJAMAA, juu ya mas'ala ya kuonekena Allah kwa macho huko akhera, na suala hili ndiyo maudhui mama ya kitabu hiki.

Na tumelizungumzia suala hili kwa namna tatu:

i) Kuithibitisha itikadi hii kupitia maandiko matakatifu ya dini yetu kama vile; Qur'an na Hadithi sahihi za Mtume Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam- pamoja na kutoa maelezo kwa muhtasari juu ya maandiko hayo.

ii) Pia nimetumia kauli za Maswahaba na wanafunzi wa Maswahaba (Taabiina) na Maimamu wakubwa wa kiislamu kama vile Imamu Malik, Imamu Shaafiy, Imamu Ah'mad bin Hanbal na wengineo kwa

lengo la kuutilia nguvu msimamo wetu, na kuibatilisha dhana ya kwamba itikadi ya kuonekana Allah akhera kwa macho ni itikadi ya wale ambao ndugu Juma na kaumu yake anawaita kuwa ni Mawahabi.

iii) Kuzivunja baadhi ya hoja batili zilizotolewa na muandishi huyo hasa zile ambazo ndiyo msingi aliojengea juu yake itikadi yake hiyo potofu.

iv) Mwisho tukamalizia kwa kuweka Khatima.
Hayo yote nimeyafanya kwa ufupi mno, na sikutaka kumjibu hoja baada ya hoja au neno kwa neno kwa kuhofia kurefusha, hasa ukizingatia kuwa ndugu Juma Mazrui amekijaza kitabu chake maneno mengi ambayo si ya kweli na yasiyo na uzito katika misingi ya kielimu.

SURA YA KWANZA

VIPI TUTAMFAHAMU MOLA WETU NA WAPI TUICHUKUE IMANI YA DINI YETU?

Hili ni swali muhimu mno na jawabu sahihi la swali hili ndiyo ufumbuzi wa matatizo mengi yaliyojitokeza katika umma wa kiislamu, kwa sababu waislamu wengi hawajui vipi watamfahamu mola wao muumba, na wapi wanatakiwa kuichukua dini yao !

Ama Ahlu Sunna wal Jama'a wao wanaitakidi kwamba:
Tutamjua mola wetu kwa vile alivyojielezea yeye mwenyewe katika kitabu chake (Qur'an tukufu) na vile alivyotuelezea mjumbe wake mtukufu katika mafundisho yake yaliyo sahihi.
Kwa kuyathibitisha yale yote ambayo Allah amejithibitishia mwenyewe au ambayo ameyathibitisha Mtume wake -swalla llaahu alayhi wasallam-, na kuzikanusha sifa ambazo Allah na Mtume wake swalla llaahu alaihi wasallam wamezikanusha, bila ya kupotosha, wala kupinga, wala kumfananisha yeye na chochote katika viumbe vyake, pamoja na kufuta dhana ya kwamba kuyathibitisha yale ambayo Allah amejisifia nayo kuwa ni kumfananisha yeye –Jalla Jalaaluh- na viumbe vyake.

Na tunaichukua imani ya dini yetu kutoka kwenye Qur'an na Sunna (mafundisho) sahihi ya Mtume wetu Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam- pamoja na kuuzingatia ufahamu wa Salaf Swaalih (wema waliotangulia) kama vile; Maswahaba na Taabi'ina (wanafunzi wa Maswahaba) na maulamaa waliokuja baada yao.
Na hivi ndivyo tulivyoamrishwa na Qur'an kadhalika Sunna sahihi za Mtume swalla llaahu alayhi wasallam.

Amesema Allah -azza wajalla-:
{وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ آمِنُواْ كَمَا آمَنَ النَّاسُ قَالُواْ أَنُؤْمِنُ كَمَا آمَنَ السُّفَهَاء أَلا إِنَّهُمْ هُمُ السُّفَهَاء وَلَـكِن لاَّ يَعْلَمُونَ
البقرة13

"Na wanapoambiwa:aminini KAMA WALIVYOAMINI WATU wanasema; Tuamini kama walivyoamini wapumbavu?…".
Suratul-Baqarah aya ya 13.

Imepokewa kutoka kwa Ibnu Mas'oud na Ibn Abbaas kwamba wamesema: "Watu waliokusudiwa hapa ni maswahaba".
Tazama tafsiri al-Durrul-Manthuur juzuu ya 1 ukurasa 70-71.

Na maana ya aya hii ni kwamba makafiri na wanafiki walikuwa wakiambiwa kwamba wamuamini Allah kama walivyoamini Maswahaba wa Mtume Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam- wao kwa sababu ya kiburi, na jeuri zao walikuwa wakiwatukana Maswahaba kwa kuwaita wapumbavu, na hali ya kuwa wapumbavu ni wao !

Na amesema tena Allah:

فَإِنْ آمَنُواْ بِمِثْلِ مَا آمَنتُم بِهِ فَقَدِ اهْتَدَواْ وَّإِن تَوَلَّوْاْ فَإِنَّمَا هُمْ فِي شِقَاقٍ فَسَيَكْفِيكَهُمُ اللّهُ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ البقرة**137**

"Basi wakiamini KAMA MLIVYOAMINI NYINYI (maswahaba) basi watakuwa wameongoka.Na wakikengeuka basi wao wamo katika upinzani".
Suratul Baqarah aya ya 137.

Katika aya hii Allah anawataka Ahlul-kitabi (Mayahudi na Wakristo) wamuamini Allah kama walivyoamini Maswahaba na waislamu wote kwa ujumla walio na imani kama ya Maswahaba, na kama wataasi wakenda kinyume na Amri hiyo, basi wao watakuwa ni waasi na ni wapinzani wa Allah.
Na amesema tena Allah:

ومن يشاقق الرسول من بعد ما تبين له الهدى ويتبع غير سبيل المؤمنين نوله ما تولى ونصله جهنم.. الآية

"Na anaye mpinga Mtume baada ya kumdhihirikia uwongofu na AKAFUATA NJIA ISIYOKUWA YA WAUMINI,tutamuelekeza alikoelekea mwenyewe,na tutamuingiza katika Jahannamu…. ".

Surat An Nisaa aya ya 115.

Amesema Allah:

والسابقون الأولون من المهاجرين والأنصار والذين اتبعوهم بإحسان رضي الله عنهم ورضوا عنه...الآية

"Na wale waliotangulia, wakwanza katika Muhajirina na Answaari,na wale waliowafuata kwa wema, Allah ameridhika nao, na wao wameridhika naye…. ".

Suratut Tawba aya ya 100.

Kwa mujibu wa aya hizo zote tulizozitaja, tunatakiwa waislamu wote kuamini kama walivyoamini maswahaba wa Mtume Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam- pamoja na kuifuata njia waliyoipita.

Na kama imani zetu zitatofautiana na imani zao na njia yetu ikitofautiana na njia yao, basi tutakuwa ndani ya mashaka makubwa mno na upotevu uliowazi kama zilivyoeleza aya tulizozitaja.

Hivyo basi, tunapolizungumzia suala zima la kumuamini Allah – Sub'haanahu Wata'alaa- ni lazima tujiulize maswali yafuatayo:

Je imani zetu zinaendana na mafundisho ya Qur'an na Sunna kama walivyofahamu wema waliotangulia (Salaf Swalih)?
Je hivi tunavyoitakidi ndivyo walivyoitakidi hao Salafu Swalihi (wema waliotangulia) au la?

Na kama jawabu likiwa la, basi tujue kwamba tumo ndani ya upotevu kwa kuifuata njia isiyokuwa ya hao waumini wa mwanzo.

Na bila shaka, wao wameifahamu vizuri Qur'an na walimfahamu vizuri Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- kuliko walivyomfahamu na wanavyomfahamu na watakavyofahamu watakaokuja baada yao, ndiyo maana Allah akawasifia wao na wale walioifuata njia yao kwa wema, na akawaahidi mambo mazuri.
Na wakati huo huo akawasema vibaya wale waliyoihalifu njia hiyo, na kuwaandalia makazi mabaya motoni -Allah atuepushe na adhabu zake-.

Hivyo basi, katika suala hili la kuonekana au kutokuonekana Allah kwa macho huko akhera pia tunatakiwa pale tunapozitazama aya na hadithi zinazo lizungumzia suala hili tuutangulize mbele ufahamu wa hao wema waliotutangulia (Salafu Swalihi) katika imani, vipi wao walizifahamu aya na hadithi hizo?
Na ilikuwaje imani yao juu ya suala hilo?
Je waliamini kwamba Allah ataonekena kwa macho huko akhera kama wanavyo amini Ahli Sunna?
Au Allah hataonekana kwa macho huko akhera kama ilivyokuwa itikadi ya makundi mengine kama vile: Jah'miyyah, Mu'tazila na wajukuu zao kama vile Shia, Ibadhi na wengineo miongoni mwa watu wa bid'a?

Inshaallah swali hili litajibiwa na kitabu chetu hiki, tafadhali fuatilia kwa makini na insafu utagundua ukweli juu ya suala hili.

Huenda mtu akatatizika au akatatizwa kwa kuambiwa: vipi tufuate njia ya hao waliotangulia (Maswahaba,Taabi'ina, na Maimamu waliokuja baada yao) na hali yakuwa wao wenyewe wametofautiana katika mambo mbalimbali?

Jawabu ni kwamba; tutashikamana na ufahamu wao katika mambo ambayo wameafikiana, na yale waliyotofautiana sisi tutaichukua kauli

iliyoungwa mkono na maandiko sahihi, na wala haifai kuzusha kauli ya tatu zaidi ya kauli zao mbili zilizo tofauti.

Ama mambo ambayo hayakuwepo katika wakati wao katika yale ambayo yanafaa kutumia akili na rai, basi huo ndiyo uwanja wa kuogelea maulamaa katika kufanya ijtihadi na kutumia rai zao kwa mujibu wa kanuni na misingi ya kielimu.

Swali la kujiuliza ni; Je hao wema waliotangulia wametofautiana juu ya suala la kumuona Allah kwa macho huko akhera?

Jawabu ni kwamba:
Maswahaba Hawakutofautiana katika suala hili, bali wote waliafikiana kwamba watu wema watamuona mola wao kwa macho huko akhera kama lilivyo thibitishwa suala hilo na Qur'an na Sunna sahihi za Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam-.
Na hakuna mtu yeyote aliyemuona, wala atakayemuona Allah kwa macho yake hapa duniani, na hivyo ndivyo wanavyoamini na kuitakidi Ah'lu Sunna Wal-jamaa.
Lakini tofauti imekuja katika jambo ambalo ni nje ya maudhui yetu hii, jambo lenyewe ni: Je bwana Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- alimuona Mola wake katika usiku aliokwenda mbinguni (Miraji) ?
Jawabu ni kwamba, kuna kauli iliyopokewa kutoka kwa Ibn Abbas -Allah amridhie- kwamba; bwana Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- alimuona Mola wake katika usiku huo.
Wengi katika wanavyuoni wakayachukulia maneno yake hayo kwamba, makusudio yake ni kuwa bwana Mtume alimuona Mola wake kwa moyo wake, na wakategemea riwaya nyingine zilizopokewa kutoka kwa huyo huyo Ibn Abbas.

Ama kuhusu suala la kumuona Allah usingizini hili pia si katika maudhui ya kitabu hiki.

SURA YA PILI

UCHAMBUZI YAKINIFU JUU YA ELIMU YA HADITHI.

Kabla ya kuanza kuzitaja hoja na dalili wanazozitegemea Ahli sunna wal- Jamaa juu ya kuonekana Allah kwa macho huko akhera, kwanza napenda kuzungumzia suala linalofungamana na elimu ya istilahi ya upokezi wa riwaya za hadithi za bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- na suala hili litakuwa katika nukta zifuatazo:

i) Kwanza, tufahamu kuwa mafundisho yote ya bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- ni wah'yi (ufunuo) utokao kwa Allah, na Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- hazungumzi kwa matashi wala matamanio ya nafsi yake.

ii) Pili, mafundisho yote ya Mtume wetu Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam- yamehifadhiwa katika vitabu vya maulamaa wa Ahlu Sunna wal-Jamaa kwa ufanisi mkubwa mno kiasi ambacho hakuna jambo lolote linalohitajika kubainisha itikadi au hukumu ya mambo ya dini ya kiislamu isipokuwa jambo hilo limedhibitiwa kwa ufanisi wa hali ya juu.

iii) Tatu, katika kuhakikisha kuwa mafundisho hayo sahihi ya dini ya kiislamu yanahifadhiwa na hayachanganyiki na upotofu wowote, maulamaa wa Ahli Sunna wal Jamaa wameweka misingi madhubuti juu ya usahihi wa mapokezi hayo ya riwaya za hadithi za bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- na ukweli wa wapokezi hao kama tulivyofundishwa na Qur'an tukufu pale aliposema Allah:

يأيها الذين آمنوا إن جاءكم فاسق بنبإ فتبينوا .

"Enyi mlioamini ! akikujilieni mwovu (fasiki) na habari yoyote basi ichunguzeni" al Hujraat (49) aya 6.

Kwa mujibu wa aya hii ni kwamba, si kila asemaye; amesema Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- atakuwa msemaji huyo ni mkweli, na atakayo yanukuu yatakuwa ni kweli maneno ya Mtume, bali ni lazima uchunguzi wa kina ufanyike ili kujua usahihi wa habari hiyo aliyoileta na udhaifu wake.

Kwa sababu hiyo, maulamaa wa hadithi baada ya kufanya utafiti wa kina pamoja na kutumia uzoefu wao wa muda mrefu, wakaweka misingi madhubuti inayowahusu wapokezi wa hadithi.
Pia wakaweka kanuni maalumu kwa ajili ya udhibiti wa njia sahihi za kukubaliwa hadithi na kurudishwa.
Na pia yakatumika maneno ya kiistalahi ambayo yanaleta maana maalumu na hayo yamejaa kwa wingi katika vitabu vyao.

Kwa mantiki hiyo, yeyote anayetaka kuzungumzia masuala yanayofungamana na elimu ya hadithi; usahihi wake na udhaifu wake, hana budi kuzijua kanuni hizo na maneno hayo ya kiistilahi.
Na kama hatafanya hivyo, basi lililobora kwake ni kunyamaza kuliko kusema, kwa sababu hatima yake ni kupotosha watu kwa kuzisahihisha hadithi zisizo sahihi au kuzidhoofisha hadithi zilizo sahihi na yote mawili ni balaa, hasa ukizingatia kwamba maneno ya Mtume Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam- ni sheria.

<u>MASHAR'TI</u>
<u>YA USAHIHI WA HADITHI</u>

1) العدالة <u>Uadilifu</u>, ni lazima kila mpokezi wa hadithi za Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- awe ni mtu mwenye akili timamu,mwenye uwezo wa kupambanua mambo hata kama ni mtoto mdogo, awe mkweli, mcha mungu na wala asiwe mwongo, zenye kuvunja heshima.

2) تمام الضبط Hifdhi nzuri wala asiwe mwenye kufanya maasia kwa dhahiri wala asiwe na tabia mbaya

, mpokezi awe na uwezo wa kudhibiti maneno aliyo yapokea, bila ya kubadilisha chochote katika maana yake,au kukosea sana,au kubabaika kulikopetuka mipaka wakati wa kusimulia mapokezi hayo.

3) اتصال السند Kuungana kwa sanadi (msururu wa wapokezi) kwa kuwa kila mpokezi awe amepokea kutoka kwa aliye juu yake mpaka mwisho wake (kwa huyo ambaye habari hiyo imenasibishwa kwake, ima bwana -Mtume swalla llaahu alayhi wasallam-, au swahaba, n.k.

4) عدم الشذوذ Isiwe habari aliyoileta mpokezi huyo ni "SHAADHUN" (ni yenye kupingana na habari ya mpokezi mwingine aliye madhubuti au wengi zaidi kuliko yeye).

5) عدم العلة الخفية القادحة Wala isiwe na ila (kasoro iliyojificha) kama vile Idh'tiraabu (mgongano baina ya wapokezi n.k) au kuwa ni habari Maq'luub (yenye kugeuzwa)

Katika masharti haya tuliyoyataja, yako ambayo likikosekana moja tu basi hadithi haitakubaliwa,kama vile:

1-Kuwa mpokezi si muadilifu,kwa kuwa ni mwongo au asherati n.k.

2-Kupatikana kasoro kama vile mgongano katika sanadi (njia) au mgongano wa maneno katika habari hiyo, kisha ikawa imeshindikana kuziunganisha au kuipa nguvu njia moja juu ya nyingine.

Tanbihi:

Habari inaweza kuwa na njia nyingi, na katika njia hizo wakawepo wapokezi wasio madhubuti kwa kuwa wanakosea kiasi, au silsila (mtiririko) wa wapokezi haukuungana, kutokana na wingi wa njia hizo habari hiyo itapata uzito na kuhesabiwa kuwa ni sahihi, na kwa lugha ya kitaalamu huwa wanaiita "HASANUN-LIGHAIRIHI".

Amesema Imamu An-Nawawiy:

"بل ما كان ضعفه لضعف حفظ راويه الصدوق الأمين من وجه آخر وصار حسناً وكذا إذا كان ضعفها لإرسال زال بمجيئه من وجه آخر...".

"Bali ile hadithi ambayo imekuwa ni dhaifu kwa sababu ya udhaifu wa mpokezi wake ambaye ni mkweli mwaminifu utaondoka (udhaifu huo) kwa kuja kwake kupitia njia nyingine na itakuwa ni HASAN (sahihi)

Na vile vile ukiwa udhaifu wake ni kwa sababu ya Ir'saal (atakaposema Taabi'I amesema Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam-) pia udhaifu huo utaondoka kwa kuja (kupokewa) kwa njia nyingine...".

Hivyo basi, inawezekana ukaifuatilia hadithi kisha ukazikuta takriban njia zake zote zina udhaifu, hapo hutakiwi kuwa na pupa na kuanza kuihukumu hadithi yote kuwa ni dhaifu, bali unatakiwa kuihukumu sanad husika tu, na useme kwamba sanad ya hadithi hii ni dhaifu.

Kwa sababu udhaifu wa sanad moja tu, si ushahidi wa udhaifu wa hadithi yote yenye njia nyingi.

Na kama ukitaka kuihukumu hadithi yote kwa njia zake zote unatakiwa ufanye kazi ya kuzikusanya sanad (njia) zote kisha ndiyo uichambue sanad moja baada ya nyingine kwa kufuata kanuni na taratibu za elimu ya hadithi (mustalahul-hadithi).

Na kama itakubainikia kuwa njia zote zina udhaifu, basi pia unatakiwa kuangalia sababu za udhaifu wake.

Je udhaifu wake ni mwepesi au mzito?

Kama ni mwepesi basi hadithi hiyo kwa kuzijumuisha njia zote hizo itakuwa ni "Hasanun-Lighayrihi" (sahihi) na itafaa kuifanya kuwa ni hoja ya kisheria, na wala haitohesabiwa kuwa ni dhaifu.

Hili ni jambo muhimu sana katika elimu ya hadithi kulifahamu na kulizingatia, lakini ndugu Juma kwa makusudi hakuuzingatia utaratibu huu kwenye kitabu chake "Hoja zenye Nguvu" kwa sababu anazozijua mwenyewe, kwani yeye ndiye aliyesema hivi:

“kitaalamu ikiwa hadithi imepokewa na wapokezi wengine kabisa, lakini hadithi ni ile ile, basi huambiwa kuwa hadithi hiyo ina shahidi.”
Mwisho wa kunukuu.
Tazama “Hoja zenye Nguvu” ukurasa 70.
Lakini huko mbele -Inshaallah- utazigumdua sababu zilizomfanya ndugu Juma aupuuze utaratibu huu.

TUHUMA ZA UWONGO DHIDI YA AHLI SUNNA

Kama ilivyokuwa kawaida ya watu wanaofuata matamanio ya nafsi zao katika mambo ya dini kama vile: Mayahudi, Manasara, Washirikina na kadhalika watu wa bid'a, huwa hawaachi kuwasema vibaya wale walioshikamana na njia sahihi na kuwataja kwa kebehi na uovu, tena mpaka kufikia kuwazulia uwongo.

Huu ndiyo mwenendo wao na sera yao tangu zamani, jambo la kusikitisha zaidi ni kuwa hata ndugu Juma naye ameifuata njia hiyo ovu dhidi ya Ahli Sunna wal-Jama'a.

Amekianza kitabu chake kwa mashambulizi yasiyo na ukweli dhidi ya Ah'li Sunna na maulamaa wao, tena bila ya kuwa na insafu wala uadilifu, bali chuki binafsi na uadui ndivyo vilivyomuongoza na kumsababishia kuacha kuyahakiki mambo kwa njia za kielimu, kwa mfano:

1-Hakuna kitu kingine zaidi ya chuki kilichomfanya awaite Ah'lu Sunna kwa jina la Mawahabi, au Hashawiya, au Mujasima.

2- Hakuna kitu kingine zaidi ya chuki dhidi ya Ah'li Sunna kilichomfanya awatie kasoro kwa mambo ambayo hayakuthibiti kuwa

ndiyo itikadi yao, kama suala la kuwa Allah ana sura ya kijana, au ana viatu vya dhahabu na mengineyo.

3-Hakuna jambo jingine zaidi ya chuki na uadui lililompelekea kuwatuhumu baadhi ya wanavyuoni wa Ah'li Sunna kama vile Ibn Taymiyyah na Ibn Al-Qayyim kwa sababu ya misimamo yao na kuwaita kuwa ni wanavyuoni wa kiwahabi! Maimamu wa Hashawiya! Mujasima! Na hali yakuwa hakuna tofauti yoyote baina ya misimamo yao hiyo na misimamo ya Maimamu wakubwa wa Ahli Sunna kama vile: Abu Hanifa, Imamu Malik, Imamu Shaafiy, Imamu Ah'mad Ibn Hanbal, Imamu Bukhari, Imamu Muslimu, Imamu Abu Daud, Imamu Tirmidhiy, Imamu Abul-Hasan Al-Ash'ariy, Imamu Abdul-Qadir Jaylaaniy !!!

Kwamfano katika suala la sifa za Allah: kuwa Allah ana mikono miwili, ana macho mawili, ana uso, anacheka, ana mguu na nyinginezo katika sifa za Allah za ukamilifu ambazo amejisifia nazo au amesifiwa na Mtume wake –swalla llaahu alayhi wasallam- utawakuta maimamu hawa wakubwa wanazithibitisha sifa hizo kama zilivyopokewa, na hivyo ndivyo anavyofanya Ibn Taymiyya na Ibn al-Qayyim.

Lakini Juma kwa sababu ya chuki zake dhidi ya Ibn Taymiyya na Ibn al-Qayyim akalizungumzia suala hilo kwa sura ambayo msomaji anaweza kudhania kuwa Ibn Taymiyya na Ibn al-Qayyim wana itikadi ambayo si ya kiislamu na wala hakuna muislamu yeyote mwenye itikadi hiyo ila Ibn Taymiyya na mwanafunzi wake Ibnul-Qayyim.

Kwa mfano amesema Juma:
"Na itikadi hizi ambazo nitakutajia sasa hivi (Inshala) zimo hasa katika madhehebu ya kiwahabi na wao wamezirithi kutoka kwa maimamu wa madhehebu za Al-hashawiya Al-mujasima kama Ibn Taymiyya Ibn Qayyim Al-

jawziya na wengineo".Mwisho wa kunukuu. Tazama kitabu chake "Hoja zenye Nguvu" ukurasa wa 23.

MAJIBU YETU

Sisi tunasema kwamba msimamo wa Sheikhul-Islami Ibn Taymiyya na mwanafunzi wake Ibn al-Qayyim katika mas'ala ya sifa za Allah hauna tofauti na msimamo wa Qur'an na Sunna, bali ndiyo msimamo wa maswahaba na wanafunzi wao, na ndiyo msimamo wa maulamaa wakubwa waliokuja baada ya wanafunzi wa maswahaba, kama vile: Abu Hanifa, Malik, Shaafiy, Ah'mad bin Hanbal, Abul-Hasan al-Ash'ariy na wengineo katika maimamu wakubwa, kwa hiyo kumuita Ibn Taymiyya na mwanafunzi wake Ibn al-Qayyim kuwa ni maimamu wa Hashawiya Mujasima ni matusi dhidi maimamu hao wote waliotangulia kama tutakavyoona hapo mbeleni Inshaallah.

TUHUMA YA KWANZA

Kisha akasema ndugu Juma katika ukurasa wa 23:
"Falsafa ya Ibn Taymiyya kuhusu maumbile ni kuwa ulimwengu una sifa ya kutangulia kama alivyosema haya katika kitabu chake NAQDU MARATIBIL AL-IJMAA.
Nini maana ya sifa ya kutangulia? Sisi waislamu tunaamini kuwa Mwenyezi Mungu tu ndiye mwenye sifa ya kutangulia, yaani kabla yake hapakuwa na kitu chochote: kila kilichopo tunapopajua na tusipopajua, tunapopaona na tusipopaona basi ni kiumbe cha Mwenyezi Mungu.
Lakini itikadi ya Ibn Taymiyya wanaemwita Sheikh wa waislamu ni kuwa Mwenyezi Mungu alikuwa navyo vitu ambavyo kutokana na hivyo ndio kaanzia kuumba maumbile yote.

Sasa suala ni kuwa hivi vitu vya nani? Je haoni yeye huyu Ibn Taymiyya kuwa falsafa hii inapelekea kurudi kwenye itikadi ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu zaidi ya mmoja?
Huyu ndiye ambaye Mawahabi wanamwita Sheikh Al-islam……".
Mwisho wa kunukuu.

MAJIBU YETU

Maneno yote haya ya ndugu Juma ni maneno ya uwongo yaliyojaa chuki dhidi ya mwanachuoni huyu mkubwa wa kiislamu, si kweli kwamba itikadi ya Ibn Taymiyya ni kuwa ulimwengu una sifa ya kutangulia.
Na wala maneno ya Ibn Taymiyya katika suala hili hayapelekei kwenye dhana ya kuwepo Mungu zaidi ya mmoja, lakini huo ni ufahamu mbaya wa ndugu yetu Juma uliosababishwa na chuki binafsi dhidi ya maulamaa wa Ah'li Sunna hasa Ibn Taymiyya.

Katika kubatilisha madai haya ya uwongo ya Juma, hebu tukunukulie kidogo ndugu msomaji maneno ya Ibn taymiyya yanayohusu masuala haya ya maumbile, amesema Ibn Taymiyya:

"كل ما سوى الرب حادث كائن بعد أن لم يكن وهو- سبحانه – المختص بالقدم والأزلية, فليس فى مفعولاته قديم وإن قدر أنه لم يزل فاعلاً وليس معه شيئ قديم بقدمه, بل ليس فى المفعولات قديم ألبته, بل لا قديم إلا هو –سبحانه- وهو وحده الخالق لكل ما سواه وكل ما سواه مخلوق كما قال – سبحانه- ((الله خالق كل شيئ))" الزمر 26
درء تعارض العقل والنقل 272/8.

"KILA KISICHOKUWA MOLA NI CHENYE KUZUKA KIMEPATIKANA BAADA YA KUTOKUWEPO, na yeye (Allah) –Sub'hanah- ndiye mwenye kuhusishwa na kutangulia na azal, hakuna kitu katika viumbe vyake kilichokuwa ni chenye kutangulia, hata kama ikikadiriwa kuwa yeye (Allah) hakuacha kuwa ni mwenye kutenda, (lakini) hakuna kitu kilichotangulia kwa kutangulia kwake, bali hakuna kabisa

katika viumbe (vyake ambavyo) ni vyenye kutangulia, BALI HAKUNA KILICHOTANGULIA ILA YEYE (ALLAH) – Sub'haanah-.
Na yeye pekeyake ndiye mwenye kukiumba kila kisichokuwa yeye, kila kisichokuwa yeye ni chenye kuumbwa kama alivyosema - Sub'ahaanah-:
((Allah ni muumba wa kila kitu))". Surat Zumar aya ya 26.
Tazama kitabu Dar'u Ta'arudh juzuu ya 8 ukurasa wa 272 cha Ibn Taymiyya.

Ndugu msomaji, je kwa maneno haya umefahamu kwamba Ibn Taymiyya ana itikadi ya kuwa ulimwengu una sifa ya kutangulia kama anavyodai Juma?
Au umefahamu kwamba Ibn Taymiyya anasema kuwa kila kisichokuwa Allah ni chenye kuzuka na kimepatikana baada ya kutokuwepo?
Je kwa maneno haya ya Ibn Taymiyya umefahamu kwamba ana itikadi ya kuwepo Mungu zaidi ya mmoja kama anavyodai ndugu Juma kuwa sheikhul islam Ibn Taymiyya ana itikadi hiyo?
Au umefahamu kwamba ndugu Juma si mkweli?
Hebu yatupie jicho maneno mengine ya Sheikul-Islam Ibn Taymiyya tuone anavyosema:
"كل واحد من أفعاله لا بد أن يكون مسبوقا بالفاعل وأن يكون مسبوقاً بالعدم, ويمتنع كون الفعل المعين مع الفاعل أزلاً وأبداً...فالفاعل يتقدم على كل فعل من أفعاله وذلك يوجب أن كل ما سواه محدث مخلوق".
مجموع الفتاوى 18/227-228.

"Kila kitu katika vitendo vyake hakuna budi kuwa ni chenye kutanguliwa na mwenye kutenda na ni chenye KUTANGULIWA NA KUTOKUWEPO. NA HAIWEZEKANI KUWA KITENDO FULANI KILIKUWEPO PAMOJA NA MTENDAJI TANGU MWANZO NA AZAL.....
Mwenye kutenda (ambaye ni Allah) anakitangulia kila kitendo katika vitendo vyake na hilo linawajibisha kuwa KILA KISICHOKUWA YEYE (ALLAH) NI CHENYE KUZUKA NA NI CHENYE KUUMBWA".

Tazama Maj'muul-Fatawa juzuu ya 18 ukurasa wa 227-228.
Bila shaka maneno haya yako wazi katika kuufichua uwongo wa ndugu Juma na wala hayahitajii maelezo.

TUHUMA YA PILI

Kisha ndugu Juma akaleta tuhuma nyingine dhidi ya Ibn Taymiyya na mwanafunzi wake (Ibn al-qayyim) kuhusiana na suala la sifa za Allah akasema:
"Anasema Ibn Al-qayyim katika kitabu chake "HADI AL-ARWAAH" ukurasa wa 13 akitaja sifa za Mwenyezi Mungu anasema:
"na kwamba yeye (Mwenyezi Mungu) ana mikono miwili bila ya mfano na ana macho mawili na ana uso". Naye Ibn Al-qayyim anasema kuwa kayanukuu maneno haya kutoka kwa Abul-hasan Al-ash'ari....
Lakini kudai kwamba maneno haya ni maneno ya Al-imamu Al-ash'ari ni kitu cha kutazama zaidi kwani wafuasi wa Al-imamu Al-ash'ari nao ni masuni kama mashafi hawakubaliani na haya".
Mwisho wa kunukuu.
Tazama ukurasa wa 24-25 katika kitabu chake "Hoja zenye Nguvu".

MAJIBU YETU

Majibu yetu dhidi ya maneno haya ya ndugu Juma yatakuwa katika nukta kuu tatu:
Nukta ya kwanza:
Suala kuwa Allah ana Mikono miwili bila ya mfano.
Ana Macho mawili bila ya mfano.
Ana Uso bila ya kuwa na mfano.

Hii si itikadi ya Ibn Taymiyya na mwanafunzi wake peke yao, hiyo ndiyo itikadi iliyo elezewa na Qur'an na Sunna na ndiyo itikadi ya maswahaba na wanafunzi wao na ndiyo itikadi ya maimamu wakubwa wa kiislamu.

Amesema Imamu Shaafiy –Allah amrehemu–:

"لله تبارك وتعالى أسماء وصفات جاء بها كتابه وأخبر بها نبيه صلى الله عليه وسلم أمته......أتانا أنه سميع وأن له يدين بقوله ((بل يداه مبسوطتان)).
وقال رحمه الله :
".......وأن له وجهاً بقوله ((كل شيئ هالك إلاّ وجهه)).

"Allah –Tabaaraka Wata'alaah– ana majina na sifa ambazo zimetajwa na kitabu chake na amezielezea Mtume wake –swalla llaahu alayhi wasallam– kwa uma wake...... zimetufikia (habari) kuwa yeye ni mwenye kusikia na ana mikono miwili kwa kauli yake (Allah) : "Bali mikono yake (Mwenyezi Mungu) iwazi".

Na akasema tena (Imamu Shaafiy) –Allah amrehemu–:

".....Na yeye (Allah) ana Uso kwa sababu ya kauli yake (Allah): ((Kila kitu ni chenye kuangamia isipokuwa Uso wake))".

Tazama kitabu "Twabaaqatul-Hanabila" juzuu ya 1 ukurasa wa 283-284 cha Imamu Ibn Abi Ya'ala.

Pia tazama kitabu "Man'haju Imami Shaafiy fi Ith'batil-Aqidah" ukurasa wa 370-378. cha Dkt. Muhammad al-Aqil.

قَالَ أَبُو عِيسَى رحمه الله:
وَقَدْ قَالَ غَيْرُ وَاحِدٍ مِنْ أَهْلِ الْعِلْمِ فِي هَذَا الْحَدِيثِ وَمَا يُشْبِهُ هَذَا مِنْ الرِّوَايَاتِ مِنْ الصِّفَاتِ وَنُزُولِ الرَّبِّ تَبَارَكَ وَتَعَالَى كُلَّ لَيْلَةٍ إِلَى السَّمَاءِ الدُّنْيَا قَالُوا قَدْ تَثْبُتُ الرِّوَايَاتُ فِي هَذَا وَيُؤْمَنُ بِهَا وَلَا يُتَوَهَّمُ وَلَا يُقَالُ كَيْفَ هَكَذَا رُوِيَ عَنْ مَالِكٍ وَسُفْيَانَ بْنِ عُيَيْنَةَ وَعَبْدِ اللَّهِ بْنِ الْمُبَارَكِ أَنَّهُمْ قَالُوا فِي هَذِهِ الْأَحَادِيثِ أَمِرُّوهَا بِلَا كَيْفٍ وَهَكَذَا قَوْلُ أَهْلِ الْعِلْمِ مِنْ أَهْلِ السُّنَّةِ وَالْجَمَاعَةِ.
وَأَمَّا الْجَهْمِيَّةُ فَأَنْكَرَتْ هَذِهِ الرِّوَايَاتِ وَقَالُوا هَذَا تَشْبِيهٌ وَقَدْ ذَكَرَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ فِي غَيْرِ مَوْضِعٍ مِنْ كِتَابِهِ : الْيَدَ وَالسَّمْعَ وَالْبَصَرَ فَتَأَوَّلَتْ الْجَهْمِيَّةُ هَذِهِ الْآيَاتِ فَفَسَّرُوهَا عَلَى غَيْرِ مَا فَسَّرَ أَهْلُ الْعِلْمِ وَقَالُوا إِنَّ اللَّهَ لَمْ يَخْلُقْ آدَمَ بِيَدِهِ وَقَالُوا إِنَّ مَعْنَى الْيَدِ هَاهُنَا الْقُوَّةُ.
و قَالَ إِسْحَقُ بْنُ إِبْرَاهِيمَ إِنَّمَا يَكُونُ التَّشْبِيهُ إِذَا قَالَ يَدٌ كَيَدٍ أَوْ مِثْلُ يَدٍ ......".
انظر جامع الترمذي 1/ 166 رقم الحديث 772.

Amesema Imamu Abu Issa Al-Tirmidhiy –Allah amrehemu- alipoitaja hadithi namba 772:

"Na wamesema wengi katika wanavyuoni kuhusu hadithi hii na inayofanana na hii katika mambo ya sifa (za Allah) na kushuka Mola katika mbingu (iliyokaribu na) dunia, wamesema: zimethibiti riwaya nyingi kuhusu suala hili, na sisi tunaliamini na wala hatusemi kwa dhana na wala hatusemi vipi? Na hivi ndivyo ilivyopokelewa kutoka kwa Malik,Ibn Uyaina, na Abdullahi bin Mubarak kuwa wamesema kuhusu hadithi hizi: zipitisheni bila ya kuzipa namna.

Na hii ndiyo kauli ya wanavyuoni wa Ah'li Sunna wal-Jamaa. Ama Jah'miya wao wamezipinga riwaya hizi na wakasema: huko ni kumfananisha Allah (na viumbe).

Na hali yakuwa ametaja Allah katika kitabu chake katika sehemu nyingi: (ametaja kuwa ana) Mkono, Usikivu, Uoni.

Lakini Jah'miya wakazitafsiri aya hizi tofauti na wanavyuoni, wakasema: Allah hakumuumba Adam kwa mkono wake, na (wakasema kuwa) maana ya mkono hapa ni nguvu.

Na amesema Is'haq bin Ibrahim: inakuwa ni kumfananisha Allah (na viumbe) atakaposema: Mkono (wa Allah) ni kama mkono au mfano wa mkono (wa kiumbe).

Tazama kitabu chake Jamiul-Tir'midhiy/Sunan Tir'midhiy hadithi namba 772.

قال الإمام أبو جعفر محمد بن جرير الطبري [224-310]:
"القول فيما أدرك علمه من الصفات خبراً, وذلك نحو إخباره عز وجل أنه سميع بصير , وأن له يدين بقوله: ((بل يداه مبسوطتان))
وأن له وجهاً بقوله: ((ويبقى وجه ربك)) وأن له قدماً بقول النبي صلى الله عليه وسلم: ((حتى يضع الرب فيها قدمه)) وأنه يضحك بقوله: ((لقي الله وهو يضحك إليه))......".
مختصر العلو للعلي الغفار ص 224.

Amesema Imamu Abu Ja'far Muhammad bin Jarir al-Tabariy aliyefariki mwaka [310 H]:

"Kauli katika yale yaliyofahamika ujuzi wake katika sifa (za Allah) kwa habari, ni mfano wa kuelezea kwake (Allah) -Azza wajalla-

kuwa yeye (Allah) ni mwenye kusikia mwenye kuona, na kwamba yeye (Allah) ana mikono miwili aliposema:
"Bali mikono yake (Mwenyezi Mungu) iwazi".

Na kwamba yeye (Allah) ana Uso pale aliposema:
"Na utabakia Uso wa Mola wako"

Na kwamba yeye Allah ana Mguu, kwa kauli ya Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam–: "Mpaka atakapo weka Mola ndani yake Mguu wake"

Na kwamba yeye (Allah) anacheka kwa kauli yake Mtume:
"Na atakutana na Allah na hali ya kuwa anamchekea".

Tazama kitabu Mukh'tasarul-Uluwi ukurasa wa 224.

قال الإمام أبو بكر الخطيب البغدادي [392-463]:
"فإذا قلنا : يد , وسمع, وبصر ,فإنما هو إثبات صفات أثبتها الله لنفسه , ولا نقول : إن معنى اليد القدرة...".
انظر كتاب " الصفات" للخطيب 16/ 43-44. بواسطة مختصر العلو ص 272.

Amesema Imamu Abu Bakar al-Khatib al-Bagh'dadiy aliyefariki mwaka [463 H]:
"Sisi tunaposema: (kuwa Allah ana) Mkono, Usikivu,na Uoni ni kuthibitisha sifa za Allah kama alivyo jithibitishia mwenyewe, na wala hatusemi maana ya mkono ni uwezo.....".
Tazama Mukh'tasarul-Uluwi ukurasa 272.

Hizi ni baadhi ya kauli za maulamaa wa Ah'li Sunna ambao wamemtangulia Ibn Taymiyya kwa kar'ne nyingi.
Wao wanasema kuwa Allah ana Macho, Mikono miwili, Mguu, n.k. na hiyo ndiyo itikadi ya maimamu wote wanne: Abu Hanifa, Malik, Shaafiy, na Ah'mad bin Habal, sasa kwanini ndugu Juma ainasibishe itikadi hii sahihi na Ibn Taymiyya na mwanafunzi wake Ibn al-Qayyim peke yao?

Kwani kuna kioja gani kwa mtu kumsifia Allah kwa sifa ambazo amejisifia nazo mwenyewe katika Qur'an na amesifiwa na Mtume wake –swalla llaahu alayhi wasallam-?
Je wakumshangaa ni yule aliyehalifu hilo au yule aliyetii? Ama kweli walimwengu wana mambo !

Amesema tena Juma:
"Lakini kudai kwamba haya ni maneno ya Al-imamu Al-ash'ari ni kitu cha kutazamwa zaidi kwani wafuasi wa Al-imamu Al-ash'ari nao ni masuni kama mashafi hawakubaliani na haya".

MAJIBU YETU

Kwa maneno haya ya ndugu Juma anatuwekea wazi zaidi namna asivyokuwa mtafiti mzuri wa mambo na huwa hukumu zake ni za kubuni.

Tangu lini mtu akahukumiwa kwa matendo ya watu wengine?
Kuwa wafuasi wa Abul-Hasan al-Ash'ari wako kinyume na itikadi yake, basi hiyo ndiyo hoja yakwamba hakusema maneno hayo?
Kwanini usiwashangae watu wanaodai kuwa ni wafuasi wa Imamu Shaafiy katika mambo ya twahara na swala lakini katika mambo la itikadi wamemfuata Abul-Hasan na wako kinyume na Imamu wao?
Kwanini wamemkwepa Imamu Shaafiy aliyefariki mwaka 205 H na kumfuata Abul-Hasan al-Ash'ariy aliyezaliwa mwaka 260 H na kufariki mwaka 324 H?
Abul-Hasan yeye amezaliwa nusu karne baada ya Imamu Shaafiy kufariki, je Imamu Shaafiy hakuwa na itikadi yoyote? Na je yeye alikuwa akimfuata nani?

Abul-Hasan al-Ash'ariy jina lake kamili ni: Aliy bin Ismail bin Is'haq bin Salim bin Ismail bin Abdillahi bin Musa bin Abi Bur'da bin Abi Musa al-Ash'ariy, amezaliwa mwaka 260 H.

Mwanzoni mwa uhai wake alikuwa na itikadi ya Mu'tazila kwa muda wa miaka 40 na sababu yakuwa na itikadi hiyo ni sheikh wake aliyesoma kwake ambaye ni baba yake wa kufikia (mume wa mamake) jina lake ni Abu Aliy al-Jubbai, yeye alikuwa na itikadi potofu za Mu'tazila (itikadi za kupinga sifa za Allah) na hiyo ni itikadi iliyo anzishwa na Waasil bin Atwaa.

Kisha Imamu Abul-Hasan akaiwacha itikadi hiyo ya Mu'tazila na kuifuata itikadi ya Ibn Kullaabi kwa muda, na miongoni mwa itikadi za Ibn Kullaabi ni kumthibitishia Allah sifa saba tu, sifa ya: Uhai, Elimu, Uwezo, Utashi, Usikivu, Uoni, na kusema.
Na ama sifa nyingine zote kama vile Uso, Mikono miwili, Mguu na mfano wa hizo alizipa tafsiri potofu.

Alijifungia ndani kwake kwa muda wa siku kumi na tano kisha akatoka akaelekea msikiti mkuu wa Bas'ra akapanda juu ya mimbari baada ya swala ya Ijumaa kisha akawaambia watu, nilijificha kwenu kwa muda kwa sababu nimezitazama dalili lakini zikawa sawa kwangu na haikunipambanukia haki na batili, nikamwomba Allah aniongoze ndipo akaniongoza kwenye haya niliyo yaweka humu kwenye vitabu hivi, na nimejivua na yale yote niliyokuwa nikiyaitakidi kama ninavyoivua kanzu yangu hii, kisha akaivua kanzu yake na akaitupa kwa watu, kisha akavitoa vitabu vyake akawapa watu.

Na miongoni mwa vitabu vyake ni "al-Ibana an Usuli-Diyana" na ndani ya kitabu hicho amesema wazi wazi kwamba msimamo wake huo ndiyo msimamo wa Salaf Swalih msimamo wa maimamu

wakubwa kama vile: Malik, Shaafiy, Ah'mad bin Hanbal na wengineo na kuwalingania watu washikamane nao.

Na wanavyuoni walio lithibitisha suala hili la kutubia kwake, kuacha misimamo hiyo potofu na kushikamana na msimamo wa Salaf Swalih na kuandika kitabu "al-Ibana", ni hawa wafuatao:

1- Abul-Qasim Aliy bin al-Hasan bin Hibatu-llaahi Ibn Asaakir aliyefariki mwaka 571 H, katika kitabu chake "al-Tabyiin" ukurasa wa 28.
2- Imamu al-Baihaqiy al-Shaafiy aliyefariki mwaka 458 katika kitabu chake al-I'tikad ukurasa wa 31na 32.
3- Imamu al-Dhah'biy aliyefariki mwaka 748 H katika kitabu chake "al-Uluwu" ukurasa wa 160.
4- Imamu Ibn al-Imadi aliyefariki mwaka 1098 H katika kitabu chake "Shadharaatul-Dha'hbi" ukurasa wa 303.
5- Imamu Abul-Hasan al-Sayyid Murtaza al-Zabidiy katika kitabu chake "It'hafu Saadatil- Mutaqina" juzuu ya 2 ukurasa 2.
6- Imamu Ibn Kathir al-Qurashiy al-Shaafiy aliyefariki mwaka 774H, katika kitabu chake "al-Bidayatu wal-Nihayah" juzuu ya 11 ukurasa wa 187.
7- Imamu Taaju-Din Abu Nasri Abdul-wahab bin Taqiyu-Din al-Subkiy al-Shaafiy aliyefariki mwaka 771 H, katika kitabu chake "Twabaqaatu al-Shaafi'iya al-Kubraa" juzuu ya 2 ukurasa 246.

Na wengi katika maulama ambao hatukuwataja, wote hao wamekiri na kuthibitisha katika vitabu vyao tulivyo vitaja kuwa Abul-Hasan aliziwacha itikadi zote hizo potofu na kushikamana na itikadi sahihi ya Salaf Swalih na akatunga kitabu "al-Ibana".

YALIYOMO KATIKA KITABU "AL-IBANA"

Hebu tunukuu baadhi ya maneno yake kutoka kwenye kitabu hicho ili tuone je anayoyasema yeye yanatofauti yoyote na yale anayoyasema Ibn Taymiyya na mwanafuzi wake? Au chuki binafsi inafanya kazi yake?

Anasema Abul-Hasan baada ya kuzitaja itikadi potofu za watu wa bid'a na kuzipinga:

"الباب الثاني

فى إبانة قول أهل الحق والسنة

فإن قال لنا قائل : قد أنكرتم قولَ المعتزلة والقدرية والجهمية والحرورية والرافضة والمرجئة , فعرِّفونا قولكم الذي به تقولون وديانتكم التي بها تدينون.

قيل له: قولنا الذي نقول به , وديانتنا التي ندين بها: التمسك بكتاب ربنا عزّ وجل , وبسنَّة نبيِّنا صلى الله عليه وسلم وما روي عن السادة الصحابة والتابعين وأئمة الحديث , ونحن بذلك معتصمون, وبما كان يقول به أبوعبدالله أحمد بن محمد بن حنبل ـنضَّر الله وجهه وفع درحته وأجزل مثوبته- قائلون.....

وجملة قولنا....وأن الله استوى على عرشه كما قال: ((الرحمن على العرش استوى)) طه 5.
وأن له سبحانه وجهاً بلا كيف كما قال: ((ويبقى وجه ربك ذوالجلال والإكرام)) الرحمن 27.
وأن له سبحانه يدين بلا كيف كما قال سبحانه: ((خلقتُ بيَدَيَّ)) ص75.وكماقال: ((بل يداه مبسوطتان)) المائدة:64.
وأن له عيناً بلا كيف كما قال سبحانه : ((تجري بأعيننا)) القمر 14...".

"MLANGO WA PILI

Katika kuibainisha kauli ya watu wa haki na sunna

Ikiwa atasema mwenye kusema : mmeipinga kauli ya Mu'tazila, na kauli ya Qadariya (wenye kupinga Qadari) na kauli ya Jah'miya na kauli ya Haruuriya (miongoni mwao ni maibadhi) na kauli ya Raafidha (Shia) na kauli ya Mur'jia (wenye kuitakidi kuwa watu wote ni sawa katika imani) basi hebu tuelezeeni kauli yenu na msimamo wenu ambao mnaufuata.

Ataambiwa: Kauli yetu tunayoisema na msimamo wetu tunaoufuata ni kushikamana na kitabu cha Mola wetu na Sunna za Mtume wetu –

swalla Ilaahu alayhi wasallam- na yale yaliyopokelewa kutoka kwa mabwana wakubwa katika maswahaba na Taabi'ina (wanafunzi wa maswahaba) na maimamu wa hadithi, sisi ni wenye kushikamana na hilo na yale anayoyasema Abu Abdillahi Ah'mad bin Muhammad bin Hanbal –Allah autie nuru Uso wake na ainyanyue daraja yake na ampe thawabu kwa wingi- sisi ni wenye kuyasema.....

Na jumla ya kauli ni kuwa sisi tunakiri kwamba ....Allah yuko juu ya Arshi yake kama alivyosema: ((Allah mwingi wa reh'ma yuko juu ya Ar'shi)) Twaha aya ya 5.

Na kwamba yeye Allah ana uso bila kuwa na namna kama alivyosema: ((Na utabakia Uso wa Mola wako wenye utukufu)). Al-Rah'man aya ya 27.

Na kwamba yeye ana mikono miwili bila ya kuwa na namna kama alivyosema Allah: ((...Niliye muumba kwa mikono yangu miwili?)) surat Saad (38) aya ya 75.
Na akasema ((Bali mikono yake (Allah) iwazi)) al-Maida aya ya 64.

Na kwamba yeye ana jicho bila kuwa na namna kama alivyosema: ((Linakwenda(jahazi la Nuh) kwa uwangalizi wa macho yetu)) al-Qamar aya ya 14."

Tazama katika kitabu chake "al-Ibana" kuanzia ukurasa wa 38-44, chapa ya Daarul-Bayaan Damascus - Syria ya mwaka 2004.

Bila shaka ndugu msomaji kwa mujibu wa nukuu hizi utakuwa umefahamu kwamba itikadi anayoielezea Ibn Taymiyya ndiyo itikadi halisi ya Ahli Sunna, itikadi ya maimamu wakubwa waliotangulia ambayo ndiyo itikadi iliyoelezwa na kitabu kitukufu Qur'an na Sunna sahihi za Mtume Muhammad –swalla Ilaahu alayhi wasallam-.

Na hiyo ndiyo itikadi ya Imamu Abul-Hasan al-Ash'ariy, kama alivyojielezea mwenyewe katika kitabu chake, kwa hiyo maneno ya ndugu Juma yanayotilia shaka maneno ya Ibn al-Qayyim na kudai kuwa ni maneno ya kutazamwa, madai hayo hayana uzito wowote wa kielimu.

TUHUMA YA TATU

Ndugu Juma hakuchoka kusema uwongo na kuwatuhumu maulamaa wa Ah'li Sunna, bali akaamua kumzushia Imamu Ibn al-Qayyim tuhuma nyingine nzito, amesema ndugu Juma:
"katika kuifasiri aya ya Mwenyezi Mungu inayosema kwamba:

"نسوا الله فنسيهم"

"Wamemsahau Mwenyezi Mungu na yeye akawasahau."

Sura ya 9 aya 67.

Kaifasiri aya hii kuwa ni kusahau kweli kweli akasema: "Zingatia kauli yake Mwenyezi Mungu (katika aya hio na ilio mfano wa hio) namna alivyofanya uadilifu kamili kwao akawasahau kama walivyo msahau !!!".
Mwisho wa kunukuu.
Tazama ukurasa wa 25 wa kitabu chake.

MAJIBU YETU

Miongoni mwa mambo mabaya kabisa katika uislamu ni kumzulia mtu jambo asilolifanya au asilosema, na kama mtu mwenyewe ni mwanachuoni basi ubaya unakuwa maradufu.
Vitendo vya ndugu Juma anavyovifanya dhidi ya maulamaa ni hiyana na ni dhulma ambayo inamporomoshea mtu uadilifu wake na kumfanya asikubaliwe maneno yake.
Je ni kweli Ibn al-Qayyim anasema kuwa Allah anasahau kweli kweli?

Au Juma amekusudia kusema uwongo ili kupotosha?

Jawabu ni kwamba, si kweli kuwa Ibn al-Qayyim anaitikadi kwamba Allah anasahau, bali itikadi yake ni itikadi ya Qur'an na Sunna kuwa Allah hasahau, lakini ndugu yetu Juma alikusudia kupotosha kama ilivyo kawaida ya watu wa batili.

Na ushahidi wa kuwa Ibn al-Qayyim hana itikadi hiyo chafu ni pale alipokuwa akiitafsiri kauli ya Allah isemayo:

" ((علمها عند الله)) طه 52 :
أي أعمال تلك القرون وكفرهم وشركهم معلوم لربي قد أحصاه وحفظه وأودعه فى كتاب فيجازيهم عليه يوم القيامة, ولم يودعه فى كتاب خشية النسيان والضلال فإنه سبحانه لا يضل ولا ينسى "!!!!!
انظر كتابه شفاء العليل ص 141 مطبعة دار الكتاب العربي بيروت – لبنان الطبعة الأولى لعام 1424هـ

"[Ujuzi wake (karne hizo) uko kwa Allah] surat Twaha aya ya 52: Makusudio ni kwamba matendo ya karne hizo (zilizopita) kufru zao na shirki zao zote zinajulika kwa Mola wangu amezidhibiti, amezihifadhi na ameziweka katika kitabu na atawalipa siku ya Qiyama, na hakuziweka katika kitabu kwa sababu ya kuogopea kusahau na kupotea
KWA SABABU YEYE -SUB'HANAH- HAPOTEI WALA HASAHAU!!!!!
Tazama kitabu chake "Shifaul-Alili" ukurasa wa 141 chapa ya Darul-kitabil- Arabi Beirut – Lebanon,chapa ya kwanza mwaka 2004.

Swali, kwa mujibu wa maneno haya, je ndugu msomaji umefahamu kwamba Ibn al-Qayyim itikadi yake ni kuwa Allah anasahau au hasahau?
Je umegundua kwamba Juma al-Mazrui anaendelea kusema uwongo?

Pengine Juma mwenyewe au mtu mwengine katika wapenzi wake anaweza kusema: lakini maneno hayo siyo aliyo yanukuu kutoka kwa Ibn al-qayyim bali yeye amenukuu maneno mengine kwenye kitabu kingine ambayo Ibn al-Qayyim anaelezea kwa uwazi kuwa Allah anasahau kweli kweli.

MAJIBU YETU

Sababu ya kunukuu kauli hiyo ya Imamu Ibn al-Qayyim ni kutaka kukuthibitishia ndugu msomaji kwamba Ibn al-Qayyim hana itikadi hiyo ya kikafiri ambayo ndugu Juma amembabatiza nayo.

Kisha ndiyo tutupie macho hayo maneno ya Ibn al-Qayyim aliyo yanukuu Juma, na tutakapoyatazama tunakuta kwamba Ibn al-Qayyim hakutoka nje ya ibara ya Qur'an na Sunna, na wala maneno yake hayamaanishi kuwa Allah anasahau kweli kweli. Na kama maneno hayo yanaleta maana hiyo, basi hata Qur'an yenyewe na Sunna zitakuwa zina maanisha hivyo.

Ibn al-Qayyim katika maneno yake ametumia ibara isemayo:

"بأن نسيهم كما نسوه"

"Bi an-nasiyahum kamaa nasuuhu"

Maana yake Kiswahili ni "kwa kuwa amewaacha (amewapuuza) wao kama walivyo msahau (walivyompuuza)"

Na ibara hiyo hiyo ndiyo iliyotumika katika Qur'an amesema Allah:

"نسوا الله فنسيهم"

"Wamemsahau Allah naye akawaacha (akawapuuza) ".

Na haya hapa ni maneno ya Ibn al-Qayyim kwa ukamilifu :

"وتأمل قوله الحق ((نسوا الله فنسيهم)) وقوله : ((ولا تكونوا كالذين نسوا الله فأنساهم أنفسهم)) كيف عدل فيهم كل العدل بأن نسيهم كما نسوه".
مختصر الصواعق المرسلة 210/1

“Izingatie kauli yake al-Haq (Allah) “Wamemsahau Allah na yeye akawaacha wao (katika adhabu), na kauli yake “Wala msiwe kama wale ambao wamemsahau Allah na yeye akawasahaulisha nafsi zao” (zingatia) namna alivyo wafanyia wao uadilifu kwa kuwa walimsahau na yeye akawaacha (katika adhabu).”
Tazama kitabu “Mukh'tasaru Sawaaiqil-Mur'slah” juzuu ya 1 ukurasa wa 210.
Hapa nataka kuelezea kitu kimoja muhimu kwa faida ya wasomaji:

Tulipo litafsiri neno “Nasiya hum” kwa maana ya kuacha, lengo si kutaka kuleta taawili na kupotosha.
Bali neno hili la kiarabu “Nasiya” ambalo limetasuliwa (limenyambuliwa) kutoka kwenye asili ya neno “Al-Nis'yaanu” lina maana mbili na zote ni za asili.

Amesema Imamu Abul-Husain Ah'mad bin Faaris aliyefariki mwaka 395 H, katika kamusi yake “Mu'jamu Maqaaisil-Lugha” ukurasa wa 987:

"نسي : النون والسين والياء أصلان صحيحان : يدل أحدهما على إغفال الشيئ , والثاني على ترك شيئ".
معجم مقاييس اللغة ص987.

“Nasiya: Nuni, Siin, na Yaau ni asili mbili zilizo sahihi: moja yao inafahamisha
“Kughafilika” na ya pili ni “Kuacha kitu”.

Kwa hiyo tumefahamu kuwa neno “Nasiya” lina maana mbili:

i) Kughafilika.
ii) Kuacha.

Na kwa mujibu wa kanuni na misingi ya elimu ya itikadi linapotumika neno lolote lenye zaidi ya maana moja: Maana moja

inalingana na utukufu wa Allah, na maana ya nyingine hailingani na utukufu wake Allah, basi neno hili litachukuliwa kwa maana ambayo inalingana na utukufu wake Allah.

Kwamfano hapa limetumika neno "Nasiyahum" ambalo maana yake ima itakuwa :
"(Allah) Amewasahau wao" au "(Allah) Amewaacha wao".
Tukitazama baina ya maana mbili hizi, ni ipi inayonasibiana na utukufu wake Allah –Jalla Jalaaluh-?
Bila shaka kulitumia neno hili kwa maana ya "kuacha" ndiyo sahihi bali ni wajibu kufanya hivyo kwa sababu Allah hasahau kama ilivyotuelezea Qur'an na Sunna na alivyotuelezea Ibn al-Qayyim hapo nyuma.
Na hakuna shaka kwamba naye Ibn al-Qayyim amelitumia neno hili hapa kwa maana inayolingana na utukufu wake Allah, nayo ni kwa maana ya "kuacha".
Na mtu akilitumia neno hili na jingine kama hili kwa utaratibu ule ule uliotumika katika Qur'an au katika Sunna hatakuwa na hatia wala hastahiki lawama, na hivyo ndivyo alivyofanya Ibn al-Qayyim, lakini kwa masikitiko makubwa jambo hili halikumfurahisha ndugu Juma na kaumu yake na wakalifanya hilo ni kosa kubwa lisilo na mfano !
Na -wali llaahil-hamdu- ukirejea sehemu mbali mbali katika vitabu vya Ibn al-Qayyim utaona anavyosema kwa uwazi kabisa kwamba:
فإنه سبحانه لا يضل ولا ينسى "!
"KWA SABABU YEYE (ALLAH) –SUB'HANAH- HAPOTEI WALA HASAHAU" !
Tazama kitabu chake "Shifaul-Alili" ukurasa wa 141 chapa ya Darul-kitabil- Arabi Beirut – Lebanon,chapa ya kwanza mwaka 2004.

Lakini ah ! tutazifanya nini sisi nyoyo zilizonyweshwa chuki, husda na uadui mpaka zikawa hazioni kwa waislamu wenzao ila shari tupu !

Lakini hii ndiyo sera ya watu wote wa bid'a tangu azal.

Ewe Mola wetu usijaalie ndani ya nyoyo zetu chuki na undani dhidi ya ndugu zetu walio amini, Allaahumma Aamin!

TUHUMA YA NNE

Amesema Juma kuhusu Ibn al-Qayyim:

"Na Ibn Al-qayyim akafikia kusema kuwa moto wa akhera kuna siku adhabu yake itakwisha kwa waislamu na wasio kuwa waislamu na utabaki mtupu bila ya mtu yeyote.

Na akainasibisha kauli hii kwa Sheikh wake Ibn Taymiyya na akaisifu kuwa kauli hii ndio inayokubaliana na Qur'an na suna."

Mwisho wa kunukuu. Tazama katika kitabu chake "Hoja zenye Nguvu" ukurasa wa 25.

MAJIBU YETU

Ibn al-Qayyim kwenye kitabu chake "Haadil-Ar'waahi" chapa ya Daarul-Kitabil-Arabi amenukuu mjadala ulio kuwa kati ya pande mbili: upande wa wasemao kuwa moto utakwisha na upande wa wasemao kuwa moto hautakwisha, kwa hiyo yeye kazi yake ilikuwa kunukuu hoja za pande mbili na ndiyo maana utaona anasema:

"والذين قطعوا بدوام النار لهم ست طرق"

"Na wale (wanaosema kwa) kukata kudumu kwa moto wana njia sita".

Tazama "Haadil-Ar'waahi" ukurasa wa 232.

Kisha akasema tena:

"قال أصحاب الفناء....".

"Wamesema wenye kusema kwisha (kwa moto)...." Tazama kitabu "Haadil-Ar'waahi" ukurasa 233.

Na mwisho alipofikia kuufunga mjadala huo akasema:

"Kama ukiulizwa ni wapi umefikia unyayo wenu katika mas'ala haya makubwa, ambayo ni makubwa kuliko dunia kwa mara nyingi?
Ataambiwa : tumefikia kwenye kauli yake –Tabaaraka wata'alaa-:

((إنَّ ربَّك فعَّالٌ لمايريد)) هود:107.

"*Kwa hakika Mola wako ni mwenye kufanya analo litaka....*".
Surat Huud aya ya 107.

Tazama "Haadil-Ar'waahi" ukurasa wa 248.

Mpaka hapo inaonyesha kwamba Ibn al-Qayyim hakuunga mkono hoja ya upande wowote ule.
Lakini ukweli ni kwamba Ibn al-Qayyim amebabaika sana katika mas'ala haya, na hakuwa na kauli ya wazi katika suala hili kwenye kitabu hiki.
Lakini tulipo yafuatilia maneno yake yaliyomo kwenye vitabu vyake vingine tukakuta kuwa ameuweka wazi msimamo wake juu ya mas'ala haya kwa mfano kwenye kitabu chake "Al-Waabilu al-Sayibu" ukurasa wa 49 chapa ya "al-Nasri", iliyohakikiwa na sheikh Ismail al-Ansaariy,amesema Ibn al-Qayyim:

"وأما النار فإنها دار الخبث فى الأقوال والمآكل والمشارب ودار الخبيثين , فالله تعالى يجمع الخبيث بعضه إلى بعض فيركمه كما يركم الشيئ لتراكب بعضه إلى بعض , ثم يجعله فى جهنم مع أهله . فليس فيها إلا خبيث , ولما كان الناس على ثلاث طبقات : طيب لا يشوبه خبث , وخبيث لا طيب فيه , وآخرون فيهم خبث وطيب- كانت دورهم ثلاثة:
دار الطيب المحض ,
ودار الخبث المحض ,
وهاتان الداران لا تفنيان.
ودار لمن معه خبث وطيب وهي الدار التي تفنى , وهي دار العصاة فإنه لا يبقى فى جهنم من عصاة الموحدين أحد , فإنهم إذا عذبوا بقدر جزائهم أخرجوا من النار فأدخلوا الجنة , ولا يبقى إلا دار الطيب المحض , ودار الخبث المحض".

انظر الوابل الصيب ورافع الكلم الطيب ص 49 تحقيق الشيخ إسماعيل الأنصاري, طبعة النصر الحديثة.

"Na ama moto ni nyumba ya uchafu wa kauli na vyakula na vinywaji na ni nyumba ya wachafu, Allah -Ta'alaa- ataukusanya uchafu wenyewe kwa wenyewe kisha aurundike kama anavyorundika kitu ili kipandane chenyewe kwa chenyewe, kisha auweke katika Jahannam pamoja na watu wake.

Hakuna katika Jahannam ila uchafu. Na kwa vile wamekuwa watu katika tabaka tatu:

Usafi usio changanyikana na uchafu.

Na uchafu usio changanyika na usafi.

Na wengine wana uchafu na usafi.

Basi yamekuwa makazi yao pia ni (namna) tatu :

Makazi ya wasafi watupu (Peponi)

Makazi ya wachafu watupu (Motoni)

Na makazi haya mawili (Pepo na Moto) HAYATAKWISHA.

Na makazi ya wale walio na uchafu uliochanganyika na usafi ni makazi ambayo yatakwisha, nayo ndiyo makazi ya waliofanya maasia miongoni mwa waislamu. Na hatabakia katika Jahannam yeyote katika waislamu waliofanya maasia, wataadhibiwa kwa kiasi cha malipo yao kisha watatolewa motoni kisha wataingizwa peponi na, HAYATABAKIA ILA MAKAZI YA WATU SAFI (PEPO) NA MAKAZI YA WATU WACHAFU (MOTO)".

Kwa maneno haya ya Ibn al-Qayyim tunapata faida kwamba huko akhera watu watakuwa katika makundi matatu:

1- Kuna watu wema walio safi kabisa, hawa makazi yao ni katika Janna (peponi).
2- Kuna watu waovu walio wachafu kabisa nao ni makafiri, hawa makazi yao ni Jahannam (motoni).
3- Na kuna watu ambao wamechanganya wema na uovu, na asili yao ni waislamu, hawa wataadhibiwa motoni kwa kadiri

ya amali zao kisha watatolewa motoni na moto wao utazimwa.

Ama kundi la kwanza watu wa peponi wataishi katika neema za milele bila ya ukomo wala kwisha.
Na kundi la pili ambao ni makafiri wao wataadhibiwa motoni milele bila ya ukomo wala adhabu zao hazitakwisha.
Na hiyo ndiyo itikadi ya Imamu Ibn al-Qayim –Rahimahu llaahu-
Kama utakuwa ndugu msomaji umesoma maneno yake kwa umakini, basi utakuwa umepata jawabu la kukutosha.
Halikadhalika yamenukuliwa maneno kutoka kwa sheikh wake sheikhul-islam Ibn Taymiyya kwamba anaitikadi hiyo, lakini kauli iliyo na nguvu ni kuwa msimamo wa Ibn Taymiyya na mwanafunzi wake Ibn al-Qayyim katika suala hili na mengineyo ni msimamo wa Salaf Swalih (wema walio tangulia).
Amesema Ibn Taymiyya:

"فإن نعيم الجنة , وعذاب النار دائمان , مع تجدد الحوادث فيهما".
منهاج السنة النبوية 146/1.طبعة جامعة الإمام محمدبن سعود الإسلامية 1406هـ.

“Kwa hakika neema za peponi na adhabu za motoni ni zenye kudumu, pamoja na kupata upya vyenye kuzuka ndani yake”.
Tazama kitabu chake “Min’haajus- Sunna” kilicho chapishwa katika chuo kikuu cha Imamu Muhammad bin Su’ud al-Islamiyah – Riyadh ya mwaka 1406 H.

وقال رحمه الله:
" وقد اتفق سلف الأمة وأئمتها وسائر أهل السنة والجماعة على أن من المخلوقات ما لا يعدم ولا يفنى بالكلية كالجنة والنار والعرش وغير ذلك ولم يقل بفناء جميع المخلوقات إلاّ طائفة من أهل الكلام المبتدعين كالجهم بن صفوان ومن وافقهم من المعتزلة ونحوهم وهذا قول باطل يخالف كتاب الله وسنة رسوله وإجماع سلف الأمة وأئمتها".
بيان تلبيس الجهمية 581/1 طبعة دار القاسم – الرياض .ومجوع فتاوى ابن تيمية308/18 مكتبة المعارف , الرياض.

Amesema Ibn Taymiyyah -Allah amrehemu-:
“Wameafikiana waliotangulia na maimamu wao na Ahli-Sunna wal-Jamaa wote kwamba kuna viumbe havitakwisha wala kutoweka kabisa, kama vile pepo,moto na vinginevyo.
Na hawakusema kuwa vitatoweka vitu vyote isipokuwa kundi la watu wa falsafa katika wazushi kama vile Jah’mi bin Saf’wan na wale waliomuafiki miongoni mwa Mu’tazila na mfano wao.
Na hii ni kauli batili ambayo inatofautiana na kitabu cha Allah na Sunna za Mtume wake na maafikiano ya walio tangulia katika uma huu na maulamaa wake”.
Tazama kitabu chake “Bayaanu Talbisul-Jah’miya” juzuu ya 1 ukurasa wa 581, kilicho chapishwa na Daarul-Qasimi- Riyadh, pia tazama “Maj’muu Fatawa” juzuu ya 18 ukurasa wa 308.

Kwa maneno haya ya Ibn Taymiyya tumefahamu kuwa:
Msimamo sahihi wa Ah’li Sunna ni kuwa pepo na moto havitakwisha Abadan.
Na msimamo wa watu wa bid’a ni kuwa pepo na moto vitakwisha.
Na msimamo huu wa kuwa moto utakwisha ni msimamo batili kwa mtazamo wa Ibn Taymiyya.
Kwa hiyo bila shaka msimamo wa Ibn Taymiyya katika jambo hili ni huo huo msimamo wa Ah’li Sunna kwamba pepo na moto havitokwisha na ndiyo maana akaubatilisha msimamo wa wale wanaodai kuwa vitu hivyo vitakwisha.
Tena hasa ukizingatia kuwa maneno haya yamo katika kitabu kinachohesbiwa kuwa ni miongoni mwa vitabu alivyoviandika mwishoni mwa umri wake “Bayaanu Talbisil-Jah’miya”.

وقال رحمه الله:
"وهذا الذي يذكره كثير من أهل الكلام الجهمية ونحوهم فى الإبتداء نظير ما يذكرونه فى الإنتهاء من أنه تفنى أجسام العالم حتى الجنة والنار....وهذا الذي ابتدعه المتكلمون باطل باتفاق سلف الأمة وأئمتها".
بيان تلبيس الجهمية 1/152-153 , طبعة دار القاسم – الرياض الطبعة الثانية.

Amesema Ibn Taymiyya:

"Na haya ambayo wanayataja watu wengi miongoni mwa wanafalsafa waki-Jah'miya na mfano wao kuhusu mwanzo kuwa ni mfano wa mwisho na kwamba viwiliwili vya walimwengu vitakwisha hadi pepo na moto pia...... haya waliyo yazua wanafalsafa ni batili kwa itifaki ya waliotangulia katika uma huu na maimamu wake".

Tazama kitabu chake Bayaanu Talbisul-Jah'miya" juzuu ya 1 ukurasa wa 152-153 kilicho chapishwa na Daarul-Qasimi- Riyadh.

Hapa Ibn Taymiyya anatuambia kuwa kauli ya wanafalsafa ya kudai kwamba vitu vyote vitakwisha na kutoweka kabisa, tena mpaka pepo na moto madai hayo ni batili.

وقال رحمه الله:

"ثم أخبر ببقاء الجنة والنار بقاءً مطلقاً ولم يخبرنا بتفصيل ما سيكون بعد ذلك...".

بيان تلبيس الجهمية 157/1.

Amesema tena Ibn Taymiyya:

"Kisha (Allah) akatuelezea kubakia pepo na moto kubaki kwa it'laki (bila ya kuwa na mwisho) na wala hakutuelezea upambanuzi wa yale yatakayo kuwa baada ya hapo...".

Tazama kitabu hicho hicho juzuu ya1 ukurasa 157.

Hapa Ibn Taymiyyah anatuambia kuwa; maandiko yamekuja kutuelezea kuwa pepo na moto zitabakia milele, na wala hayakutuelezea yatakayo tokea baada ya hapo.

SURA YA TATU

CHANZO NA CHIMBUKO LA UPOTEVU

Ndugu msomaji kama utakuwa ni mfuatiliaji mzuri wa mambo ya dini yetu hii ya kiislamu na ukawa unashughulishwa na kufuatilia matatizo yanayo usibu umma huu mtukufu, bila shaka utaziona athari za wazi wazi za tofauti za wafuasi wa dini hii tukufu, tena baadhi ya tofauti ni zile tofauti nzito ambazo huwezi kutoa hukumu kwamba wote hao waliotofautiana wako katika haki.

Na pengine unaweza kujiuliza ni nini sababu zilizowaingiza watu hawa katika tofauti hizi na itikadi potofu na batili?

Ndugu Juma M. Al-Mazrui yeye anadai kwamba chanzo cha watu kutumbukia katika itikadi za batili:

"Ni kukanusha kwao kuwepo kwa MAJAZI katika lugha ya kiarabu na hasa katika Qur'an".

Tazama kitabu chake "Hoja zenye Nguvu" ukurasa wa 32.

Bila shaka sababu hii aliyoitoa si sababu ya msingi wala haina uzito wowote kwa mtazamo wa kisheria, na hakuna muislamu yeyote yule, awe msomi au hata asiye msomi atakayekubaliana naye na hii sababu aliyoitoa, kwa kuwa ni sababu dhaifu ambayo haikuchunga vigezo vya kisheria.

Sisi kwa upande wetu tunasema kwamba:

Chanzo kikuu na chimbuko la kupotea kwa watu wengi mpaka kufikia kuingia katika itikadi potofu ni kuacha kuifuata njia ya Mtume Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam- na kuuacha mwenendo sahihi wa wema waliotangulia katika kuifahamu dini.

Na hili ni jambo ambalo Allah na Mtume wake -swalla llaahu alayhi wasallam -wamelitahadharisha kwa ukali mno.

Amesema Allah:

ومن يشاقق الرسول من بعد ما تبين له الهدى ويتبع غير سبيل المؤمنين نوله ما تولّى ونصله جهنم الآية ...

“Na atakayemwasi Mtume baada ya kumdhihirikia uwongofu na AKAFUATA NJIA ISIYOKUWA YA WAUMINI,tutamuelekeza aliko elekea, na tutamuingiza katika Jahannamu….. ”.

Surat An Nisaa aya ya 115

Kama utaizingatia aya hiyo hapo nyuma, utagundua kuwa kufuata njia isiyokuwa ya waumini ni moja miongoni mwa vyanzo vya upotevu katika umma huu.

Na hapana shaka kuwa, hakuna waumini waliokusudiwa hapo zaidi ya wale ambao Allah ametangaza kuwapa radhi zake, wao na wote wenye kufuata nyendo zao kwa wema pale aliposema:

وَالسَّابِقُونَ الأَوَّلُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالأَنصَارِ وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُم بِإِحْسَانٍ رَّضِيَ اللّهُ عَنْهُمْ وَرَضُواْ .. عَنْهُ.

“Na wale waliotangulia,wakwanza katika Muhajirina na Answaari, na wale waliowafuata kwa wema, Allah ameridhika nao, na wao wameridhika naye…. ”.

Suratul-Tawba aya ya 100.

Na kwa hakika isiyopingika hakuna wengine waliokusudiwa na haya hii zaidi ya Maswahaba ambao Allah amewataka watu wote wamuamini yeye Allah kama walivyomuamini watu hao pale aliposema:

"وإذا قيل لهم ءَامِنوا كما آمن الناس قالوا أنؤمن كما آمن السفهآء"

“Na wanapoambiwa:aminini KAMA WALIVYOAMINI WATU wanasema;hivi tuamini kama walivyoamini wapumbavu?… ”.

Suratul Baqarah aya ya 13.

Na amesema tena Allah:

"فإن آمنوا بمثل مآ ءَامنوا به فقد اهتدَوا وإن تولّوا فإنما هم فى شقاق"

“Basi wakiamini KAMA MLIVYOAMINI NYINYI (maswahaba) basi watakuwa wameongoka.Na wakikengeuka basi wao wamo katika upinzani”.

Suratul Baqarah aya ya 137.

Pamoja na kuwa aya hizi tulizozitaja zinaeleza kwa uwazi ulazima wa kuifuata njia ya hao wema na kuwatahadharisha watu kufuata njia nyinginezo ambazo ndiyo chanzo cha upotevu wa watu na hatima yake ni kuingia motoni, lakini kwa makusudi kabisa ndugu Juma M. Al-Mazrui kaamua kuzifumbia macho aya hizo na kuzikwepa, kisha akaamua kuunda sababu nyingine ambazo ukizitazama kwa makini utagundua kuwa si sababu za msingi wala hazina uzito wowote katika mizani ya kielimu.

Pia ndugu Juma alitangulia kusema:
"Na umma huu nao sasa umefika mbali katika kuitakidi mambo ya upotovu.Na chanzo chake ni itikadi mbili:
moja ni kuamini kuwa Mwenyezi Mungu ataonekana,na la pili ni kuamini kuwa watu wataingia motoni kukoshwa dhambi zao tu:kisha wataingizwa katika pepo".
Tazama kitabu chake hicho ukurasa wa 17.

Ndugu Juma pia anadai kwamba miongoni mwa vyanzo vya upotevu ni watu kuitakidi kuwa Allah ataonekana huko akhera kwa macho. Na kadhalika kuitakidi kuwa waislamu waliomuasi Allah wataingia motoni kisha watatolewa !?

Itikadi zote hizi ambazo ndugu Juma ameziita kuwa ni vyanzo vya upotevu zimetajwa na Qur'an na Sunna sahihi za Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- na ndiyo itikadi ya Maswahaba wa Mtume Muhammad –swalla llaahu alayhi wasallam- na wafuasi wao walio wafuatia kwa wema.
Juma hakusema kwamba vyanzo vya upotevu ni:
Kutoshikamana na Qur'an na Sunna,
Kumtii shetani na askari wake,
Kufuata matamanio ya nafsi,Ujinga,Kiburi,
Kufanya is'rafu katika matumizi ya majazi ndani ya Qur'an, na kuzipotosha tafsiri za baadhi ya aya kwa madai kuwa kuna majazi.

Na nyinginezo miongoni mwa sababu zilizotajwa na Qur'an au Sunna.
Bali yeye ameamua kutaja mambo hayo kuwa ndiyo vyanzo vya upotovu, na hali ya kuwa yeye mwenyewe ana yakini kwamba hawezi kututhibitishia kielimu kwamba itikadi hizo ni vyanzo vya upotevu kivipi?

Lakini ninazidi kuamini kuwa upofu ni upofu wa moyo ! Ee Mola wetu tukinge na upofu wa macho na moyo –Aamin-.

Ama kuhusu suala la majazi kuwepo kwake ndani ya Qur'an au kutokuwepo tutalitolea ufafanuzi kwa muhtasari katika sehemu hiyo ifuatayo inshaallah:

UCHAMBUZI YAKINIFU JUU YA SUALA LA MAJAZI

Ama madai ya kwamba umma umeingia katika upotevu kwa sababu ya kuitakidi kuonekana Allah kwa macho huko akhera ni madai batili kwa hoja tutakazo zitoa katika kitabu chetu hiki Inshaallaah.
Na ama kuitakidi kwamba kuna waislamu ambao wataingia motoni kisha watatoka kwa sababu ya shafaa (uombezi):

Suala hili limethibiti kwa hoja zenye nguvu katika kitabu (Qur'an) na sunna sahihi za bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam-.

Ama madai yake ya uwongo kuwa suala la kupinga kuwepo kwa majazi ndani ya Qur'an kuwa ndiyo chanzo cha kupotea watu, ufafanuzi wake ni kama ufuatavyo:

Suala kuwepo majazi na kutokuwepo kwake katika Qur'an na lugha ya kiarabu ni jambo ambalo maulamaa wametofautiana tangu zamani kama walivyotofautiana katika mambo mengine.

Ndugu Juma Al-Mazrui katika kitabu chake "Hoja zenye Nguvu" ukurasa wa 32 amefanya jaribio la kutaka kuuficha ukweli huo ambao uko wazi tena mbele ya macho yake na akafanya upotoshaji kwa makusudi dhidi ya watu anaowaita Mawahabi (akiwa ana wakusudia Ahlu sunna wal Jamaa) kwa kudai kwamba watu hao wamepotea, na chanzo cha upotevu wao huo ni kukanusha kuwepo kwa majazi katika lugha na Qur'an.

Amesema ndugu Juma al Mazrui baada ya kichwa cha habari kisemacho:

"CHANZO CHA KUTUMBUKIA KATIKA ITIKADI BATILI

Kisha akasema:
"Sababu kubwa na chanzo cha Mawahabi kuwa na itikadi hizi za kumfananisha Mwenyezi Mungu na viumbe, wakasema kuwa Mwenyezi Mungu ana mikono, miguu, uso, macho...ni kukanusha kwao kuwepo kwa majazi katika lugha ya kiarabu na hasa hasa katika Qur'an.
Miongoni mwa walioandika kwa urefu na kukataa jambo hili ni Ibn Qayyim Al-jawziyya katika kitabu chake "MUKHTASAR AL-SAWAAIQ AL MURSALA"....
Na maana ya "majazi"ni kutumika neno tafauti na maana yake ya asili...
Sasa wao Mawahabi wanakataa kuwa katika Qur'an hakuna majazi".
Mwisho wa kunukuu.

Majibu yetu yatakuwa katika nukta tatu:
Nukta ya kwanza:
Ni kuhusu maelezo yake kuhusu neno "Majazi",kwa ufupi ni kwamba maelezo ya Juma kuhusu majazi yana upungufu alitakiwa aseme hivi: "Majazi ni kutumia neno katika isiyokuwa maana yake ya asili pamoja na kuwepo dalili inayozuia kukusudiwa maana yake ya asili kwa mafungamano ambayo yapo baina ya neno la asili na neno ambalo si la asili.

Kwa sababu ili maneno yawe ni majazi, ni lazima masharti matatu makuu yatimie, nayo ni:

1-Kutumika neno katika isiyo kuwa maana yake ya asili.
2-Lazima kuwepo na "QARINATUN MAANI'ATUN MIN IRADATI MA'ANAL ASLIY" dalili yenye kuzuia kukusudiwa maana ya asili.

3-Lazima kuwepo na "ALAAQAH"mafungamano baina ya neno la asili na neno lisilo la asili.
Na likikosekana sharti moja kati ya haya matatu tuliyoyataja basi hakutakuwa na majazi na atakayedai kuwa ni majazi basi huyo ni mwongo mkubwa na hajui lugha ya kiarabu.

Kwa mfano nikisema: "Nimemuona Simba anamla Swala".
Kwa mujibu wa misingi ya lugha ya kiarabu neno "Simba"hapa limetumika katika maana yake ya asili.
Kwa sababu katika maneno haya hakuna "QARINATUN MAANI'ATUN MIN IRADATI MA'ANAL ASLIY" dalili yenye kuzuia kuikusudia maana ya asili.

Na yanapotamkwa maneno hayo kila mwenye kusikia atakuwa ameelewa moja kwa moja kwamba simba aliyekusudiwa hapo ni simba mnyama mkali wa porini na wala sivinginevyo.

Lakini mtu akisema; "nimemuona simba kwenye uwanja wa mapambano ameshika upanga".
Bila shaka hakuna atakayedhania kwamba simba aliyekusudiwa hapa ni yule mnyama pori, na sababu iliyozuia mtu asidhanie hivyo ni kauli ya msemaji; "ameshika upanga" maana simba asili hawezi kushika upanga, bali huyo ni mtu shujaa aliyefananishwa na simba kwa sababu ya ushajaa wake.
Kwa hiyo kusema tu;kwamba majazi ni kutumia neno tafauti na maana yake ya asili,ni makosa kwa sababu tulizozitaja.

Nukta ya pili;
Sina shaka kuwa ndugu Juma na wengineo katika watu wa bid'a wanapokuwa wanataja neno;"Mawahabi" huwa wanawakusudia AHLU SUNNA WAL-JAMAA, nao ni wale ambao wanaziunga mkono hoja na dalili na kazi ya daawa alioifanya Sheikhul Islaam Muhammad bin Abdul Wahaab ambaye amezaliwa mwaka 1115 H na kufariki mwaka 1206 H.
Swali, Je ni kweli kwamba hao ambao ndugu Juma anawaita mawahabi ndio wanaopinga majazi?

Maulamaa ambao wanapinga kuwepo kwa "Majazi" wako katika makundi mawili:
a) wanaopinga kuwepo kwa majazi katika lugha na Qur'an.
b) wanaopinga kuwepo kwa majazi katika Qur'an tu.

a) Hawa wafuatao ni baadhi ya maulamaa waliopinga kuwepo kwa majazi katika lugha ya kiarabu na halikadhalika katika Qur'an:

1- Imamu Abu Is'haaq Ibrahim bin Muhammad bin Mih'raan Al-Is'fraayiiniy Al-Shaafiy aliyefariki mwaka 418 H.

2- Imamu Abu Aliy Al Hassan bin Ahmad bin Abdil-Ghaffaar Al-Fasawiy aliyefariki mwaka 377 H.

3-Sheikhul Islaam Abul Abbaas Ahmad bin Abdul-Haliim Ibn Taymiyyah aliyefariki mwaka 728 H.
4-Shamsud Din Abu Abdillahi Muhammad bin Abi Bakar mashuhuri kwa jina la Ibnul Qayyim al Jawziyyah aliyefariki mwaka 751 H.

b) Na hawa wafuatao ni maulamaa ambao wamepinga kuwepo kwa majazi ndani ya Qur'an tu, lakini wakathibitisha kuwepo kwake katika lugha ya kiarabu:

1-Muhammad bin Ahmad bin Abdillahi mashuhuri kwa Ibn Khuwayz Min'daad katika maulamaa wa madhehbu ya Ki-Maalik.

2-Imamu Abul Abbaas Ahmad bin Ahmad Al-Twabariy Al-Shaafiy mashuhuri kwa Ibnul-Qaadhiy aliyefariki mwaka 335 H.

Ndugu msomaji kama ukiutazama kwa makini mwaka aliozaliwa Sheikh Muhammad bin Abdil-Wahab na mwaka waliokufa maulamaa hawa tuliowataja utagundua kwamba ndugu Juma al-Mazrui ni mwongo.

Kwa mfano,baina ya Sheikh Muhammad bin Abdil Wahaab aliyezaliwa mwaka 1115 H na kufariki mwaka 1206 H na baina ya Imamu Abu Is'haaq al Isfraayiiniy aliyefariki mwaka 418 H, ambaye ni miongoni mwa wanaopinga kuwepo kwa "Majazi" utaona kuwa baina yao kuna miaka takriban 697, kabla ya kuzaliwa huyo wanaedai kuwa ndiyo muasisi wa huo uwahabi! Kwa miaka hiyo tayari upingaji wa majazi ulikuwepo duniani.

Sasa utasemaje kwamba Mawahabi wanapinga majazi na hali yakuwa huyo muasisi wa huo mnaouita uwahabi amezaliwa miaka 697 baada ya kauli hiyo ya kupinga majazi ? au unataka kutuambia kwamba Imamu Abu Is'haaq Al-Isfraayiiniy alifufuka baada ya kuzaliwa Muhammad bin Abdul-wahab kisha akamfuata sheikh Muhammad bin Abdil-wahab ?
Au mnataka kutuambia kuwa hawa nao pia ni Mawahabi?

JE WENYE KUPINGA MAJAZI WANA HOJA ZA KIELIMU?

Jambo muhimu la kulizingatia ni; je hao maulamaa waliopinga kuwepo kwa majazi, wamepinga kwa hoja na dalili za kielimu? Au ni kwa maneno matupu?
Jawabu ni kama ifuatavyo:
Ukirejea kauli za maulamaa hao waliopinga kuwepo kwa majazi ima katika lugha ya kiarabu na Qur'an, au katika Qur'an tu, utagundua kwamba kuna hoja za msingi walizozitoa ambazo haitakiwi kuzipuuza, bali inatakiwa zitazamwe kielimu na kwa jicho la insafu.
Hizi zifuatazo ni baadhi ya hoja zao:

HOJA YAO YA KWANZA

Miongoni mwa hoja zao zinazowafanya kupinga kuwepo majazi katika lugha na halikadhalika katika Qur'an, ni kuwa maana ya maneno hufahamika kwa kuutazama mtiririko au muktadha (context) na dalili za uhalisia.
Pia wakadai kuwa neno linapokuwa peke yake halileti maana kamili mpaka liwe katika sentensi, na linapo unganishwa katika sentensi huwa ule mtirirko wa maneno ndio unao ainisha maana husika ya neno hilo.

Mfano, neno "رأس" "Ra'asun" lina maana nyingi, lakini maana zote zinaainishwa na mtiririko wa maneno, kwa mfano mtu akisema:
Ra'asul-Jabali, atakuwa hapa anakusudia kilele cha mlima.
Na kama atasema:
Ra'asul-Maali, atakuwa anakusudia msingi wa mali au rasilimali.
Na kama atasema:
Ra'asul-Insaani, atakuwa anakusudia kichwa cha binadamu.
Na maana zote za neno hili zimeanishwa na mtirirko wa maneno, na wala hakuna binadamu yeyote anaeweza kututhibitishia kwa hoja na dalili kwamba maana ya asili ya neno "Ra'asi" ni kichwa cha binadamu, na katika sehemu nyingine zote ni Majazi.

HOJA YAO YA PILI

Itifaki iliyopo baina ya maulamaa wa lugha ya kiarabu kwamba mtu anaweza akayapinga maneno ambayo yanadaiwa kuwa ni majazi. Na kwa wakati huo huo akawa huyo mpingaji ni mkweli na yule mwenye kudai kuwa maneno hayo ni majazi pia akawa ni mkweli.

Kwa mfano mtu akisema kwa kutumia majazi:

"Nimemuona simba ameshika upanga" akiwa anamkusudia mtu shujaa, kama akitokea mtu mwingine akisema huo ni uwongo! huyo uliemuona wewe si simba, bali ni mtu shujaa, anakuwa huyu mwenye kutumia majazi ni mkweli na wakati huo huo huyu aliyepinga naye pia ni mkweli !

Kwa sababu hiyo wakasema wenye kupinga majazi:

Kwa mujibu wa itifaki hiyo ni kwamba mtu akisema kwamba ndani ya Qur'an kuna majazi atakuwa moja kwa moja ameshasema kuwa ndani ya Qur'an kuna vitu ambavyo kuna uwezekano wa mtu

akasema kuwa ni uwongo na akawa huyo msemaji kwa wakati huo ni mkweli !

Na bila shaka hilo si sahihi kwa itifaki ya waislamu wote, kwa sababu wamekubaliana waislamu wote duniani tangu hapo kale hadi sasa kwamba hakuna kitu chochote ambacho kiko ndani ya Qur'an kinachofaa kukipinga bali ukiipinga herufi moja tu utakuwa tayari umekufuru.
Na hii itikadi ya kuwepo kwa Majazi ndani ya Qur'an inawafungulia watu mlango wa kuliingia jambo hilo la hatari.

Kwa mfano, pale aliposema Allah:

وجاء ربك والملك صفاً صفاً

"Na akaja Mola wako na Malaika safu safu".

Suratul-Fajri (89) aya ya 22.

Baadhi ya watu wakaigeuza maana ya aya hii wakasema hapana, hatakuja Mola Muumba wa kila kitu, bali itakuja amri yake!

Kwa madai kwamba eti kuna "Majazul-Hadh'fi" majazi ya kuondosha kwa hiyo kuna kitu kimeondoshwa.
Na kitu kilichowapa ujasiri wa kukana kwao kuja kwa Allah siku ya Qiyama ni pale walipofunguliwa mlango huo na hicho kitu kiitwacho "Majazi".

Kwa mfano, ukiwauliza kwa nini mmekimbilia kuitakidi kwamba hapo kuna majazi ? Na hali yakuwa majazi si asili na hairuhusiwi kuiwacha asili na kukimbilia kwenye majazi mpaka itakapo shindikana maana ya asili?

Wanadai kuwa asili imeshindikana, kwa sababu Allah hawezi kuja, na kitendo cha kuja kinaonyesha kuwa Allah ana mahali na hiyo ni

sifa ya kiwiliwili, na kumpa Allah sifa hiyo ni kumfananisha na viumbe na kufanya hivyo ni kufru!!!

Madai haya si sahihi, kwa sababu kwanza, inatakiwa kukithibitisha kile ambacho Allah amejithibitishia nafsi yake kama anavyo stahiki, pamoja na kumtakasa na kufanana na viumbe, kama tutakavyo lifafanua suala hili mahali pake Inshaallah.

HOJA ZA WENYE KUTHIBITISHA MAJAZI

Wakajitetea wenye kuthibitisha kuwepo majazi ndani ya Qur'an kwa kusema:
Majazi ni sehemu katika fasihi za lugha ya kiarabu, na hii Qur'an imeshuka kwa lugha ya kiarabu.
Na kila ambacho kinafaa kuwepo katika lugha ya kiarabu kinafaa kuwemo ndani ya Qur'an.
Na miongoni mwa mambo yaliyomo ndani ya lugha ya kiarabu ni haya majazi.
Kwahiyo, tunapata natija kwamba "Majazi" yamo katika Qur'an.

MAJIBU YA WENYE KUPINGA

Wakawajibu wenye kupinga kuwepo majazi ndani ya Qur'an kama ifuatavyo:
Tumewakubalia (AL-MUQADDIMATU AL-SUGH'RAA) kwamba majazi yamo katika lugha ya kiarabu, lakini hatuwakubalii (AL-MUQADDIMATUL-KUBRAA) kwamba kila kilichomo katika lugha ya kiarabu kinafaa kuwemo ndani ya Qur'an, bali sisi tunasema kinyume chake, kwamba; kuna baadhi ya vitu vimo katika lugha ya kiarabu, lakini havifai bali ni haramu kuitakidi kuwemo ndani ya Qur'an.

Kwa mfano;

Katika elimu ya balagha sehemu ya Badi'i katika sehemu ya "Muhassinaatul-Ma'anawiyyah" (vitu vyenye kupendezesha maana), kuna kitu kinachoitwa "AL-HAZ'LU" (mzaha/utani).

Kitu hiki kimo ndani ya lugha ya kiarabu, lakini huwezi kusema kwamba maadamu kimo kwenye lugha, basi kinafaa kuwemo ndani ya Qur'an, kwa sababu Allah anasema kuhusu Qur'an:

إنه لقولٌ فصلٌ *وما هو بالهزل

"Kwa hakika hii (Qur'an) ni kauli kupambanua (13) Na wala si mzaha (14)".

Suratul-Twaariq (86) aya ya 13-14

Miongoni mwa fani za lugha ya kiarabu ni suala la utani, lakini ndani ya Qur'ani hakuna utani na mwenye kuitakidi kuwa katika Qur'an kuna utani atakuwa tayari amekufuru.

Halikadhalika ndani ya lugha ya kiarabu kuna kitu katika milango ya elimu ya balagha kiitwacho "al Ruju'u" kujirudi, msemaji anaweza kusema neno halafu hapo hapo anajikadhibisha mwenyewe kwa kuwa alisema maneno hayo bila ya uhakika, kutokana na kuweweseka, au hofu, au kuzidiwa na mapenzi n.k.

Halikadhalika kuna kitu kitachoitwa "Hus'nu Ta'alili" kutoa sababu ya kitu ambayo si halisia.

Mfano mtu akisema: Mvua imenyesha mjini kwetu kwa sababu ya kutuona haya.

Mambo haya na mengineyo ambayo sikuyataja, yamo katika lugha ya kiarabu lakini hayamo na wala hayafai kuwemo katika Qur'an, bali kuitakidi kuwemo ndani ya Qur'an ni ukafiri.

Kwa hiyo madai ya kwamba kila kilichomo kwenye lugha ya kiarabu kinafaa kuwemo ndani ya Qur'an, madai hayo hapa yanaporomoka.

Na kwa kuzitumia njia za kimantiki (logic) wanasema kwamba;

"نقض الكلية الموجبة جزئية سالبة"

"Kichanguzi cha Kulliyyatun Muujibah" ni "Juz'iyyatun Saalibah"
Kwamfano;
"Kulliyatun Muujibah" kama vile ukisema: kila ambacho kimo kwenye lugha ya kiarabu kinafaa kuwemo katika Qur'an.

Maneno hayo yanavunjwa na "Juz'iyyatun Saalibah" ambayo ni kusema:
Kuna vitu vingi vimo katika lugha ya kiarabu lakini havifai kuwemo kwenye Qur'an.
Na msingi huu (Juz'iyyatun Saalibah" ukithibiti kwa hoja basi msingi huo wa kwanza (Kulliyyatun Muujibah) unaporomoka.
Na hapo nyuma tumekuthibitishia kuwepo katika lugha ya kiarabu vitu vingi ambavyo kudai kwamba vimo ndani ya Qur'an ni haramu.

Tazama maelezo hayo kwa urefu zaidi katika kitabu "Man'u Jawazil-Majaazi" cha Imamu wa tafsiri katika zama hizi Sheikh Muhammad al-Amin bin Muhammad al-Shin'qitwiy.

HOJA YAO YA TATU

Pia ukitazama kwa makini utakuta kuwa hakuna vigezo na vidhibiti vya uhakika katika kuitolea Ta'arif (definition) sahihi "Majaazi al-Mur'sal" (Absolute Metaphor), na matumizi yake, na hilo linasababisha mgongano katika matumizi yake kilugha jambo ambalo ni muhali kuwemo katika Qur'an.

Kwa mfano mtu akisema: "Nimeingiza kidole sikioni".
Kwa mujibu wa maelezo ya wenye kudai kuwepo majazi wanasema kuwa hapo kuna "Majaazul-Mursal" (Absolute Metaphor) na maana

yake ni kwamba umeingiza baadhi ya kidole, kwa sababu kidole chote hakiingii sikioni, kwa hiyo utakuwa umekitaja kidole lakini makusudio ni baadhi yake.
Wakiwa wanaifanyia kazi "Qaaidah" (kanuni) iliyopo katika"Majaazil Mursali" (Absolute Metaphor) isemayo:
"Min It'laaqil-Kulli wa Iraadatil-Ba'adhi" (ni kukitataja kitu kizima lakini makusudio ni baadhi yake)".

Lakini ukifanya utafiti wa kina utagundua kwamba wenye kuitumia "Qaaidah" (kanuni) hii wameshindwa kuidhibiti kitaalamu, kiasi ambacho inafikia kuifanya sehemu kubwa ya lugha ya kiarabu kama si yote kuwa ni Majazi! Jambo ambalo si sahihi.

Kwa sababu wanakubaliana wataalamu wote wa lugha ya kiarabu kwamba matumizi ya maneno katika maana zake za asili ni mengi zaidi kuliko maana za ki-Majazi.
Na hilo linapingana na kanuni hiyo na nyinginezo za kimajazi.

Kwa kuitumia "Qaaidah" hiyo ya kukitaja kitu kizima lakini makusudio ni baadhi yake, kunavunja itifaki hiyo.
Kwamfano, mtu akisema:
Nimekula wali, au
Nimekunywa maji, au
Nimekwenda Makka.
Kwa mujibu wa kanuni hiyo yanakuwa maneno yote hayo ni "Majazi" hata kama wenye kuyathibitisha hawasemi hivyo, lakini kanuni hiyo waliyoiweka ndiyo inavyoelekeza, kwa sababu utaambiwa wewe umekula baadhi ya wali na hukula wali wote.
Na utaambiwa kuwa umekunywa baadhi ya maji na hukunywa maji yote.
Na umefika baadhi ya sehemu za jiji la Makka na hukufika Makka yote, pengine umefika Mina, Aziiziyyah, Ajyaad, Ghaza na katika msikiti mtukufu, lakini hukufika Misfala, wala Hafaair, wala Ka'akiyyah

na sehemu nyinginezo katika mitaa ya Makka, kwa hiyo ukisema nimefika Makka ni majazi kwa kuwa umetaja Makka lakini makusudio yako ni baadhi yake.

Halikadhalika ukisema nimekaa msikitini, au nyumbani, au darasani, au ofisini, maneno yote hayo ni majazi kwa sababu kiuhakika kabisa utakuwa hukukaa katika msikiti wote bali umekaa katika baadhi ya eneo la msikiti, au nyumba, au darasa, au ofisi.

Hivyo basi, kwa sababu ya kukosekana udhibiti ulio makini wa suala hili ndiyo baadhi ya maulamaa wakasema kuwa maneno yote hayo ni hakika na wala si majazi na mtiririko wa maneno (context) ndiyo ulio ainisha maana ya maneno hayo.

Pia maulamaa wanaopinga kuwepo kwa majazi wanapowahoji na kuwapa changamoto (challenge) wenye kuthibitisha kuwepo kwa majazi hawapati majibu yoyote ya kuridhisha ndipo pale wakalipinga suala hili ili:

-Lugha ya kiarabu isichezewe.
-Ili watu wa batili wasipate nafasi ya kuichezea Qur'an kwa kupotosha maana yake kwa madai ya kwamba kuna majazi, na hili walilolifikiria ndilo lililotokea.
Kwa sababu wamejitokeza baadhi ya watu wakazipotosha aya nyingi zinazotaja sifa za Allah kwa madai kwamba kuna majazi kwa madai ya kumtakasa Allah na sifa za viumbe na hatima yake wakaingia katika upotofu.
Mpaka hapo itabainika kwamba;
Kupinga kuwepo kwa Majazi ndani ya Qur'an ili kufunga milango ya kuwaingiza watu kwenye upotofu ndiyo msimamo sahihi na wa haki na unaokubaliana na akili zaidi kuliko kudai kinyume chake.

Na ama baadhi ya mifano ambayo hutolewa kama ni hoja ya kuwakandamiza wenye kupinga majazi Imamu Ibnul-Qayyim katika kitabu chake "AL-SWAWAAI'QUL-MUR'SALA" ameyajibu kwa ufundi mkubwa mno.
Kadhalika Imamu wa Tafsiri na Usuul katika zama hizi sheikh Muhammad al-Amin al-Shanqitwiy pia amezijibu hoja nyingi tena kwa ufanisi wa hali ya juu kwa mwenye kutaka faida na arejee kwenye kitabu chake: "MAN'U JAWAAZIL-MAJAZI"

Na ukizitazama kwa makini hoja zao utagundua kwamba tofauti ni ya kimatamshi, hawa wameona utaratibu huo wauite "Majazi", na kwa hakika hilo lina mapungufu mengi kama tulivyo thibitisha hapo nyuma.
Na wengine wameona wauite "Usluubun min Asaalibil-Lugha" (utaratibu/mfumo katika taratibu za lugha) na njia hii ndiyo iliyokaribu na usahihi, ili kuwazuia watu wa batili wasiyapotoshe maandiko kwa kuupitia mlango huu.

SURA YA NNE

HOJA ZA WENYE KUITAKIDI KUONEKANA ALLAH HUKO AKHERA.

Hizi zifuatazo ni baadhi ya hoja za Ahli-Sunna wal-Jamaa katika kuthibitisha usahihi wa kuonekana Allah kwa macho huko akhera.
Mara baada ya kutaja hoja na dalili za Ahlu Sunna zenye kuthibitiha suala hili na kuzitolea maelezo Inshaallah tutafuatishia kutaja majaribio aliyoyafanya ndugu Juma M. Al-Mazrui dhidi ya hoja hizo kwa lengo la kuzipotosha na kisha yatafuata majibu yetu baada ya hapo ili kuthibitisha usahihi wa hoja hizo.

HOJA YA KWANZA.

Miongoni mwa hoja za wenye kuthibitisha kuonekana Allah huko akhera kwa macho ni pale aliposema Allah;

"وجوه يومئذ ناضرة***إلى ربها ناظرة".

"Zipo nyuso siku hiyo ni zenye kung'ara Ni zenye kumwangalia (kumuona) Mola wake".*

Surat al-Qiyamah aya 22-23.

Aya hii ni miongoni mwa hoja zilizowazi ambazo Ahlu-Sunna wanazitegemea katika kuthibitisha kwamba watu wema watamuona Mola wao huko akhera kwa macho yao. Na kuna hoja nyingi zinazoipa nguvu hoja hii yenye kuthibitisha kuonekana Allah –Azza wajallah- huko akhera kwa macho:
kuna hoja za ndani na hoja za nje.

Hoja za aina ya kwanza ni:-
Hoja za ndani, ni muweko wa neno hili katika upande wa kilugha, kwa sababu limetumika neno "Naadhirah" ambalo limenyambuliwa kutokana na asili ya neno "Nadharan", na likawa neno hili limekuja

baada ya herufi "ILAA", na kwa mujibu wa kanuni za lugha ya kiarabu linapokuwa neno hili limekuja baada ya herufi hiyo maana yake ya asili ni kutazama kwa macho.
Na kwa bahati nzuri hata wale wenye kupinga kuonekana Allah huko akhera wanakubaliana na sisi katika hilo, na ushahidi wa madai haya ni kauli ya ndugu
Juma M. Al-Mazrui aliposema katika ukurasa wa 53 wa kitabu chake, pale alipokuwa akielezea maana za neno "AL-NADHARU":

"Tukitazama maana ya neno hili: " (al-nadharu) kupitia kiyoo cha Qur'an tunakuta ni:

1) Kutazama kikawaida kwa macho: NA HII NDIO MAANA YA MSINGI YA NENO HILO....". mwisho wa kunukuu.

Kama ndugu Juma anakubaliana na sisi kuwa neno "AL-NADHARU" maana yake ya asili ni kutazama kwa macho, basi anatakiwa pia akubali kwamba
kwa mujibu wa kanuni za lugha ya kiarabu ambazo wataalamu wote wa lugha hiyo wamekubaliana ni kuwa: maana ya kwanza inayozingatiwa katika matumizi ya neno ni kulitumia neno katika maana yake ya asili kwanza, kabla hatujakwenda katika maana nyingine.

Pamoja na kwamba inawezekana likatumika neno katika maana nyingine isiyokuwa ya asili, lakini mpaka ishindikane kutumika maana ya asili, kisha kuweko na dalili itakayotufahamisha kushindakana matumizi hayo ya asili ya neno hilo na kwenda nje ya asili yake.

Na sisi tukilitazama neno "NAADHIRAH" hapa tunaona kuwa bado haijashindikana kulitumia katika maana yake ya asili ambayo ni kutazama kwa macho, na wala hakuna hoja yoyote ya msingi yenye kutufanya tutoke nje ya asili ya neno hili, bali ni kinyume chake; kuna hoja nyingi zinazolipa nguvu neno hilo libaki katika matumizi yake ya asili ambayo ni (kutazama kwa macho). Kama vile kutajwa neno: "وجوه" "Wujuuhun" (Nyuso) katika aya tunayoijadili.

Hoja za aina ya pili ni:
Hoja za nje, nazo ni zile dalili ambazo zimekuja kwa wingi mno katika Qur'ani na Sunna, na kauli za maulamaa wakubwa katika Maswahaba, na wanafunzi wao na maimamu waliokuja baada yao, kauli ambazo ni tafsiri za aya hii na nyinginezo zinazosema kwamba Allah ataonekana kwa macho akhera.
Ama kuhusu dalili za Sunna tutazitaja hapo mbeleni -Inshaallaah- hapa tutaitaja kauli moja ya "Taabi'yyun" (mwanafunzi wa swahaba) ambaye ni Ikrimah bin Abdillahi –rahimahu llaahu-.

Amesema Imamu Al-Tabariy katika kitabu chake JAAMIUL-BAYAAN (mashuhuri kwa jina la Tafsirul-Twabariy) katika juzuu ya 29 ukurasa wa 228:
Ametusimulia Muhammad bin Mansour Al-Tusiy, na Ibrahimu bin Sa'ad Al-Jauhariy (wote wawili) wamesema; ametusimulia Aliy bin Al-Hasan bin Shaqiq, amesema ametusilulia Al-Husain bin Waaqid kutoka kwa Yazid Al-Nahwiy kutoka kwa Ikrimah (amesema kuhusu kauli ya Allah):

"وجوه يومئذ ناضرة***إلى ربها ناظرة".

"Zipo nyuso siku hiyo zenye kung'ara Ni zenye kumwangalia (kumuona) Mola wake".*

Surat al-Qiyamah aya 22-23.

Akasema Ikrimah: "Zitamtazama Mola wake Mlezi".
Bila shaka, tafsiri hii ya Ikrimah inaipanguvu hoja ya wale wanaosema kwamba watu wema watamuona Mola wao huko akhera kwa macho yao, na si rahisi kuwa haya ni mawazo yake binafsi, bali ni tafsiri ambayo ameipokea kutoka kwa sheikh wake swahaba mtukufu Ibn Abbaas –radhiyallahu an'humaa- naye amemsikia bwana

Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- akitamka maneno hayo, na nina thubutu kusema hivi kwa sababu ya maandiko mengine ambayo yamepokewa kutoka kwa bwana Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- ambayo yanaipa nguvu kauli hii.

Pamoja na kuwa hoja hii iko wazi katika kuithibitisha itikadi hii sahihi ya Ahli Sunna juu ya kuonekana Allah huko akhera kwa macho, lakini wapinzani wa hoja hii hawakuwacha kuitilia mashaka tena kwa madai ambayo ni dhaifu mno. Na haya yafuatayo ni baadhi ya madai yao yanayoonekana yana uzito kidogo:

JARIBIO LA KWANZA LA KUIPOTOSHA HOJA HII

Katika kufanya jaribio la kuipotosha hoja hii inayozungumzia kuonekana kwa Allah huko akhera ndugu Juma M.Al-Mazrui ameleta madai mengi ambayo hayana msingi, na haya yafuatayo ni baadhi ya madai hayo:

1) Madai yake ya kwanza juu ya hoja hii ni kwamba, neno "Naadhirah" amabalo limetumika katika sura hii lina maana pana zaidi, kuliko kuona. Kwa sababu mtu anaweza kusema:
Nimeutazama mwezi lakini sikuuona.
Kwa hiyo neno kutazama halimaanishi kuwa lazima mtu aone.
Tazama ukarasa wa 50 katika kitabu chake.

Akiwa na maana kwamba, hata hao watakao mtazama Mola wao huko akhera kuna uwezekano wasimuone maana si lazima ukitazama ni sharti uone!!!

2) Madai yake ya pili ni kuhusu neno hili (nadharu) lina maana nyingi katika lugha ya kiarabu: haiwezekani kusema kwamba maana fulani ndio iliokusudiwa ila kwa dalili na ushahidi.

Na dalili ikiwa na maana nyingi basi ushahidi wake ni batili ila ikipata uzito kwa dalili nyingine nje ya hiyo au itapata uzito katika vifuatanishi vya maneno (context).
Tazama ukurasa wa 51,na 56 katika kitabu chake.

3) Hadithi zote ambazo zimepokewa zenye kuifasiri aya hii kuwa maana yake ni kumuona Mwenyezi Mungu ni hadithi batili na za uwongo !!!.
Tazama ukurasa wa 74-75 katika kitabu chake.

4) Akatoa dalili za kimaandishi zinazopingana na aya hiyo -kwa mtazamo wake- kama vile kauli yake Allah aliposema:
"Macho hayamfikii naye anayafikia macho (yote)".
Sura ya 6 aya ya 103.
Na hadithi isemayo :
"Na hakuna kinachozuia baina ya watu na kumtazama Mola wao isipokuwa lile vazi la kibri chake...".

MAJIBU YETU

Majibu yetu kuhusu madai yake ya kwanza, kwamba neno "naadhira" lina maana pana kuliko kuona kwa sababu mtu anaweza kutazama lakini asione, sisi tunasema hilo ni kweli, lakini neno "Naadhira" hapa limetumika kwa maana ya kuona kwa sababu hizi zifuatazo:

i) Hivi unadhania kwamba siku ya Qiyamah nyuso zitang'ara na kutoa nuru kwa kumtazama wasiemuona?
Unapomtazama unayempenda ambaye una shauku ya kumuona halafu usimuone je hiyo ni starehe au adhabu?
Je kutakuwa na tofauti gani baina ya wema na waovu katika hilo?

Makusudio makubwa ya kumuona Allah huko akhera ni Takrima watakayokirimiwa waja wema waliomuamini Mola huyo Mkarimu hapa duniani wakiwa hawamuoni –Ewe Allah ! Turuzuku ladha ya kuuona uso wako mtukufu- Aamin-.

ii) Pia kuna ushahidi wa aya nyinyingine za Qur'an kama aya ya 26 katika surat Yunus na hadithi nyingi za Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- ambazo zimefikia kiwango cha "MUTAWAATIR" (Idadi kubwa ambayo ni muhali kuwa wapokezi wake wameafikiana kutunga uwongo) hadithi zote hizo zinaiunga mkono aya hii.
Kwa mfano kauli yake bwana Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- aliposema:

إِنَّكُمْ سَتَرَوْنَ رَبَّكُمْ

"Kwa hakika nyinyi mtamuona Mola wenu".

Hadithi hii ameipokea Imamu Al-Bukhari namba 7435, na maelezo yake Inshaallah yatakuja huko mbeleni.

Ama kuhusu madai yake ya pili, ni pale aliposema:
"Neno hili (nadharu) lina maana nyingi katika lugha ya kiarabu: haiwezekani kusema kwamba maana fulani ndio iliokusudiwa ila kwa dalili na ushahidi".
Sisi tunasema kwamba bado kauli hii ya Juma si hoja ya kuibatilisha maana ya "kutazama" iliyobebwa na neno "naadhirah", kwa sababu maana hiyo ndiyo ya msingi na ya asili kama alivyokiri Juma.
Na katika kanuni za lugha ya kiarabu, mtu aliyeshikamana na maana ya asili ya neno hana wajibu wa kuleta hoja wala dalili ili kuthibitisha kwanini ameshikamana na maana ya asili, bali anayetakiwa kuleta hoja ni yule anayedai kinyume cha asili, na wale wanaoitumia aya hii kuthibitisha kuonekana Allah, wao wameshikamana na maana ya asili ya neno hili. Kwa hiyo wenye kuitakidi kinyume chake na wakalitafsiri neno NAADHIRAH kwa

maana ya KUNGOJEA badala ya maana ya asili KUTAZAMA wao ndio walio na wajibu wa kuleta hoja kwa nini wameikimbia maana hii ya asili na wakaamua kwenda nje ya asili bila ya hoja wala dalili yoyote yenye nguvu?

3- Madai yake ya tatu ni kwamba hadithi zote zilizokuja kuifasiri aya hii kuwa maana yake ni kumuona Mwenyezi Mungu ni hadithi batili na za uwongo! Kisha akaanza kuidhoofisha kauli ya Taabi'i Ikrimah kwa kusema:
"Hadithi hii pia ni dhaifu ! na udhaifu wake ni kuwa katika wapokezi wake yumo HUSAIN BIN WAQID naye ni dhaifu wanavyuoni wa hadithi hawamkubali.
Anasema Ibn Hajar Al-as'qalaani katika wanavyuoni wakubwa wa madhehebu ya Al-shafi:
"AL-HUSAIN BIN WAQID AL-MARUZI, ABU ABDALLAH AL-QADHI alikuwa mkweli lakini anasahau na anakosea sana....".
Mwisho wa kunukuu.
Tazama ukurasa wa 67 katika kitabu chake.

MAJIBU YETU

Hapa ndugu Juma ametumia uwongo na lengo lake ni kuwadanganya wasio na taaluma ya kutosha katika mambo ya elimu ya hadithi.
Hapa ameidhoofisha kauli ya Taabi'i Ikrimah kwa madai ya kuwa mpokezi wake ambaye ni AL-Husain bin Waaqid anakosea sana!

Jawabu yetu dhidi ya maneno ya ndugu Juma yatakuwa kama ifuatavyo:

Kwa hakika mimi ninashangazwa sana na tabia hii ya kusema uwongo anayoitumia ndugu Juma, kwa kweli mimi ninashangazwa sana na tabia yake hii ! nikafikia kujiuliza inakuwaje mtu anaamua

kuwadanganya watu katika mambo ya dini?! Kweli mtu huyo atakua ana nia njema? Au ana jambo jingine nyuma ya pazia?
Na uwongo wake huo uko pale alipodai kwamba Al-Husein bin Waaqid ni DHAIFU! Kisha akadai kuwa WANAVYUONI WA HADITHI NAO HAWAMKUBALI!!! Halafu maneno hayo akamsingizia Ibni Hajar kuwa ndiye aliyeyasema!
Je ni kweli Ibn Hajar amemdhoofisha mpokezi huyu? Hebu tuyatazame hayo maneno ya Ibn Hajar kuhusu mpokezi huyu, yeye anasema nini?

Anasema Ibni Hajar:

"الحسين بن واقد المروزي أبو عبد الله القاضي ثقة له أوهام".

"AL-HUSAIN BIN WAQID AL-MAR'WAZIY ABU ABDILLAHI AL-QADHIY NI THIQA (mwadilifu mwenye kuhifadhi) na ANA MAKOSA".
Tazama Al-Taq'ribu tar'jama namba1492.

Hayo ndiyo maneno ya Ibni Hajar Al-Asqalaniy kuhusu Al-Husain Ibn Waaqid, sasa hebu tuanze kuyachambua kwa kuhoji:
Je Ibn Hajar amesema kuwa Husein ni THIQA (muadilifu mwenye uwezo mzuri wa kuhifadhi) Au amesema kuwa Husein ni DHAIFU?
Jawabu liko wazi katika maneno yake hayo hapo nyuma, kwa hiyo Juma analazimika kutueleza ni mahali gani Ibni Hajar amesema kuwa Husein ni dhaifu?
Huwenda Juma akawa ametatizika na kauli ya Ibn Hajar pale aliposema: "ANA MAKOSA" yeye haraka haraka kwa sababu ya nia yake mbaya akadhania kwamba kuwa makusudio ya Ibn Hajar ni kuwa Husein "ANAKOSEA SANAA"!
Na kama hiyo ndiyo sababu iliyomfanya ndugu Juma aseme kuwa Husein ni dhaifu, je hakuiona kauli ya Ibni Hajar aliyosema kuwa Husein ni THIQA kabla ya kusema anakosea?

ii) Lau kama Husein angekuwa na makosa mengi ya kumfanya awe ni dhaifu na asikubaliwe na wanavyuoni wa hadithi, kitaalamu ingesemwa "Faahishul-ghalat" au "Kathirul-Khatai" au "Sayyiul-Hifdhi" lakini maneno yaliyotumika hapo ni "Lahu Auhaam" (ana makosa) na hiyo si sababu ya kumhukumu mpokezi kuwa ni dhaifu, kwani ni nani asiyekosea na kutatizika?

iii) Ndugu Juma yeye amesema ni "AL-MARUZI"! Na kutamka hivi si sahihi, sahihi ni AL-MAR'WAZIY , na hii pia ni ishara tosha kwamba yeye si mtaalamu, na hayuko makini katika fani hii, maana makosa yake katika jambo hili ni mengi mno kushinda hayo makosa anayomsingizia nayo Husein Al-Mar'waziy.

iv) Hebu tuwatazame maulamaa wa hadithi wanasema nini kuhusu Husein? Je ni kweli hawamkubali kama anavyodai ndugu Juma? Au huo ni uwongo wake alioubuni ili kuzihadaa akili za watu?

Amesema Imamu Abu Bakar Ahmad bin Muhammad Al-Ath'ram;
"Nilimuuliza Imamu Ahmad bin Hanbal: unasema nini kuhusu Al-HUSAIN BIN WAQID?
Akasema "hana ubaya wowote kisha akamsifia sana".

Amesema Imamu Yah'ya Ibn Mai'n: Husain ni "THIQA" (mwadilifu mwenye kuhifadhi vizuri).
Amesema Imamu Abu Zur'a: Husain "hana ubaya wowote".
Amesema Imamu Al-Nasai: Husain "hana ubaya wowote".
Amesema Imamu Abu Daud: Husain "hana ubaya wowote".
Amesema Imamu Ibn Sa'd : Husain: "alikuwa ni mwenye hadithi nzuri".
Amesema Imamu Ibn Hibbaan: "alikuwa Husain ni miongoni mwa watu bora na mara nyingine hukosea katika mapokezi".

Tazama maelezo hayo yote katika vitabu vifuatavyo:

Sualaatul-Ath'rami ukurasa wa 61.
Al-Jar'hu wal-Ta'adili juzuu ya 3 ukursa wa 306.
Tah'dhibul-Kamaal juzuu ya 6 ukurasa wa 493.
Taarikhul-Duuriy juzuu ya 2 ukurasa wa 119.
Taarikhu Abi Zur'a ukurasa wa 208.
Tabaqaatu Ibn Sa'd juzuu ya 7 ukurasa wa 371.
Tah'dhibul-Tah'dhibi juzuu ya 1 ukurasa 543.
Al-Taqribu, tarjama namba 1392.

Ndugu msomaji, kwa mujibu wa kauli hizi za maulamaa hawa wakubwa wa hadithi, je ni kweli kwamba hawamkubali Husein kama anavyodai ndugu Juma Al-Mazrui? Au Juma amekusudia kudanganya?

Haya ni machache katika mengi ya uwongo aliyoyajaza kwenye kitabu chake alichokiita;

"HOJA ZENYE NGUVU JUU KUTOONEKANA MWENYEZI MUNGU KWA MACHO" sawa sawa angekiita "HOJA ZA UWONGO JUU YA KUTOONEKANA MWENYEZI MUNGU.....". Bila shaka angekuwa amepatia zaidi.

Pamoja na kuwa ndugu Juma hapa ametumia maneno machache, lakini makosa yake ni mengi mno:

Kwanza amemzulia Ibn Hajar kwamba amesema kuwa Husein ni dhaifu, lakini tulipoyarejea maneno ya Ibn Hajar kuhusu Husein tukakuta maneno yake ni kinyume na alivyodai Juma.

Pili amewazulia uwongo maulamaa wa hadithi kwamba hawamkubali Husein, na hali ya kuwa madai hayo pia hayana ukweli.

4) Ama dalili za kimaandishi alizozitoa ndugu Juma kuonyesha kwamba zinapingana na aya hii, jawabu ni kwamba hazipingani bali ni ufahamu wake finyu, na hilo tutalielezea kwa kina -Inshaallah- tutakapokuwa tunazijibu hoja zao.

Katika upande wa ki-lugha ndugu Juma amefanya majaribio mawili kwa lengo la kutaka kuipotosha maana ya aya hii, amedai kwamba :

(a) hakuna "Muqaabala".
(b) kuna "al-Hasru".

Ni nini maana ya maneno haya? Fuatilia maelezo yafuatayo, Inshaallah utaubaini uwongo wake.

Dhamira kubwa ya ndugu Juma ililenga katika kuubatilisha ushahidi uliobebwa na aya hii wa kuthibitisha kuonekana Allah kwa macho huko akhera, lakini -wali llaahil-hamdu- hakufaulu na matokeo yake amewadhihirishia watu wenye elimu uwelewa wake mdogo katika suala hili na ufahamu finyu.

Hebu tuanze na huo "Muqaabala"
Amesema Juma:
"Kanuni ya kwanza ni ile inayojulikana kuwa "المقابلة البلاغية" (muelekeo wa neno au maneno na kinyume chake)."

"Muqaabala ni; kuleta maana mbili au tatu zenye kuafikiana kisha ukaleta kinyume chake kwa mpangilio."
Kasha akatoa mifano takriban mitano, kisha akasema: "katika aya hizi zote sehemu ya mwanzo ya aya ni tofauti na sehemu yake ya pili, nayo ni kinyume chake, na kila neno linaelekeana au linakabiliana na mwenzake kimaana. Huu ndio mukabala wa balagha ya kiarabu: yanapotajwa maneno fulani kisha yakaletwa mengine yanayo kabiliana na hayo yaliyotajwa mwanzo kimaana basi ni lazima yawe maneno ya kwanza ni kinyume cha maneno ya pili."
Tazama katika ukurasa wa 77 katika kitabu chake "Hoja zenye Nguvu"

Kisha akasema tena:

"Sasa kama tutafasiri kuwa nyuso za watu wema zinamuona Mwenyezi Mungu basi maana itakuwa hivi: "kuna nyuso zinamuona Mwenyezi Mungu na kuna nyuso zinatazamia kuteremkiwa na adhabu." Tazama jinsi tafsiri ilivyokuwa haioani, na huo mukabala wa balagha ya kiarabu unavyopotea. Nyuso za watu wema zinamuona Mwenyezi Mungu wakati za watu wabaya zinatazamia kuteremkiwa na adhabu !!!".

Tazama kitabu chake Hoja zenye Nguvu ukurasa wa 81.

MAJIBU YETU

Majibu yetu yatakua katika masuala mawili:

Suala la kwanza ni kuhusu (المقابلة") Muqaabala, sisi tunasema kwamba: kuitafsiri aya hii kwa maana ya kumuona Allah hakuupotezi muqaabala, bali muqaabala upo isipokuwa Juma hakuutaka kwa sababu ni kinyume na itikadi yake, na yeye huwa anatanguliza kwanza itikadi yake kisha mambo mengine yatapimwa na anavyoitakidi, jambo likiafikiana na itikadi yake, hilo litakuwa ni zuri na linafaa hata kama ni baya lisilofaa, na kama haliafikiani na itikadi yake basi hilo ni baya na halifai hata kama ni mafundisho ya Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam-, na mpokezi anayekubalika ni yule anayepokea riwaya ya kuipa nguvu itikadi yake hata kama ni dhaifu, na yule anayepokea kinyume na itikadi yake huyo ni dhaifu, mwongo, na anaghushi! Na umeshayaona pale alipomzulia Ibn Hajar ili amdhoofishe mpokezi mkweli anaekubalika (Husein Al-Waqidiy) na Inshaallah hayo utayaona kwa wingi huko mbeleni.

Sisi hapa tunasema kwamba:

Nyuso za watu wema siku ya Qiyama zitang'ara.

Kwa sababu watu wema watakua katika neema kubwa ya kumuona Mola wao.

Na nyuso za watu waovu zitajikunja.
Kwa sababu watu waovu watakua katika adhabu kali na huku wana yakini kwamba watafikwa na adhabu kubwa kuliko hiyo.

Kwa hiyo watu wema nyuso zao zitatoa nuru.
Na watu waovu nyuso zao zitakunjana.

Watu wema watakua katika neema kubwa.
Na watu waovu watakua katika adhabu kali.

Na huu ndiyo Muqaabala wenyewe, ambao Juma hakuutaka kwa sababu unapingana na itikadi yake ya kiibadhi.
Imamu Al-Aluusiy katika tafsiri yake "Ruhul-Ma'aniy" juzuu ya 29 ukurasa wa 75 anaitilia nguvu hoja hii kwa kusema:

"وتحقيق ذلك أن ما يفعل بهم فى مقابلة النظر إلى الرب سبحانه لكون ذلك غاية النعمة وهذا غاية النقمة...".

"Na uthibitisho wa hilo ni kuwa yale wanayofanyiwa hao (waovu) ni muqaabala wa kumtazama Mola –Sub'haanah- kwa kuwa hilo ni ukomo wa neema, na hili (wanalo fanyiwa waovu) ni ukomo wa mateso".
Suala la pili ni mas'ala ya (الحصر) kutangulizwa mtendwa, amesema Juma:

"Watu wa fani ya balagha wanaita hii kuwa ni:

"تقديم المعمول على العامل"

"Kumtanguliza mtendwa badala ya mtenda."

Yaani kawaida ni kuwa atangulie mtenda sio mtendwa: mtendwa aje baadaye. Huu ndio utaratibu wa asili wa lugha ya kiarabu kama tulivyosema mwanzo.
Sasa je kama kutangulia mtenda ndio utaratibu wa asili wa lugha hii, inapokuja kinyume na hivi akatangulia mtendwa huwa inamaanisha nini?

Wanasema kitaalam kuwa hii inaonesha "الحصر" yaani kumuusisha mtenda na kitu kimoja tu na huwa hafanyi cha pili."
Mwisho wa kunukuu.
Tazama kitabu chake "Hoja zenye Nguvu" ukurasa wa 83.

Kisha akasema tena:
"Sasa ikiwa tutaifasiri kutazama hapa kwa maana ya kuona basi tafsiri haitokuwa sahihi: itapingana na uhakika ulivyo.
Kwanini? Kwa sababu tafsiri itabidi iwe hivi: "(nyuso hizo) zinamuona Mola wake tu." Na huu si ukweli: ukweli ni kuwa watu huko kwenye kisimamo cha kiama na kwenye pepo wataonana na wataona kheri zilizoandaliwa katika pepo.
Yote haya yanaonesha kuwa makusudio ya aya hii si kuona."
Mwisho wa kunukuu.
Tazama katika kitabu hicho ukurasa wa 85.

MAJIBU YETU

Majibu ya maneno haya yatakuwa katika njia zifuatazo:
Njia ya kwanza:
Ninataka kumfahamisha ndugu Juma na wengineo kwamba: mas'ala haya huwa mahali pake ni katika elimu ya balagha sehemu ya "Il'mul-Ma'ani" mlango wa "Al-Qasru".
Kuna njia nyingi za "Al-Qasru" moja katika hizo ni hii ya kumtanguliza mtendwa kabla ya mtenda, hili ni jambo ambalo linafahamika na wala halina upinzani.
Lakini jambo muhimu la kulijadili hapa, je matumizi ya lugha kwa utaratibu huu hayaleti ila maana moja tu nayo ni: "الحصر" kumhusisha mtenda na kitu kimoja tu akawa hafanyi cha pili kama anavyodai Juma?
Au anapotangulizwa mtendwa juu ya mtenda kuna malengo mengine kinyume na aliyoyataja Juma?

Sisi tunasema: naam, inawezekana akatangulizwa mtendwa kabla ya mtenda kwa malengo mengine kinyume na aliyoyataja Juma.
Inawezekana kuwa Juma ameghafilika, au hilo hajui, au anajua lakini amekusudia kupotosha.
Kwa mfano; kuna uwezekano wa kutangulizwa mtendwa kwa lengo la:

1-Kumpa umuhimu mtendwa (الإهتمام)

2- Kuchunga utaratibu wa utungo wa maneno (رعاية التناسب فى نظام الكلام).

Na malengo mengineyo ambayo wanavyuoni wa fani ya balagha wameyaeleza kwa marefu na mapana kwenye vitabu vyao.
Na yote tuliyoyataja yana mifano tele kwenye Qur'an na maneno ya waarabu.
Labda hapa tutoe mifano miwili mitatu:
Mfano wa kwanza; amesema Allah:

{وَأَمَّا ثَمُودُ فَهَدَيْنَاهُمْ فَاسْتَحَبُّوا الْعَمَى عَلَى الْهُدَى }فصلت17}

"Na ama Thamudi tuliwaongoza, wakapenda upofu kuliko uwongofu".
Surat Fussilat (41) aya ya 17.

Neno "Thamudi" hapa ni mtendwa kwa mujibu wa Qiraa (kisomo) cha baadhi ya wasomaji walipolisoma kwa Fat'ha ya Dali. Hapo neno "Thamudi" limetangulia na haki yake ilikua ni kuja baada ya mtenda, na huyo mtenda ni dhamiri (pronoun) aliyoambatana na Fi'ilu (kitendo) هديناهم "tuliwaongoza".

Kwa hiyo si makusudio ya aya hii kuuhusisha uwongofu wa Allah kwa kabila la Thamudi tu, kwa sababu ya kuwa mtendwa ametangulia, kwa sababu wapo watu wengine waliongozwa na Allah na wao si katika kabila la Thamudi, bali makusudio ni kuonyesha kwamba mtendwa hapo amepewa umuhimu na kupatilizwa.

Mfano wa pili; amesema Allah:

"وَالأَنْعَامَ خَلَقَهَا"
النحل5

"Na wanyama hoa amekuumbieni"
Suratun Nah'l (16) aya ya 5.

Pia si makusudio ya aya hii kwamba Allah ametuumbia wanyama hoa pekee, bali hata wanyama pori pia amewaumba yeye.
Mfano wa tatu; amesema Allah:

"فَأَمَّا الْيَتِيمَ فَلَا تَقْهَرْ"
الضحى9

"Basi Yatima usimwonee".
Suratul-Dhuhaa (93) aya ya 9.

Uonevu ni haramu kwa kila mtu, na si kwa yatima peke yake, na yaliyo haramu kumfanyia yatima ni mengi na si uonevu pekee, kwa hivyo huwezi kusema kwamba: haifai kumwonea yatima tu, kwa sababu mtendwa ametangulizwa, la hasha! Bali hata wengine wasiokua yatima pia ni haramu kuwaonea, pia huwezi kusema kwamba lililo haramu ni uonevu tu kwa yatima, lakini uovu mwingine wowote usio kuwa uonevu unaweza kumfanyia.
Kwa hiyo kitendo alichokifanya Juma si sahihi, kwa sababu yeye katika maneno yake ameleta dhana ya kwamba utaratibu huu wa "kumtanguliza mtendwa kabla ya mtenda" hauleti isipokuwa maana moja tu, nayo ni; kumhusisha mtenda na kitu kimoja tu, na dhana hiyo si ya kweli kwa maelezo tuliyo yatoa, na kwa maelezo hayo ndiyo unadhihirika ufahamu finyu alio nao Juma katika mas'ala haya ya kielimu.

Pili, hadithi zilizo kuja kuizungumzia itikadi hii zinaukata mzozo huu kwa kuifafanua aya hii na nyinginezo, na kutuwekea wazi juu ya kuthibiti kwa jambo hili la kuonekana Allah kwa macho huko akhera. Kwa hiyo hoja yetu hii bado imesimama na Juma na kaumu yake hawakufaulu katika majaribio yao ya kutaka kuiporomosha.

Hebu sasa na tuiangalie hoja ya pili:

Miongoni mwa hoja zilizo na nguvu zinazothibitisha kuonekana kwa Allah huko akhera kwa macho ni kauli yake Allah –Azza wajalla- aliposema:

{لِّلَّذِينَ أَحْسَنُواْ الْحُسْنَى وَزِيَادَةٌ }
يونس26
'Wale waliofanya mema watapata wema na ziada''.
Surat Yunus (10) aya ya 26.

Katika aya hii limetajwa neno ziada, na wala haikuanishwa hiyo ziada yenyewe ni nini? wala hakikutajwa kiwango chake, na hilo ni katika mambo ya ghaibu hatuna njia ya kulifahamu ila kwa kupitia wah'yi utokao kwa Allah, na tulipomrejea bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- tuanona anatwambia kuwa maana ya neno ziada lililotajwa katika aya hii ni: "kumuona Allah huko akhera".
Na tafsiri hiyo imeelezwa kwa mapokezi haya yafuatayo:

قال الإمام مسلم رحمه الله تعالى:
حَدَّثَنَا عُبَيْدُ اللَّهِ بْنُ مَيْسَرَةَ قَالَ حَدَّثَنِي عَبْدُ الرَّحْمَنِ بْنُ مَهْدِيٍّ حَدَّثَنَا حَمَّادُ بْنُ سَلَمَةَ عَنْ ثَابِتٍ الْبُنَانِيِّ عَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ أَبِي لَيْلَى عَنْ صُهَيْبٍ عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ:
إِذَا دَخَلَ أَهْلُ الْجَنَّةِ الْجَنَّةَ قَالَ يَقُولُ اللَّهُ تَبَارَكَ وَتَعَالَى تُرِيدُونَ شَيْئًا أَزِيدُكُمْ فَيَقُولُونَ أَلَمْ تُبَيِّضْ وُجُوهَنَا أَلَمْ تُدْخِلْنَا الْجَنَّةَ وَتُنَجِّنَا مِنْ النَّارِ قَالَ فَيَكْشِفُ الْحِجَابَ فَمَا أُعْطُوا شَيْئًا أَحَبَّ إِلَيْهِمْ مِنْ النَّظَرِ إِلَى رَبِّهِمْ عَزَّ وَجَلَّ
حَدَّثَنَا أَبُو بَكْرِ بْنُ أَبِي شَيْبَةَ حَدَّثَنَا يَزِيدُ بْنُ هَارُونَ عَنْ حَمَّادِ بْنِ سَلَمَةَ بِهَذَا الْإِسْنَادِ وَزَادَ ثُمَّ تَلَا هَذِهِ الْآيَةَ { لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَى وَزِيَادَةٌ }

Amesema Imamu Muslimu: Ametusimulia Ubaidu-llahi Ibn Maysarah, Amesema: ametusimulia Abdul-rahman bin Mah'di, amesema: ametusimulia HAMAD BIN SALAMAH, kutoka kwa Thabiti bin Aslam al-Bunani, kutoka kwa Abdul-Rah'man Ibn Abi Laylaa, kutoka kwa Suheib, kutoka kwa Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- amesema:
"Watakapoingia watu wa peponi katika pepo atanadi mwenye kunadi: hakika nyinyi mna ahadi mbele ya Allah anataka kukutekelezeeni.

Watasema kwani hukuzing'arisha nyuso zetu na ukatuokoa na moto na ukatuingiza peponi?

Akasema (Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam-);

Kisha ataondoa pazia, kwa hakika hawajawahi kupewa kitu wanacho kipenda zaidi kuliko kumtazama yeye (Allah subhaanahu wata'alaa).

Amesema Imamu Muslimu: ametusimulia Abu Bakri Ibn Abi Shaiba, ametusimulia Yazid Ibn Haroun, kutoka kwa HAMAD IBN SALAMAH kwa sanad hii hii na akazidisha (kwamba Mtume swalla llaahu alayhi wasallam) kisha akasoma:

"Wale waliofanya mema watapata wema na ziada".

Tazama sahihul muslim hadithi namba 449.

قال الإمام الترمذي:

حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ بَشَّارٍ حَدَّثَنَا عَبْدُ الرَّحْمَنِ بْنُ مَهْدِيٍّ حَدَّثَنَا حَمَّادُ بْنُ سَلَمَةَ عَنْ ثَابِتٍ الْبُنَانِيِّ عَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ أَبِي لَيْلَى عَنْ صُهَيْبٍ عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي قَوْلِهِ:

{ لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَى وَزِيَادَةٌ }

قَالَ إِذَا دَخَلَ أَهْلُ الْجَنَّةِ الْجَنَّةَ نَادَى مُنَادٍ إِنَّ لَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ مَوْعِدًا قَالُوا أَلَمْ يُبَيِّضْ وُجُوهَنَا وَيُنَجِّنَا مِنْ النَّارِ وَيُدْخِلْنَا الْجَنَّةَ قَالُوا بَلَى قَالَ فَيَنْكَشِفُ الْحِجَابُ قَالَ فَوَاللَّهِ مَا أَعْطَاهُمْ شَيْئًا أَحَبَّ إِلَيْهِمْ مِنْ النَّظَرِ إِلَيْهِ.

Amesema Imamu Tirmidhiy: "Ametusimulia Muhammad bin Bashaar" Amesema: ametusimulia Abdul-rahman bin Mah'di, amesema: ametusimulia Hammaad bin Salamah, kutoka kwa Thabiti bin Aslam al-Bunani, kutoka kwa Abdul-Rah'man Ibn Abi Laylaa, kutoka kwa Suheib, kutoka kwa Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- kuhusiana na kauli ya Allah:

"Wale waliofanya mema watapata wema na ziada".

Akasema (Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam-):

Watakapoingia watu wa peponi katika pepo atanadi mwenye kunadi: hakika nyinyi mna ahadi mbele ya Allah anataka kukutekelezeeni.

Watasema kwani hakuzing'arisha nyuso zetu na akatuokoa na moto na akatuingiza peponi?

Akasema (Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam-);

Kisha litafunuka pazia. Akasema: Naapa kwa Allah ! Hajawahi kuwapa kitu wanacho kipenda zaidi kuliko kumtazama yeye (Allah subhaanahu wata'alaa).

Tazama Jaamiul-Tirmidhiy hadithi namba 2552.

قال الإمام ابن أبي عاصم:

ثنا هدبة بن خالد ، ثنا حماد بن سلمة ، ثنا ثابت ، عن عبد الرحمن بن أبي ليلى ، عن صهيب ، أن رسول الله صلى الله عليه وسلم قال في هذه الآية (للذين أحسنوا الحسنى وزيادة قال :
« إذا دخل أهل الجنة الجنة ، وأهل النار النار ، نادوا : يا أهل الجنة إن لكم عند الله تعالى موعدا يريد أن ينجزكموه . قالوا : ما هو ؟ ألم يبيض وجوهنا ، ويدخلنا الجنة ، ويجرنا من النار ؟ فيكشف الله عنهم الحجاب ، فينظرون إلى الله تعالى ، فما شيء أعطوه أحب إليهم من النظر إليه ، وهي الزيادة »

Amesema Imamu Ibn Abi A'sim: ametusimulia Hud'ba Ibn Khalid Ametusimulia Hammaad bin Salamah, kutoka kwa Thabiti bin Aslam al-Bunani, kutoka kwa Abdul-Rahman Ibn Abi Laylaa, kutoka kwa Suheib, kwamba Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- amesema kuhusiana na kauli ya Allah:

"Wale waliofanya mema watapata wema na ziada".

Akasema Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam-;

Watakapoingia watu wa peponi katika pepo, na wakaingia watu wa motoni katika moto, atanadi (mwenye kunadi): Enyi watu wa peponi! Hakika nyinyi mna ahadi mbele ya Allah anataka kukutekelezeeni.

Watasema ni ahadi gani hiyo? kwani hakuzing'arisha nyuso zetu na akatuingiza peponi, na katuokoa na moto?

Akasema (Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam-):

Kisha Allah atawaondolea pazia, watamtazama Allah ! Hakuna kitu walichopewa wanacho kipenda zaidi kuliko kumtazama yeye (Allah subhaanahu wata'alaa), na HIYO NDIO ZIADA.

Tazama kitabu al-Sunna cha Ibn Abi A'sim, ukurasa wa 217 hadithi namba 472.

Hadithi hii ni sahihi kwa mujibu wa utafiti wa misingi ya mapokezi ya hadithi za Mtume Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam- na

wala haina kasoro yoyote. Pia maulamaa wa hadithi wameisahihisha na wala hakuna aliyeitia kasoro.
Ama kuhusu kasoro alizozitaja Juma al-Mazrui katika kitabu chake "Hoja zenye nguvu" kutoka kwa sheikh wake wa kiibadhi al-Qannubi, Inshaallah hapo mbele tutakuwekea wazi ili uzione hiyana na hila zinazofanywa na watu hawa, ima kwa sababu ya ujahili katika elimu ya hadithi au kwa sababu ya nia zao mbaya.
Ndugu msomaji, bila shaka ukiitazama hadithi hii kwa mazingatio utaona namna bwana Mtume Muhammad –swalla llaahu alayhi wasallam- alivyoifafanua kwa uwazi usio na kificho na kuibainisha maana sahihi ya aya 26 ya surat Yunus (10).

Basi ni nani aliyekosa haya akadai kuwa yeye anajua zaidi maana na makusudio ya kitabu cha Allah -tabaaraka wata'alaa- (Qur'an) kumshinda bwana Mtume Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam? Bila shaka hakuna muislamu yoyote atakayeweza kudai hilo, kwa sababu Allah yeye ndiye aliyemteua Mtume Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam- kuwa wadhifa wake ni kuwabainishia watu yaliyomo ndani ya kitabu kitukufu (Qur'an) pale aliposema Allah:

"وأنزلنا إليك الذكر لتبين للناس ما نزل إليهم " الآية من سورة النحل 44.

"Na tumekuteremshia wewe dhikri (Qur'an) ili upate kuwabainishia watu kile kilichoteremshwa kwao".

Surat al Nahli aya ya 44.

Na halikadhalika tunakubaliana waislamu wote kuwa hatuna hiyari katika kuufuata ubainifu wa mjumbe huyu mtukufu, bali ni wajibu wetu kuamini, kukubaliana, na kufuata yale yote aliyotufundisha kutoka kwa Allah –sub'haanahu wata'alaa- kwa sababu mjumbe huyo hatamki kwa matamanio ya nafsi yake bali kila analolitamka ni kwa amri ya mola wake jalla jalaaluh.

Hivyo basi, kwa bayana hii ya bwana Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- inatubainikia kwamba;

Allah atawakirimu waja wake waumini huko akhera kwa neema nyingi, na neema iliyo kubwa kuliko zote ni ile ya kumuona yeye Tabaaraka wata'alaa kwa macho yao bila ya kuwepo kizuizi chochote, na hiyo ndiyo maana ya ziada iliyotajwa katika aya ya 26 ya sura ya 10 (surat Yunus).

JARIBIO LA KWANZA LA KUIPOTOSHA HOJA YA PILI

Baada ya ndugu Juma kuona kuwa mapokezi hayo yamethibiti kwa njia zilizo sahihi kutoka kwa Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- katika kuitafsiri aya ya 26 ya surat Yunus, na ikawa tafsiri yake inalingana na itikadi ya Ahli sunna yakuwa Allah ataonekana huko akhera kwa macho, na ikawa pia tafsiri hiyo inapingana na itikadi potofu ya kiibadhi yakwamba Allah hataonekana akhera kwa macho, ndipo hapo hiyana za kielimu zilipoanza kutoka kwa ndugu Juma M. Al-Mazrui huku akipata msaada kutoka kwa sheikh wake aliyemvika kilemba cha ukoka, naye si mwingine bali ni Said Mabruuk al-Qannubi, wakaanza kuyapotosha maandiko sahihi ili kuihami itikadi yao hiyo potofu kwa kutumia uwongo, hila na hadaa, subhaana llaah!

Sasa hebu nikunakilie maneno yake kuhusu hadithi hii kutoka katika kitabu chake "Hoja zenye Nguvu". Amesema katika ukurasa wa 111:

''..na hapa nitakunakilia namna mbili tu katika maneno ya AL IMAMU SAID BIN MABRUK AL- QANNUBI IMAMU WA HADITHI ,FIQHI NA USULI uone jawabu yake juu ya hadithi hii...anasema Al imamu Al qannubi:

''Na hadithi hii ni batili na ubainifu wa haya ni kwa njia mbili:

Ni kuwa katika sanad yake yumo HAMAD BIN SALAMA, naye japo kuwa ni mkweli katika nafsi yake lakini

HIFDHI YAKE NI MBOVU:

ANASAHAU na

KUKOSEA na

AMECHANGANYIKIWA na KUBADILIKA MWISHONI MWA UMRI WAKE; kwahivyo yeye hafai kuwa hoja''.
Mwisho wa kunukuu.

MAJIBU YETU

Majibu yetu dhidi ya maneno haya ya Juma Al-Mazrui aliyoyanakili kutoka kwa sheikh wake Al-qannubi, sisi Inshaallah tutayajibu kwenye nukta mbili:

Nukta ya kwanza:
Ni kuhusu kauli yake ya kumuita Al-Qannubi kuwa ni Imamu wa hadithi.
Bila shaka kwa watu walio na maarifa juu elimu hii ya hadithi wanaifahamu daraja hii ya uimamu katika fani hii kwamba si kila mtu alipewa daraja hiyo bali walipewa watu wachache mno kama vile:

Sufyaan al-Thawry, Sufyaan bin Uyaina, Malik bin Anas, Ali bin al Madini, Ahmad bin Hanbali, Muhammad bin Ismail al Bukhari na wengineo wachache.

Kwa uthibitisho zaidi hebu fungua vitabu vya tarjama kisha usome kwa utulivu utaligundua hili ninalokueleza, hebu soma vitabu kama vile;
Tah'dhibul kamal,ya al mizziy.
Tah'dhibut Tah'dhibi na al-Taq'ribu vya al Haafidh Ibn Hajar al-As'qalaani.
Mizanul-I'tidaal ya Imamu al-Dhah'bi n.k.

Pamoja na kuwa mlango wa kuitana hivyo haujafungwa, lakini je ni kila mtu anaweza kupewa wasifu huo hata wale wasiostahiki?

Lakini unajua ni kwanini ndugu Juma ameamua kumpa al-Qannubi daraja hiyo katika fani hii hususani alipokuwa akilizungumzia suala hili?

Si kwa nia nyingine bali lengo lake ni kumkuza mbele ya macho ya wasomaji ili aipe uhalali kazi aliyoikusudia kuifanya, nayo ni kazi ya kuyapotosha maandiko sahihi yaliyopokelewa kutoka kwa Mtume mtukufu Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam- yanayotufundisha kwamba Allah -subhaanahu wata'ala- ataonekana kwa macho huko akhera na kuyafanya maandiko hayo kuwa ni batili kwa sababu yanapingana na itikadi ya madhehebu yake ! ndiyo akaamua kumnyanyua na kumpa cheo cha uimamu katika hadithi ili msomaji aone kwamba kuna mwanachuoni mkubwa, tena Imamu wa hadithi na fiq'hi……ameibatilisha hadithi hii !!! Na hakumpa cheo hicho kwa kuwa anastahiki, hapana! Kwa sababu hapo mbeleni Inshaallah utakubainikia ujahili wa mtu huyo aitwaye imamu wa hadithi katika elimu hii.

Nukta ya pili:
Ni madai yake kwamba Hamad bin Salama hifdhi yake ni mbovu, anasahau, anakosea na amechanganyikiwa na kubadilika mwishoni mwa umri wake.
Madai haya ya kwamba hifdhi ya Hamad bin Salama ni mbovu si madai ya kweli na mwenye kudai hilo anatakiwa alete ushahidi juu ya hilo, na hakuna ushahidi wowote juu ya madai hayo, bali kinyume chake ndio sahihi. Na Inshaallah tutayajibu maneno hayo kwa njia tatu:

Njia ya kwanza:-
Kauli za maulamaa wakubwa wa hadithi kuhusu hifdhi ya Hamad bin Salama:

1-Amesema Imamu Ahmad bin Hambali:

وقال أحمد: أثبتهم فى ثابت حماد بن سلمة.
"Mtu madhubuti kuliko wote (waliopokea kutoka kwa) Thabit ni Hamad bin Salama".
Na hadithi hii Hamad bin Salama ameipokea kutoka kwa Thabiti, lizingatie hilo kwa sababu ni jambo muhimu.
Na amesema tena Imamu Ah'amd kuhusu Hamad bin Salama kuwa ni:
"(Mtu) Madhubuti".

2-Amesema Imamu Yahya bin Mai'n:
وقال ابن معين: من خالف حماد بن سلمة فى ثابت فالقول قول حماد.
"Yeyote atakayetofautiana na Hamad bin Salama kuhusu (mapokezi kutoka) kwa Thabit kauli (ya kuchukuliwa) ni kauli ya Hamad".
Pia amesema tena:
(Hamad bin Salama) ni ''Thiqa'' (muadilifu mwenye hifdhi nzuri).

3-Amesema Al Imamu al Saajiy:
وقال الساجي: كان حافظا ثقة مأمونا
''Alikuwa (Hamad bin Salama) ni mwenye kuhifadhi tena ni ''Thiqa'' (muadilifu) na ni mwenye kuaminiwa''.

4-Amesema Ibn Sa'ad:
وقال ابن سعد: كان ثقة كثير الحديث وربما حدث بالحديث المنكر
"Na alikuwa (Hamad) ni mtu Thiqa (muadilifu mwenye hifdhi nzuri) mwenye hadithi nyingi, lakini mara nyingine anasimulia hadithi Munkar".
Hapo limetumika neno la kiarabu ''Rubba'' nalo huleta maana ya uchache.

5-Amesema Al I'jliy:
وقال العجلي: ثقة رجل صالح حسن الحديث
(Hamad) ni: ''Thiqa (muadilifu mwenye hifdhi nzuri) mtu mwema mwenye hadithi nzuri''.
6-Amesema Al Haafidh Ibn Hajar katika kitabu chake al Taq'ribu uk 195:

قال الحافظ ابن حجر فى التقريب ص 195 رقم الترجمة 1636:
حماد بن سلمة بن دينار البصري أبو سلمة ثقة عابد أثبت الناس فى ثابت وتغير حفظه بآخره..".

"Hamad bin Salama bin Dinar al Basriy Abu Salama ni Thiqa (muadilifu mwenye hifdhi nzuri) mcha mungu na ni mtu madhubuti zaidi (kati ya waliopokea kutoka) kwa Thabit, na hifdhi yake ilibadilika mwishoni mwa umri wake".

7-Amesema Imamu Aliy bin Abdillahi bin al-Madiniy sheikh wake Imamu al-Bukhariy:

وقال ابن المديني: من سمعتموه يتكلم فى حماد فاتهموه

"Utakapomsikia mtu anamsema kwa ubaya Hamad bin Salama basi mtuhumuni (mtu huyo)".
Juma Mazrui na sheikh wake Qannubi wanamsema vibaya Hammad, bila shaka wanafanya hivyo kwa sababu ya nia zao mbaya, na sisi tuna watuhumu kwa hilo.
Tazama maneno hayo ya maulamaa kwenye vitabu vifuatavyo:
Al-thiqaat cha Ibn Hibbaan juzuu ya 6 ukurasa wa 216.
Twabaqaatul-Kubraa cha Ibn Sa'd juzuu ya 7 ukurasa 282.
Taarikhu Thiqaat cha al-Ij'liy ukurasa wa 131.
Mizaanul-I'tidaal cha al-Dhah'biy juzuu ya 1 ukurasa 590-595.
Tah'dhibut-Tah'dhibi cha Ibn Hajar al-As'qalaaniy juzuu ya 2 ukurasa wa 10-13.
Al-Taq'ribu pia cha al-Hafidh Ibn Hajar al-As'qalaaniy, tarjama namba 1636.

Sasa hebu ndugu msomaji mtukufu linganisha kauli hizo za maulamaa hao wakubwa wa hadithi juu ya Hamad bin Salama na kauli za huyo al-Qannubi aliyevishwa kilemba cha ukoka na ndugu Juma! Bila shaka ukweli utakubainikia na hapo ndiyo utagundua kwamba kuna agenda ya siri baina ya huyo sheikh aliyesimikwa daraja ya uimamu (al-Qannubi) na mwanafunzi wake (Juma).

Njia ya pili:-

Ni kuhusu suala la kuwa Hamad bin Salama anakosea na anasahau, jawabu ni kwamba kukosea na kusahau ni katika tabia za kibinaadamu, hakuna mwanadamu yeyote asiyekosea au kusahau ila yule aliyekingwa na Allah -Tabaaraka wata'alaa- asikosee wala kusahau.
Isipokuwa nataka ifahamike kwamba kukosea au kusahau kukizidi mno kupita kiasi hiyo itakuwa ni kasoro, lakini tumeona katika kauli ya Imamu Ibn Sa'ad kuwa Hamad ana hadithi nyingi mno lakini ni mara chache kukosea. Haya ni nani huyo asiyekosea? Hebu na atutajie! Na ni nani huyo asiyesahau? Alisahau Adam baba wa watu wote seuze Hamad bin Salama?

Amesema Allah:

وَلَقَدْ عَهِدْنَا إِلَى آدَمَ مِن قَبْلُ فَنَسِيَ وَلَمْ نَجِدْ لَهُ عَزْماً

طه115

"Na tulimpa ahadi (Nabii) Adam zamani,lakini alisahau wala hatukuona kwake azma".

Surat Twaha (20) aya ya 115.

Bali amesahau Musa bin Imran Mtume wa Allah, soma aya ya 73 katika surat al Kahfi (18). Kwa hiyo kusahau si kasoro katika upokezi wa habari, lakini ikithibiti kwamba mpokezi amesahau katika habari aliyoipokea, au kusahau kwake kumevuka mipaka bila shaka hiyo itakuwa ni dosari na itaathiri katika habari zake atakazo zipokea, hapa Juma na sheikh wake Qannubi hawajatuthibitishia kwa maandiko yoyote ya kielimu kuhusu kukosea kwa Hammad, je kumevuka mipaka au wameamua kumtuhumu tu? Na kama ndugu yangu msomaji umeyazingatia maneno ya maulamaa tuliyokutajia kuhusu Hammad utagundua kuwa ni kinyume na wanavyosema wazushi hawa.
Njia ya tatu:-
Ni kuhusu suala la kuwa Hamad amechanganyikiwa mwishoni mwa umri wake, suala hili ni kweli na wanavyuoni wamelitaja kwenye vitabu vyao na linaweza kuyatia kasoro mapokezi ya mpokeaji, lakini

swali la msingi la kujiuliza ni wakati gani huko kuchanganyikiwa kutatia kasoro mapokezi hayo?

Ufafanuzi wake ni kama ufuatavyo:

Hukumu ya riwaya za mpokezi aliyechanganyikiwa mwishoni mwa umri wake si moja bali iko katika namna tatu:

i) Namna ya kwanza ni kuwa riwaya zote alizosimulia kabla ya kuchanganyikiwa na zikajulikana, riwaya hizo zitakubalika.

ii) Namna ya pili ni zile riwaya ambazo amezisimulia baada ya kuchanganyikiwa hizo hazitokubaliwa.

iii) Ni zile ambazo hazikujulikana kuwa amezisimulia kabla ya kuchanganyikiwa au baada yake, riwaya hizo hazitatumika mpaka zibainike, je zimesimuliwa kabla ya kuchanganyikiwa au baada?

Amesema Imamu al Nawawy:
"يقبل ما روي عنهم قبل الإختلاط ولا يقبل ما بعده أو شك فيه".

"Hukubaliwa (habari) zile ambazo zimepokewa kutoka kwa hao (walio changanyikiwa) kabla ya kuchanganyikiwa na hazitokubaliwa zilizokuwa baada yake, hata zile ambazo zimetiliwa shaka (kuwa ni baada au kabla pia hazitakubaliwa)".
Tazama Taqtribun-Nawaawy pamoja na Tad'ribul-raawiy juzuu ya 2 ukurasa 372.

Kwahiyo hukumu hii ya ujumla iliyotolewa na ndugu Juma na sheikh wake aliyemvika kilemba cha ukoka Al-Qannubi dhidi Hamad bin Salama haikufuata kanuni za kielimu, kwa sababu walikuwa wana wajibu wa kuthibitisha kitaalamu kwamba mpokezi aliyepokea hadithi hii kutoka kwa Hamad bin Salamah amesimuliwa baada yakuwa

tayari Hamad amechanganyikiwa, na wala si kwa kutoa hukumu kiujumla na hali ya kuwa jambo lina upambanuzi wa kielimu kama huu tulioutoa.
Na si Juma wala sheikh wake Qannubi anayeweza kufanya hivyo, na akijaribu ataumbuka, kwa sababu mpokezi aliyepokea hadithi hii kutoka kwa Hamad ibn Salama ni Abdul-rahaman bin Mah'di ambaye ni katika jumla ya wanafunzi wakubwa wa Hamad ambao wamepokea kutoka kwa sheikh wao Hamad bin Salama kabla ya kuchanganyikiwa.

Mpaka hapo ndugu msomaji utakuwa umegundua namna ndugu Juma na sheikh wake wanavyotumia ujanja ujanja katika masuala ya kielimu, na hakuna shaka kuwa kufanya hivyo ni kuwafanyia hiyana watu wasiojua na hiyo ni dhulma ya wazi.
Na hakuna budi kwa sheikh na mwanafunzi wake wakubali moja ya mambo mawili;
1-Wakubali kuwa wao ni waongo, wamekusudia kuwadanganya na kuwalaghai waislamu.
2-Au ni wajinga, wanasema katika elimu hii wasichokijua. Na kila watakalo lichagua kwao wao ni baya.

Baada ya Juma na sheikh wake kusema uongo na sisi kuubainisha uongo huo, sasa Juma na sheikh wake huyo aliyemuita kuwa ni imamu wa hadithi (Qannubi) wanaamua kumzulia sheikh Al-Bani.
Amesema Juma M. al-Mazrui katika kitabu chake "Hoja zenye nguvu" ukurasa wa 112 na hapa ninamnakili kama alivyoandika mwenyewe:
''Na akasema Al-albani (mwanachuoni wa hadithi wa kiwahabi) katika kitabu chake ''AL DHAIFA'' juzuu ya 2 ukurasa wa 333:
''hakika ya Hamad anakosea sana.''

Kisha akasema tena Juma:

‘‘Hii ni nakala kutoka katika kitabu ‘‘ALTUFAN AL-JAARIF LI KATAAIB AL-BAGHYI WAL-UDWAAN’’ juzuu ya 3 sehemu ya 1 ukurasa 308. cha Imam wa hadithi, fiq’hi na usuli Al-huja Said bin Mabruk al-qannubi.’’
Mwisho wa kunukuu.

MAJIBU YETU

Majibu yetu juu ya maneno haya ni kwa njia mbili:-

Njia ya kwanza:
Ni kama tulivyotangulia kusema hapo nyuma kwamba Juma na sheikh wake ima ni waongo au ni wajinga wasiofahamu maneno ya maulamaa, nimesema hivyo si kwa kutaka kuwakashifu na kuwadhalilisha, bali ninasema hivyo kwa sababu hii ifuatayo:

Maneno ya Sheikh Al-Bani -Allah amrehemu – yako kinyume na anavyosema Juma akinukuu kutoka kwa sheikh wake Al-Qannubi, na ukiyarejea maneno ya sheikh Al-Bani utayaona yamekuja baada ya kuitaja hadithi isemayo:

“Mwenye kuiacha sehemu ya unywele mmoja katika janaba na asiuoshe atafanywa kadha wa kadha huko motoni”. 2/332.
Hadithi hii imepokelewa kutoka kwa swahaba mtukufu Aliy –Allah amridhie- na katika sanad yake yumo Atwaa bin Saaib na Hamad bin Salamah.

Kisha akasema (sheikh Al-Bani):
“Amesema Imamu Ibn Hajar:
“Sanadi ya hadithi hiyo ni sahihi kwa sababu Atwaa amepokea kutoka kwa Hamad kabla ya Hamad hajachanganyikiwa, lakini

imesemwa kwamba; sahihi ni kuwa hadithi hii ni Mauquf kwa Aliy (maneno ya swahaba mtukufu Aliy na si maneno ya Mtume swalla llaahu alayhi wasallam)…".

Naye Imamu al-Nawawy akasema;

"Hadithi hii ni dhaifu kwa sababu Atwaa amedhoofishwa, na Hamad anakosea…".

Baada ya Sheikh Al-Bani kutoa maelezo ya maulamaa kuhusu hadithi hiyo ndiyo akaanza kulichambua kosa moja baada ya jingine lengo lake ni kuyachambua makosa ya kweli, na ambayo si makosa kwa mujibu wa misingi ya elimu ya ''mustalahul hadithi''.

Kwa sababu kuna baadhi ya maulamaa kama Imamu Al-Nawawy wameona kuwa miongoni mwa makosa yaliyopelekea udhaifu wa hadithi hiyo ya kuoga janaba ni kuwa Hamad bin Salama anakosea.

Sheikh Al-albani akasema kumtetea Hamad na kuwajibu wale walioidhoofisha hadithi hiyo kwa sababu ya Hammad, na haya yafuatayo ni maneno ya sheikh Al-Bani:

"وهذا التعليل واهٍ كالذي قبله فإن حماد بن سلمة إمام من أئمة المسلمين ثقة حجة ما فى ذلك شك ولا ريب ولا يخرجه من ذلك أن له أوهاماً وإلا فمن الذي ليس له أوهام؟ ولو كان الراوي الثقة يرد حديثه لمجرد أوهام له لما سلم لنا إلا القليل من جماهير الثقات من رجال الصحيحين فضلا عن غيرهما.
ولذلك جرى علماء الحديث سلفا وخلفا- منهم النووي – على الإحتجاج بحديث حماد بن سلمة إلا إذا ثبت وهمه...".
انظر سلسلة الأحاديث الضعيفة والموضوعة 2/332-333.

"Hii ni sababu nyonge kama ilivyo sababu iliyotangulia kabla yake, kwa sababu Hamad bin Salama ni IMAMU miongoni mwa maimamu wa kiislamu ni THIQA (muadilifu mwenye hifdhi nzuri) tena ni HOJA na hakuna shaka yoyote katika hilo, na suala la kukosea halimtoi katika daraja hiyo, kwani ni nani asiyekosea?

Lau kama kila mpokezi zitakataliwa hadithi zake kwa sababu ya kuwa anakosea tu, basi wasingesalimika ila wachache miongoni mwa kundi kubwa la watu Thiqaat (wadilifu wenye hifdhi nzuri) tena katika watu waliomo katika sahihi mbili (Sahihi Bukhari na Sahihi Muslim) wachalia mbali vitabu vingine.

Na kwenye hilo la kuzikubali hadithi za Hamad ndivyo walivyopita maulamaa wa hadithi waliotangulia na waliofuatia –na miongoni mwa hao ni huyo Imamu al Nawawy- isipokuwa itakapothibiti kukosea kwake".

Mwisho wa kunukuu.

Tazama Sil sila Dhaifa juzuu ya 2 ukurasa 332-333.

Hebu ndugu msomaji yasome tena maneno ya ndugu Juma ambayo amemnukuu sheikh wake al Qannubi kwa uangalifu,amesema bwana Juma:

"Na akasema Al-albani (mwanachuoni wa hadithi wa kiwahabi) katika kitabu chake "AL DHAIFA" juzuu ya 2 ukurasa wa 333:

"hakika ya Hamad anakosea sana".!!!

Mwisho wa kunukuu.

Ndugu msomaji, hebu linganisha maneno haya ya ndugu Juma na sheikh wake Al-Qannubi wanayodai kuwa ni maneno ya sheikh Al-albani, na hayo maneno yenyewe ya sheikh Al-albani ambayo tumeyakunukuu hapo juu kutoka kwenye kitabu chake, ukilinganisha utaona yanatofautiana sheikh Al-Bani anasema:

"HAMAD BIN SALAMA NI IMAMU MIONGONI MWA MAIMAMU WA KIISLAMU NI THIQA TENA NI HOJA NA HAKUNA SHAKA YOYOTE KATIKA HILO, NA SUALA LA KUKOSEA HALIMTOI KATIKA DARAJA HIYO, KWANI NI NANI ASIEKOSEA ?

Juma anadai kwamba sheikh Al-Bani amesema: "HAKIKA HAMAD ANAKOSEA SANA" na maneno hayo ameyanukuu Juma kutoka kwa sheikh wake al-Qannubi!

Bali la ajabu zaidi ni kuwa tunaona katika maneno ya sheikh Al-Bani kinyume chake: kwamba HAMAD NI IMAMU MIONGONI MWA MAIMAMU WA KIISLAMU, THIQA, TENA HOJA…?!

Bali isitoshe sheikh Al-Bani amemtetea sana Hamad dhidi ya wale wenye kudai kwamba anakosea.

Bila shaka ndugu msomaji kwa maelezo haya utakuwa umebainikiwa na uongo alioufanya Juma na sheikh wake al-Qannubi.Wameamua kufanya hivyo kwa makusudi baada kugundua kwamba sheikh Al-bani mwanachuoni mkubwa wa hadithi katika zama hizi, anayekubalika na waislamu wengi duniani tena kwa kiwango cha juu mno! Kwa hiyo wakaona wamtumie kama ngazi ili wafikie malengo yao mabaya, ndipo bila haya wala aibu wakaamua kumzulia uongo wa wazi.

Wameamua kumzulia uongo sheikh huyo ili msomaji akiyasoma maneno hayo moja kwa moja adhanie kwamba sheikh Al-albani naye ni miongoni mwa wanaomtia kasoro Hamad bin Salama na kumdhoofisha kwa sababu ya kukosea sana, na hali yakuwa hivyo sivyo kabisa ! bali ni uwongo mweupe kama jua la mchana wa saa sita. Na hapana shaka kuwa kitendo hiki ni kitendo kiovu tena cha kidhalimu, na huo si mwenendo wala sera za maulamaa waliosimama katika njia ya haki ambao lengo lao ni kutaka kuwaelimisha watu haki ili waifuate, bali hivyo ni vitendo vya watu wa batili waliofilisika katika hoja, kwa sababu siku zote mtu mkweli mwenye hoja zenye nguvu hayuko tayari kughushi wala kusema uongo katika suala lolote, wachilia mbali suala la dini, sasa inakuwaje mtu mwenye kudai uimamu na ijtihadi tena mcha Mungu awafanyie ghushi waislamu katika jambo la itikadi ya dini yao kwa sababu ya kulinda misimamo ya kimadhehebu na ukabila ?!
Bali kwa mujibu wa itikadi yao ya batili ya kikhawariji (kiibadhi) hiyo ni dhambi ya kumuingiza mtu motoni milele na wala hatoki tena, na hakuna wa kumuombea, na kama ataombewa basi maombi hayo hayatokubaliwa !
Na hapa Juma anajinyonga mwenyewe kwa kitanzi chake kwa sababu ya itikadi yao potofu, anasema katika kitabu chake "KISIMAMO KATIKA SALA" ukurasa wa 28 :

"Na unajua Sheikh X. ni kitu gani kimewafanya wanazuoni wa kiibadhi wasiseme uwongo?

Ni kwa sababu ya itikadi yao kwamba MADHAMBI MAKUBWA YANAMUWEKA MTU MOTONI MILELE NA YANAMPOROMOSHEA MEMA YAKE, NA UWONGO NI KATIKA MADHAMBI MAKUBWA".
Mwisho wa kunukuu.

Tazama hapa namna wanavyojinyonga na kamba yao wenyewe! Je wewe ndugu Juma, na sheikh wako Al-Qannubi hamuogopi kukaa motoni milele kwa kusema uongo? Je hamuogopi kuporomoshewa amali zenu na kuanguka uadilifu wenu?
Hivi ndugu Juma kwa sababu ya uongo wenu kama huu ndiyo mnataka kufanya mijadala na maulamaa wakubwa kama Ibn Baz -kama mnavyodai- na mko tayari kwenda kuapa kwenye Ka'aba?! Hamuogopi ?!
Hivi kweli mnaweza kudai kwamba mwanchuoni mkubwa kama al-Allaama sheikh Abdul-Aziz Ibn Baz awakimbie watu kama nyinyi wenye hoja dhaifu tena za uongo namna hii ?!!!
Kama mkiwa mmeweza kupotosha yaliyoandikwa vitabuni ambayo yako dhahiri shahiri, na mkaweza kuwazulia maulamaa mambo ambayo hawakusema, kweli mtashindwa kuzipotosha, na kuzigeuza habari zilizofanyika ndani ya ofisi tena kwa siri, tena mashahidi wa tukio hilo ni nyinyi wenyewe? Eti Ibn Bazi amkimbia Khalili! Kwa hoja gani alizonazo Khalili na wafuasi wake? Hoja zenyewe ni hizi za uwongo anazozitaja Juma kutoka kwa Qannubi na Khalili?
Vitabu vya Al-bani vimejaa ulimwenguni mashariki na magharibi, mmemzulia wazi wazi ! je mtashindwa kuzua yaliyofanyika ofisini kwa siri?

Ndiyo maana ukiyatazama maneno ya Juma kuhusu suala la kukutana Ibn Baz na Khalili utauona uongo unaelea juu juu, kwa mfano pale aliposema:
"Kwa hivyo Al-khalili akamtaka Bin Baz ambaye kawaita maibadhi MAKAFIRI wende mbele ya Al-kaba Takatifu wakaombe hivi hivi, lakini Bin Baz akaogopa.

Na hii inatosha kuonesha kuwa hata yeye mwenyewe sh. Bin Baz hana hakika na itikadi yake.
Na kama si hivyo kipi kimemzuia kumtaka Mwenyezi Mungu aibainishe haki baina yake na watu ambao kawaita makafiri."!!!!
Mwisho wa kunukuu uwongo wa ndugu Juma.
Tazama kitabu chake "Hoja zenye Nguvu" ukurasa wa 42.

Je ni kweli Ibn Baz amewaita maibadhi makafiri?
Ni mahali gani hapo? Kitabu gani ? Mbona hukututajia?
Vitabu vya Ibn Baz vimejaa tele hapa duniani, hebu tutajie kitabu kimoja ambacho Ibn Baz amesema maneno hayo, na hii ni chalenji nina kupa wewe Juma na masheikh zako Khalili, al-Qannubi, na Ahmad bin Su'ud al-Siyabi mtutajie ni mahali gani Ibn Baz amewaita maibadhi kuwa ni makafiri kwa uwazi kabisa, bila ya kuhitajia taawili.
Na haya ndiyo maajabu ya makhawariji hawa wa akhiril-zaman! Wanasema uongo wala hawana haya, na vitabu vyao vimejaa uongo. Kwa ushahidi zaidi hebu tukudokolee mfano mmoja wa uongo wao na mingine itafuatia katika sehemu zake, ni pale mufti wao Khalili alipoamua kulipindua shairi la Ibnul-Qayyim kwa makusudi, kisha Juma naye akafuatia vivyo hivyo ! Ametaja al-Khalili katika kitabu chake AL-HAQU DAMIGH, naye Juma katika kitabu chake "Kisimamo" ukurasa wa 93 akasema hivi:
"Na akasema katika "NUNIA" kuhusu wote ambao hawana itikadi ya kihashawiya (Kiwahabi) kwamba ni maaduwi ambao ukafiri wao ni mkubwa kuliko mushrikina (wenye kuabudu masanamu) Anasema (Ibnul-Qayyim):

إن المعطل بالعداوة معلن * والمشركون أخف فى الكفران**

Na muatil ni mwenye kuutangaza uadui *** na washirikina ni wepesi zaidi katika ukafiri."
Juma na mufti wake Khalili wameyapindua maneno haya ya Ibnul-Qayyim kwa makusudi, mimi ninawapa chalenji watuletee maneno

haya, na mimi ninasema kwamba maneno haya hayamo katika "NUNIA" ya Ibnul-Qayyim.
Maneno yaliyomo katika "NUNIA" ni haya:

إن المعطل بالعداوة معلن** * فى قالب التنزيه للرحمن

Na muatila ni wenye kuutangaza uadui *** kwa sura ya kumtakasa Rah'man (Allah mwingi wa reh'ma).

Haya ndugu msomaji ni machache kati ya mengi ya uongo yaliyojaa kwenye vitabu vya makhawarij (maibadhi) wa zama hizi, mpaka Mufti wao pia asema uongo! Na inaonekana kuwa Juma hasomi vitabu kwa kuhakiki mambo, bali yeye ananukuu kiupofu kutoka katika vitabu vya masheikh zake Khalili na Qannubi.

Hebu tuendelee kuyatupia macho maneno ya ndugu Juma al-Mazrui katika kitabu chake "Hoja zenye Nguvu" ukurasa wa 113, kuhusu hadithi hii, anasema ndugu huyo:

"KASORO YA PILI YA HADITHI HII:
NAKALA KUTOKA KWA AL-QANNUBI.

Jambo la pili ni kuwa hadithi hii ina kasoro ya pili nayo ni kuwa **"موقوف"** (haitoki kwa Mtume (S.A.W.). Anasema Al imamu Al-tirmidhi "hadithi hii HAMAD BIN SALAMA kainasibisha na Mtume (S.A.W.) (Wala haitoki kwake) na ameipokea (hadithi hii) Hamad bin Zaid na Sulaimaan bin Mughira kutoka kwa Thabit Al-banaani kutoka kwa Abdul-rahmaan bin Abi Leila (ni) KATIKA MANENO YAKE" (yaani hadithi hii ni maneno ya Abdul-rahamaan bi Abi Leila na si maneno ya Mtume (S.A.W.)....".
Kisha akasema tena ndugu Juma al Mazrui:
"Mpaka hapa inatubainikia kwamba hadithi hii si ya kutegemea...".
Mwisho wa kunukuu.

Njia ya kwanza:

Kama tulivyotangulia kukutajia kauli za maulamaa wa hadithi kuhusu riwaya za Hamad bin Salama kutoka kwa Thabit al-Bunaani (hapa ndugu Juma amekosea kwa kumuita Al-banaan, na sahihi ni Al – bunaani) kwamba yeye Hamad bin Salama ni mtu madhubuti zaidi kwa mapokezi kutoka kwa Thabit na iwapo atatokea mtu yeyote kupingana na mapokezi ya Hamad bin Salama kutoka kwa Thabit basi kauli ya kuchukuliwa ni kauli ya Hamad.

Na hapa tunaona kwamba Hamad bin Zaid na Sulaimaan Ibnul-Mughira wawili hawa wametofautiana na Hamad bin Salama katika riwaya hii kutoka kwa Thabit al-Bunaani.

Amesema Imamu Yahya bin Mai'n:

وقال ابن معين: من خالف حماد بن سلمة فى ثابت فالقول قول حماد.

"Yeyote atakayetofautiana na Hamad bin Salama katika (mapokezi yake kutoka) kwa Thabit, basi kauli (ya kuchukuliwa) ni kauli ya Hamad".

Tazama Mizanul I'tidali 1/591.

Njia ya pili:

Hamad bin Zaid ni mashuhuri kwa tabia ya kuzifanya Mawquuf hadithi ambazo ni Mar fu'u au kwa lugha nyingine ana tabia ya kuzinasibisha na Maswahaba kauli ambazo ni za Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- huwenda hapa pia amelifanya jambo hilo.

Amesema Imamu Ya'aqub bin Shaibah:

"Hamad bin Zaid ni madhubuti zaidi kuliko Hamad bin Salama na wote hao ni watu Thiqa isipokuwa Hamad bin Zaid ni maarufu kwa kuzifupisha isnadi na kuzifanya kuwa Mawqufu hadithi ambazo ni Marfu'u..".

Tazama Tah'dhibul-Tah'dhibi juzuu2 ukurasa 10.

Njia ya tatu:

Zimepokewa hadithi nyingine nyingi kutoka kwa Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- na kauli nyingi kutoka kwa Maswahaba zinazoitilia nguvu hadithi hii ambayo katika sanadi yake yumo Hamad bin Salama ambaye ni mtu madhubuti zaidi katika riwaya za Thabit al-Bunaani kuliko wapokezi wote wanaopokea kutoka kwa Thaabit.

Mpaka hapo ndugu msomaji utakua umebainikiwa na majibu yetu juu ya sanadi ya hadithi hii dhidi ya upotoshaji uliofanywa na jamaa hawa, na -wali llaahil hamdu – hoja zetu zimekubainikia dhidi ya hoja dhaifu za bwana Juma na sheikh wake.

Kisha ndugu Juma akazidhoofisha riwaya nyingine ambazo nyingi katika hizo wapokezi wake ni dhaifu, na hakuishia hapo tu, bali hata hadithi nyingine ambazo ni sahihi zilizopokelewa kwa njia nyingi lakini baadhi yake zina udhaifu pia amezidhoofisha, kinyume na ulivyo utaratibu katika taaluma ya elimu hii ya mambo ya hadithi.

Ndugu Juma yeye hakuzichunga kanuni hizo wala hakuzijali, na akazidhoofisha hadithi hizo bila ya kuheshimu kanuni za taaluma hii.

Kisha akahitimisha maudhui kwa mukhtasari kwa kusema:

"Mpaka hapa tumefikia mwisho wa mjadala wetu wa kuielezea aya ya 26 ya sura ya 10 yenye kusema:

لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَى وَزِيَادَةٌ

"*Wale waliofanya mema watalipwa wema na ziada*".

Pamoja na riwaya zake ambazo wamezitegemea wale wenye kuitakidi kumuona Mwenyezi Mungu katika tafsiri yao hiyo.Tumebainisha kwa ushahidi wa kielimu kuwa riwaya hizi zote ni batili: hakuna hata riwaya moja ambayo ni sahihi: zote zimesimuliwa na wapokezi madhaifu, wenye kughushi na waongo".

Mwisho wa kunukuu.

Tazama ukurasa 132-133 katika kitabu chake.

Hayo ndiyo yalikuwa malengo yake makubwa ya ule mchezo wake mchafu wa kuzidhoofisha hadithi za Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam-, aliamua kwa makusudi kuyapindisha baadhi ya maandiko na kupotosha maana zake ili afikie kwenye lengo hili, nalo si lengo jingine zaidi ya kupingana na tafsiri sahihi ya bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- alioitoa juu ya aya 26 ya surat Yunus !
Ili yeye atuletee tafsiri yake ambayo itaafikiana na madhehebu yake ya kiibadhi inayopinga kuonekana Allah huko akhera kwa macho, na ndiyo maana hakuufanya utafiti wake kuwa ni wa kielimu ulio na insafu (uadilifu), bali akatumia zaidi uongo na hila.
Lakini uhakika wa mambo si kama alivyodai ndugu huyo, kwamba hadithi zote zilizoitafsiri aya hii ni batili, bali ni kama tulivyokuthibitishia kielimu na uadilifu kwamba:

-Ziko riwaya ambazo wapokezi wake ni dhaifu na hakuna namna ya kuzipa nguvu.

-Na ziko riwaya nyingine ambazo wapokezi wake ni madhubuti, na kama kuna kasoro ndogo ndogo basi ni zile za kibinaadamu ambazo kiutaalamu haziyaathiri mapokezi yao bali zinaweza kukubalika kwa kujumuishwa na riwaya nyingine zinazozitiliana nguvu.

-Pia ziko riwaya ambazo ni sahihi na wala hazina shaka juu ya usahihi wake. Kama riwaya hii tuliyoitaja hapo nyuma.

Amesema tena ndugu Juma:
"Na neno "ZIADA" ambalo limo katika aya hii, Mwenyezi Mungu hakusema ni ziada gani.
Na kwahivyo haitakiwi tudai katika mambo ya itikadi kitu ambacho hakina ushahidi sahihi".

Mwisho wa kunuku.Tazama katika kitabu chake hicho ukurasa wa 133.

Majibu yetu ni kwa njia mbili:

a) Kama yakiwa makusudio ya Juma ni kwamba hakuna aya ya Qur'an iliyoelezea maana ya neno ziada, hilo ni kweli.

b) Lakini kama anakusudia kuwa hakuna kabisa hata katika maneno ya mjumbe wa Allah, bila shaka hilo si kweli, kama tulivyolithibitisha hilo kupitia hadithi sahihi ya bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- alipokuwa akiitafsiri aya hii kama ilivyokuja katika hadithi hii ambayo:-

Imepokewa kutoka kwa Suheib, kutoka kwa Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- amesema kuhusiana na kauli ya Allah:

"Wale waliofanya mema watapata wema na ziada".

Akasema Mtume swalla llaahu alayhi wasallam:-

"Watakapoingia watu wa peponi katika pepo atanadi mwenye kunadi: hakika nyinyi mna ahadi mbele ya Allah anataka kukutekelezeeni.

Watasema kwani hukuzing'arisha nyuso zetu na ukatuokoa na moto na ukatuingiza peponi?

Akasema (Mtume swalla llaahu alayhi wasallam):

BASI LITAONDOLEWA PAZIA NA WATAMTAZAMA YEYE ALLAH NA HAWAJAWAHI KUPEWA KITU WANACHOKIPENDA MNO KULIKO HUKO KUMTAZAMA YEYE ALLAH NA HIYO NDIYO ZIADA".

Hadithi hii ni sahihi imepokewa na Imamu Muslimu tazama sahihul muslim hadithi namba 449.

Bila shaka tafsiri hii ya bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- inaukata mzozo uliopo baina ya wale wenye kuitakidi kuonekana Allah huko akhera kwa macho na wale wenye kuipinga itikadi hiyo.

Na haipingi hukumu hii ya Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- ila yule ambaye moyo wake umejaaa unafiki, kibri, na kufuata matamanio ya nafsi yake.

Ama kuhusu majaribio ya ndugu Juma ya kutaka kuidhoofisha hadithi hii bila shaka majaribio hayo yamefeli kama ilivyokudhihirikia katika uchambuzi wetu.

Kisha akasema tena:
"Na kwa kutazama hizo kauli nyengine tofauti zilizosemwa basi utaona kuwa iliyokaribu na usahihi ni kauli ya Alqama bin Qais ambaye amesema kwamba "ZIADA" hapa ni kuzidishwa matendo ya watu wema aliyefanya moja akalipwa mara kumi ya wema wake..".
Mwisho wa kunukuu.
Tazama katika kitabu chake "Hoja zenye nguvu"ukurasa wa 133.

MAJIBU YETU

Majibu yetu hapa ni kwa njia tatu:
Njia ya kwanza:
Kila muislamu anatakiwa kuamini kwamba Allah ni mwingi wa fadhila mwingi wa huruma kwa waja wake, amewakirimu waja wake kwa fadhila nyingi hapa duniani, na ataendelea kuwakirimu zaidi huko akhera, atawapa waja wake fadhila nyingi mpaka waridhike.
Kwa kuwa yamekuja maandiko tofauti ambayo yanaelezea kuwa watu wema huko akhera watalipwa wema wao na ziada juu, tunatakiwa kuyakubali maandiko yote sahihi yaliyo tufahamisha hivyo, na kufanya hivyo si kuthibitisha mgongano baina ya maandiko hayo, ndiyo maana akasema Imamu Ibn kathir katika kitabu chake cha tafsiri alipokua akiitafsiri aya isemayo:

لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَى وَزِيَادَةٌ وَلَا يَرْهَقُ وُجُوهَهُمْ قَتَرٌ وَلَا ذِلَّةٌ أُولَئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمْ فِيهَا خَالِدُون (26)

"Na wale waliofanya mema watapata wema na ziada.Wala vumbi halitawafunika nyuso zao, wala madhila.Hao ndio watu wa Peponi. Humo watakaa milele." Yunus 26.

Akasema Ibn Kathir:

وقوله: { وَزِيَادَة } هي تضعيف ثواب الأعمال بالحسنة عشر أمثالها إلى سبعمائة ضعف، وزيادة على ذلك أيضا ويشمل ما يعطيهم الله في الجنان من القُصُور والحُور والرضا عنهم، وما أخفاه لهم من قرة أعين، وأفضل من ذلك وأعلاه النظرُ إلى وجهه الكريم، فإنه زيادة أعظم من جميع ما أعطوه، لا يستحقونها بعملهم، بل بفضله ورحمته ."

Na kauli yake (Allah): "ZIADA" ni kuzidishiwa malipo ya matendo; jema moja utazidishiwa mema kumi mfano wake, mpaka ziada mia saba, na zaidi ya hapo. Pia ziada itakusanya yale yote atakayowapa Allah huko peponi: Makasri, Hurul-a'in (wanawake wa peponi), radhi zake Allah, na yale aliyowafichia miongoni mwa vitulizo vya jicho na (ZIADA) ILIYO BORA KULIKO ZOTE, NA ILIYO JUU ZAIDI NI KUUTAZAMA USO WAKE ALLAH ULIOMTUKUFU. Kwa sababu hiyo ndiyo ziada kubwa kuliko vitu vyote walivyopewa, na hawakustahiki kupata hilo kwa sababu ya matendo yao, bali ni kwa fadhila zake (Allah) na rehma zake".

Mwisho wa kunukuu.

Tazama tafsirul Qur'anil adhim juzuu 4 ukurasa chapa ya kwanza ya daaru Ibn Hazm ya mwaka 1419=1998.

Kwa mujibu wa maneno hayo ni kwamba watu watapata ziada nyingi, na miongoni mwa ziada hizo ni: kwamba yule aliyefanya wema mmoja atalipwa mara kumi ya wema wake, na hali kadhalika atafadhiliwa kumuona mola wake -Jalla jalaaluh-, na kuyatafsiri maandiko kwa namna hii ni kuitumia ile kanuni ya upatanisho (the juristic law of reconciliation between the apparently conraditory texts) kanunni ya upatanisho baina ya maandiko ambayo dhahiri yake yanagongana, kanuni ambayo ndugu Juma pia ameikubali, na kuitumia kama alivyoielezea katika ukurasa wa 261 katika kitabu chake.

Lakini kwa masikitiko makubwa kabisa, ameshindwa au hakutaka kuifanyia kazi kanuni hiyo aliyoikubali mwenyewe na alipofika kwenye maandiko haya yaliyokuja kuitafsiri aya hii akaitupilia mbali kwa sababu haiendi sambamba na itikadi yake!

Njia ya pili:

Je, unajua ni kwanini ndugu yangu msomaji ndugu yetu Juma ameipa nguvu kauli ya Alqama bin Qais? Ni kwa sababu riwaya hiyo ina nguvu kuliko riwaya nyingine? Au ameipa nguvu kwa sababu inaafikiana na msimamo wake batili?

Jawabu ni hili hapa:

Ndugu Juma ameipa nguvu kauli ya Alqama bin Qais si kwa sababu kuwa ni sahihi na ina nguvu, bali ni kwa sababu inaafikiana na msimamo wake batili.

Na kama utaifanyia utafiti wa kielimu riwaya hiyo utaona kwamba miongoni mwa wapokezi wake ni "IBN HUMAID" (jina lake kamili ni; MUHAMMAD BIN HUMAID BIN HAYYAAN AL-TAMIMI AL-RAZI) kama alivyoeleza Ibn Jarir al-Twabariy katika kitabu chake cha tafsiri juzuu ya 11 ukurasa 125.

Ibn Humaid huyo huyo ndiye yule ambaye ndugu yetu Juma alimtia kasoro na kuidhoofisha riwaya yake, kama alivyoelezea katika kitabu chake "Hoja zenye Nguvu" ukurasa 123. Lakini hapa bwana Juma anaitaja riwaya yake na anaipa nguvu!

Hivi inakuwaje mpokezi mmoja huyo huyo ambaye ametuelezea kwa vishindo kwamba ni dhaifu, mwongo !!! Mara ghafla anakuja kutubadilikia na kutwambia kwamba riwaya yake ni sahihi tena ndiyo yenye nguvu !!! Je hapo kuna uadilifu?!

Kauli ya Juma kuhusu Ibn Huamid:

Hebu ndugu msomaji ni kunakilie maneno ya Juma alipokuwa akimuelezea Ibn Humaid, amesema Juma:

"Sanad hii ni dhaifu sana kwa sababu ina msururu wa wapokezi madhaifu na waongo…".

Kisha akasema:

1) IBN HUMAID na jina lake kamili ni MUHAMMAD BIN HUMAID BIN HAYAAN AL-TAMIMI AL-RAZI….amesema Is'haq bin Mansur al-kuusaj! Akisimulia kauli ya Ali bin Mihran juu ya MUHAMMAD BIN HUMAID akisema kwamba;

> “sijapata kuona mtu （anayejifanya） jasiri juu ya Mwenyezi Mungu （hamuogopi Mwenyezi Mungu） kuliko yeye alikuwa akizichukua hadithi za watu kisha akizigeuza” Na akasema tena kuwa “sijapata kuona mtu bingwa wa uwongo kuliko watu wawili: Sulaiman Al-shadhakuni na MUHAMMAD BIN HUMAID”.！！！ Mwisho wa kunukuu.

Tazama katika ukurasa wa 122-123 katika kitabu chake “Hoja zenye Nguvu”.

Haya ndugu msomaji bila shaka umejionea mwenyewe namna watu hawa wanavyocheza karata tatu！ Inakuaje mpokezi akipokea riwaya inayopingana na msimamo wa kiibadhi hafai ni dhaifu, anaghushi, muongo, na riwaya zake hazikubaliki, tena mpaka inafikia kiwango cha kuwazulia baadhi ya maulamaa uongo ilimradi dau lifike pwani.

Lakini mpokezi huyo huyo akipokea riwaya ambazo zinaafikiana na msimamo wa kiibadhi basi riwaya hizo hazina neno bali ndizo zenye nguvu！！！

Bila shaka ndugu msomaji mpaka hapa utakuwa umethibitisha yale niliyokuambia huko nyuma kwamba: hawa watu wako katika kutetea itikadi zao tu, tena si kwa uadilifu wala kwa hoja za kielimu, bali wako tayari kuupindisha ukweli kwa mas’lahi yao, mpokezi mkweli ni yule anayepokea riwaya za kuwaunga mkono wao, ama yule anayepokea riwaya kinyume na itikadi zao za kikhawariji basi huyo ni muongo,dhaifu, anaghushi na tuhuma nyingi za uongo.

Nadhani ndugu msomaji umejionea mwenyewe, mpokezi mmoja huyo huyo amepewa hukumu mbili tofauti！ Huko nyuma riwaya yake ina nguvu, lakini hapa ni muongo na hakuna muongo kama yeye！！！

Siku zote mtu unapofanya utafiti wa kielimu, kwa lengo la kuwafaidisha watu na utafiti wako, basi ni lazima uwe na sifa kuu mbili:

1） Elimu ya kutosha juu ya jambo unalolifanyia utafiti.

2） Uwe mkweli na muaminifu katika utafiti wako.

Na sifa zote hizi Juma amezikosa, na kama mtu atakosa sifa moja kati ya hizo mbili lazima kutapatikana upotoshaji wa haki na wala ukweli hautakuwepo, sikwambii zikikosekana sifa zote mbili.
Lakini hilo halinishangazi sana kwa sababu hizo ndizo sera za Ahlul ah'waa (watu wanaofuata matamanio yao katika mambo ya dini).

MUKHTASARI.

Kwa ufupi ni kwamba watu wema watakaoingia peponi, Allah -jalla jalaaluh- atawakirimu kwa neema nyingi mno na kubwa katika neema hizo ni kupata radhi zake na kumuona yeye -sub'haanahu wata'alaa- kwa macho yao.

Na miongoni mwa ushahidi wa jambo hilo ni aya hiyo ya 26 katika surat Yunus (10) aya ambayo imetafsiriwa na bwana Mtume Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam- Mtume ambaye ametumwa kwa kazi hiyo ya kuwabainishia watu yale yaliyoletwa kutoka kwa mola wao, na katika tafsiri yake mjumbe huyo mtukufu anasema kwamba neno "ZIADA" lililotajwa katika aya hiyo maana yake ni KUMUONA ALLAH -sub'haanah- huko peponi, na hilo limepokewa kwa mapokezi yaliyo sahihi kabisa ambayo hayana shaka ndani yake japokuwa ndugu Juma na kaumu yake walijaribu kuyatia dosari.
Kwa hiyo tunasema kwamba itikadi ya kuonekana Allah huko akhera ni itikadi sahihi ambayo imeelezewa na Qur'an tukufu kitabu ambacho hakiingiliwi na mambo batili, na Sunna sahihi za Mtume Muhammad swalla llaahu alaihi wasallam, na wakaichukua itikadi hiyo Maswahaba zake watukufu Allah awaridhie.

HOJA YA TATU

Hoja ya tatu wanayoitegemea Ah'lu Sunna katika kuithibitisha kuonekana Allah kwa macho huko akhera ni hadithi sahihi

zilizopokelewa kutoka kwa Mtume Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam-.

Inshaallaha katika sehemu hii tutazitaja hadithi ambazo zimethibiti kutoka kwa bwana Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- kwa mapokezi yaliyo sahihi yasiyo na shaka yoyote kwa kuzingatia kanuni za mapokezi ya hadithi.
Na hadithi sahihi juu ya mas'ala haya ziko nyingi mno, lakini hapa tutazitaja kwa uchache tu kwa lengo la kufupisha.
Ama kuhusu chalenji aliyoitoa Juma ya kutaka aletewe hadithi moja tu sahihi, ni chalenji ambayo haina uzito wowote wa kielimu, maana Juma amejigamba na kujisifu kwa kusema katika kitabu chake "KISIMAMO KATIKA SALA" ukurasa wa 22:
"Chukua- kwa mfano, hadithi za kuonekana kwa Mungu: Hadithi hizi ziko kwa wingi, lakini na kuchalenj Sheikh X. wewe na wanazuoni wako uniletee hadithi moja tu sahihi inayosema kwa uwazi kwamba Mungu ataonekana."!!!
Mwisho wa kunukuu.

Tazama namna watu walivyo na jeuri na kiburi katika mas'ala ya elimu ! badala ya kuomba msaada wa kuelimishwa juu ya mas'ala ya kielimu asiyoyajua, yeye analeta lugha ya kiburi na jeuri, eti: nakuchalenj uniletee hadithi moja tu sahihi inayosema kwa uwazi kwamba Mungu ataonekana !!!
Mtu mwenyewe anayesema hivyo kazi yake kunukuu tu kutoka kwa masheikh zake wala hawezi kuyahakiki mambo ya kielimu, wakikosea naye anakosea, wakidanganya naye anadanganya kama ulivyojioenea.

Sisi tunamwambia ndugu Juma awache jeuri na kibri ajitahidi kusoma na kufanya utafiti zaidi kwa misingi ya uadilifu haki itambainikia badala ya kung'ang'ani kasumba za kujikweza na kufuata umadhehebu.

Na hizi zifuatazo ni baadhi ya hadithi sahihi zinazosema kwa uwazi kabisa kwamba watu wema watamuona Mola wao huko akhera kwa macho:

HADITHI YA KWANZA

Hadithi hii imepokewa kwa njia nyingi, lakini kwa kufupisha tutazitaja baadhi ya njia hizo:

Njia ya kwanza:

قال الإمام البخاري رحمه الله:
حَدَّثَنَا عَمْرُو بْنُ عَوْنٍ حَدَّثَنَا خَالِدٌ وَهُشَيْمٌ عَنْ إِسْمَاعِيلَ عَنْ قَيْسٍ عَنْ جَرِيرٍ قَالَ
كُنَّا جُلُوسًا عِنْدَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذْ نَظَرَ إِلَى الْقَمَرِ لَيْلَةَ الْبَدْرِ قَالَ إِنَّكُمْ سَتَرَوْنَ رَبَّكُمْ كَمَا تَرَوْنَ هَذَا الْقَمَرَ لَا تُضَامُونَ فِي رُؤْيَتِهِ...."

Amesema Imamu al-Bukhari:
Ametusimulia Amru bin Aun, amesema: ametusimulia Khalid na Hushaim, kutoka kwa Ismail, kutoka kwa Qais, kutoka kwa Jarir:
Tulikua ni wenye kukaa mbele ya Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- kwa ghafla akautazama mwezi, katika usiku wa mwezi mpevu, akasema:
Kwa hakika nyinyi mtamuona Mola wenu kama mnavyouona huu (mwezi) hamtasongamana katika kuuona....".
Tazama Sahihul-Bukhari, hadithi namba 6882.

Njia ya pili:

قال الإمام مسلم رحمه الله:
حَدَّثَنَا زُهَيْرُ بْنُ حَرْبٍ حَدَّثَنَا مَرْوَانُ بْنُ مُعَاوِيَةَ الْفَزَارِيُّ أَخْبَرَنَا إِسْمَعِيلُ بْنُ أَبِي خَالِدٍ حَدَّثَنَا قَيْسُ بْنُ أَبِي حَازِمٍ قَالَ سَمِعْتُ جَرِيرَ بْنَ عَبْدِ اللَّهِ وَهُوَ يَقُولُ:
كُنَّا جُلُوسًا عِنْدَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذْ نَظَرَ إِلَى الْقَمَرِ لَيْلَةَ الْبَدْرِ فَقَالَ أَمَا إِنَّكُمْ سَتَرَوْنَ رَبَّكُمْ كَمَا تَرَوْنَ هَذَا الْقَمَرَ لَا تُضَامُّونَ فِي رُؤْيَتِهِ...." م

Amesema Imamu Muslimu -Allah amrehemu-:
Ametusimulia Zuhayr Ibn Har'bi, amesema: ametusimulia Mar'wan Ibn Mua'wiya al-Fazaariy, amesema: ametusimulia Ismail Ismail Ibn Abi

Khalid, amesema ametusimulia Qais Ibn Abi Hazim, amesema: nimemsikia Jarir Ibn Abdillahi anasema:

Tulikua ni wenye kukaa mbele ya Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- kwa ghafla akautazama mwezi, katika usiku wa mwezi mpevu, akasema:

Kwa hakika nyinyi mtamuona Mola wenu kama mnavyouona huu (mwezi) hamtasongamana katika kuuona....".

Tazama Sahihu Muslim, hadithi namba 1002.

Njia ya tatu:

قال لإمام أبو داود رحمه الله:

حَدَّثَنَا إِسْحَقُ بْنُ إِسْمَعِيلَ حَدَّثَنَا سُفْيَانُ عَنْ سُهَيْلِ بْنِ أَبِي صَالِحٍ عَنْ أَبِيهِ أَنَّهُ سَمِعَهُ يُحَدِّثُ عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ قَالَ نَاسٌ يَا رَسُولَ اللَّهِ أَنَرَى رَبَّنَا يَوْمَ الْقِيَامَةِ قَالَ هَلْ تُضَارُّونَ فِي رُؤْيَةِ الشَّمْسِ فِي الظَّهِيرَةِ لَيْسَتْ فِي سَحَابَةٍ قَالُوا لَا قَالَ هَلْ تُضَارُّونَ فِي رُؤْيَةِ الْقَمَرِ لَيْلَةَ الْبَدْرِ لَيْسَ فِي سَحَابَةٍ قَالُوا لَا قَالَ وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَا تُضَارُّونَ فِي رُؤْيَتِهِ إِلَّا كَمَا تُضَارُّونَ فِي رُؤْيَةِ أَحَدِهِمَا. د

Amesema Imamu Abu Daud -Allah amrehemu:-

Ametusimulia Is'aq Ibn Ismail, amesema: ametusimulia Sufyani, kutoka kwa Suheil Ibn Abi Swaleh, kutoka kwa baba yake (Abu Swaleh) kwamba amemsikia yeye akisimulia kutoka kwa Abu Hurayra, amesema: walisema watu: Ewe Mtume wa Allah ! Je tutamuona Mola wetu siku ya Qiyama?

Akasema: Je mnadhuriana katika kuliona jua wakati wa mchana ambao hakuna mawingu?

Wakasema: hapana. Akasema (Mtume): Je mnadhuriana katika kuuona mwezi katika usiku wa mwezi mpevu na hali hakuna mawingu? Wakasema: hapana. Akasema (Mtume): Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake, hamtodhuriana katika kumuona yeye (Allah) kama msivyo dhuriana katika kukiona kimoja kati ya hivyo (jua na mwezi)."

Tazama kitabu Sunan Abi Daud, hadithi namba 4105.

Njia ya nne:

قال الإمام أحمد بن حنبل رحمه الله:

حَدَّثَنَا يَحْيَى بْنُ آدَمَ حَدَّثَنَا أَبُو بَكْرِ بْنُ عَيَّاشٍ عَنِ الْأَعْمَشِ عَنْ أَبِي صَالِحٍ عَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ قَالَ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ:
" إِنَّكُمْ سَتَرَوْنَ رَبَّكُمْ عَزَّ وَجَلَّ قَالُوا يَا رَسُولَ اللَّهِ نَرَى رَبَّنَا قَالَ فَقَالَ هَلْ تُضَارُّونَ فِي رُؤْيَةِ الشَّمْسِ نِصْفَ النَّهَارِ قَالُوا لَا قَالَ فَتُضَارُّونَ فِي رُؤْيَةِ الْقَمَرِ لَيْلَةَ الْبَدْرِ قَالُوا لَا قَالَ فَإِنَّكُمْ لَا تُضَارُّونَ فِي رُؤْيَتِهِ إِلَّا كَمَا تُضَارُّونَ فِي ذَلِكَ".

Amesema Imamu Ah'mad Ibn Hanbal:

Ametusimulia Yahya Ibn Adam, ametusimlia Abu Bakri Ibn Ayyash, kutoka kwa A'mashi kutoka kwa Abu Swaleh, kutoka kwa Abu Said al-Khud'riy-Radhiyallaahu An'hu- amesema: amesema Mtume – swalla llaahu alayhi wasallam-:

Kwa hakika nyinyi mtamuona Mola wenu -Azza Wajalla-, wakasema (Maswahaba): Ee Mtume wa Allah! Tutamuona Mola wetu?

Akasema (Mtume): Je mnadhuriana katika kuliona jua katika nusu ya mchana ? wakasema: Hapana.

Akasema (Mtume): Je mnadhuriana katika kuuona mwezi katika usiku wa mwezi mpevu? Wakasema: Hapana.

Akasema: basi nyinyi hamtadhuriana katika kumuona yeye (Mola wenu) kama ambavyo hamdhuriani katika kuliona (jua na mwezi mpevu)."

Tazama katika kitabu "Musnad" cha Imamu Ahmda, hadithi namba 10697.

Kadhalika ameitaja hadithi hii Imamu al Bukhari katika Sahihul-Bukhari hadithi namba 7434.Na Imamu Muslimu katika Sahihi yake hadithi namba 182.Na Imamu Ibn Abi Asim hadithi namba: 443,444,445,446,447,448,449 mpaka 458.

SANADI YA HADITHI HII

Ama kuhusu sanadi ya hadithi hii:

Sanadi yake ni sahihi na wala hakuna mwanachuoni yeyote wa hadithi aliyeitia dosari zaidi ya Juma na sheikh wake al-Qannubi na Inshaallah utaliona jawabu letu dhidi ya ubabaishaji wao.

KUHUSU MAT'NI YA HADITHI HII:

Ama kuhusu maana ya hadithi:

Bila shaka hadithi hii iko wazi kabisa na wala haihitajii maelezo marefu ili ieleweke, isipokuwa kuna jambo muhimu la kutanabahisha nalo ni kwamba:

Bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- ametubainishia kuwa tutamuona Allah -Sub'haanah- kwa uwazi kabisa bila ya kudhuriana wala msongamano wowote, kama vile ambavyo watu hawasongamani wala hawakanyagani katika kuutazama mwezi mpevu wa tarehe kumi na nne, na kama vile ambavyo watu hawasongamani wala hawakanyagani katika kulitazama jua la mchana ambao hakuna mawingu.

Na zimepokewa hadithi nyingi ambazo zina maana kama hii walizozipokea Maswahaba wengi kutoka kwa Mtume Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam-, lakini kwa kufupisha tutosheke na riwaya hizi chache zilizo pokelewa kutoka kwa Maswahaba watatu wa Mtume Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam- (Jarir Ibn Abdillahi, Abu Said al-Khud'riy na Abu Huraira Allah awe radhi nao, na mwenye kutaka ziada basi arejee vitabu vya hadithi.

Na muislamu yeyote mwenye imani ya kweli akifikiwa na habari yoyote ambayo ni sahihi kutoka kwa Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- hana budi kuikubali na kuusadiki ujumbe uliobebwa na hadithi hiyo na huo ndio ukamilifu wa "Shahaadatu Anna Muhammadan Rasuulu-llahi" (kukiri kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Allah) nayo ni:

Kuyaamini yote aliyokuja nayo mjumbe huyo na kuyasadikisha yote aliyoyaelezea kutoka kwa mola wake hata kama akili zetu duni hazikubali, na kadhalika kumtii Mtukufu huyo kwa kutenda mema aliyoyaamrisha na kuyaacha mabaya aliyoyakataza.

JARIBIO LA KWANZA LA KUPOTOSHA HADITHI HII

Jaribio lake la kwanza ndugu Juma amelielekeza katika Sanadi ya hadithi hii, na akazielekeza tuhuma zake kwa mpokezi "QAIS BIN ABI HAAZIM".
Amesema Juma al-Mzrui katika kitabu chake "Hoja zenye nguvu" ukurasa wa 253:
"Hadithi hii imepokewa kupitia kwa Qais naye ni QAIS BIN ABI HAAZIM. Na mtu huyu wanavyuoni wengi wamemdhaifisha (wamesema kwamba ni dhaifu)".
Mwisho wa kunukuu.

MAJIBU YETU

Katika itikadi ya makhawaarij (maibadhi) ni kwamba mtu akifanya dhambi kubwa kama vile kusema uongo, basi anakua kafiri na huko akhera ataingia motoni milele na hatoki katu. Sasa ajabu ni maibadhi hawa wa zama hizi kwa nini wanasema uongo?!!

Na ushahidi juu ya uongo wao ni huu ufuatao:
Ndugu Juma anadai kwamba Qais ni ''DHAIFU'' na wanavyuoni wengi wamemdhaifisha!!!
Maneno haya ni uongo na ukweli ni kwamba Qais ni ''THIQA'' (ni mtu muadilifu mwenye hifdhi nzuri) kwa mujibu wa kauli za maulamaa wa hadithi.
1-Amesema Imamu Yahya bin Mai'n : "THIQA".

2-Amesema Imamu Abu Daud: "Mtu mwenye sanadi nzuri kuliko Taabi'ina wote (taabi'ina ni wafuasi wa maswahaba) ni Qais bin Abi Haazim.

3-Amesema Ya'qub bin Abi Shaibah:
"Alikuwa Qais ni katika Taabi'ina wa zamani mno…na yeye ni mwenye ufanisi katika kupokea riwaya".

4-Amesema Ismail bin Abi Khalid:
"Alikuwa (Qais) ni mtu madhubuti".

5-Na Imamu Ibn Hibbaana amemtaja miongoni mwa Thiqaat (watu madhubuti katika riwaya).

6-Amesema Imamu al-Dhah'biy :
"Wameafikiana (maulamaa wa hadithi) juu ya kumfanya (Qais) kuwa ni Hoja na mtu YEYOTE ATAKAYEMSEMA VIBAYA BASI AMEJIUDHI MWENYEWE".

7-Na amesema al Hafidh Ibn Hajar:
"Qais bin Abi Haazim al Bajaliy Abu Abdillahi al Kufiy ni THIQA".

Tazama vitabu vifuatavyo:
Taarikhul-Duuriy juzuu ya 2 ukurasa wa 95.
Kitabu Al-Thiqat cha Ibn Hibbaan juzuu ya 5 ukurasa 307.
Tahdhibul-Tahdhibi juzuu ya 4 ukurasa wa 561 -586.
Al-Taq'ribu ukurasa 134-135, tarjama namba 6250.

Mpaka hapa madai ya Juma kwamba Qais ni dhaifu yatakuwa yameporoka.

TUHUMA YAKE YA PILI DHIDI YA QAIS:

Amesema ndugu Juma:
"Anasema Ya'aqub bin Abi Shaiba "QAIS ni katika wafuasi wa maswahaba wa mwanzo ……. na wamesema wanavyuoni wetu wengine wakamtukuza……(na) wengine wakamshambulia na wakasema kuwa ana hadithi (nyingi) MUNAKiR."
Na anasema Ismail bin Abi Khalid, ambaye hadithi hii imepita kwake, kuwa: "QAIS"aliishi mpaka akavuka miaka mia na ziada nyingi juu mpaka akaharibika fahamu na kurukwa na akili".

Na akasema Ibn Al –Madini "kaniambia Yahya bin Said kuwa QAIS BIN ABI HAAZIM hadithi zake ni MUNKAR, kisha akazitaja Yahya hadithi (zake nyingi ambazo ni) MUNKAR"....kwahivyo kutokana na maneno haya hadithi hii haina usahihi wowote". !!!
Mwisho wa kunukuu.Tazama maneno hayo ya bwana Juma katika kitabu chake "Hoja zenye nguvu" ukurasa wa 253-254.

MAJIBU YETU:

Majibu yetu Inshaallah yatakuwa kwa njia mbili:
Njia ya kwanza, ni kuhusu kauli ya Ibn al-Madini kuwa ameambiwa na Yahya bin Said kwamba Qais bin Abi Haazim hadithi zake ni MUNKAR.

Ameijibu tuhuma hii Imamu al-Dhah'biy pale alipoitaja kauli hiyo kwa kusema:
"Kisha (Yahya bin Said) akazitaja hadithi ambazo ameziona kuwa ni munkar, lakini hakufanya kitu, bali hadithi hizo zimethibiti, na wala haishangazi kupwekeka nazo (kuwa amezipokea peke yake) kwa sababu ya upana wa aliyoyapokea, na miongoni mwa hadithi hizo ni (ile inayotaja habari za) Mbwa wa Hauab''.
Tazama mizanul itidaal juzuu ya 3 ukurasa 392-393.

Maana ya maneno haya ya Imamu al-Dhah'biy ni kwamba si sahihi kusema kwamba Qais hadithi zake ni MUNKAR au hadithi zake nyingi ni MANAKIR kwa sababu ya kupwekeka kwake katika kupokea baadhi ya hadithi bila ya kushirikiana katika mapokezi hayo na watu wengine, kwa sababu Qais alikuwa na hifdhi pana na riwaya nyingi, na baada ya kuzifuatilia hadithi zake imegundulika kwamba ni hadithi sahihi na miongoni mwa hadithi hizo ni ile ambayo Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- alitabiri kwamba baadhi ya wake zake

watabwekewa na mbwa pindi wafikapo mahali paitwapo Hauab na hiyo ni hadithi sahihi.

Maana nyingine ya neno Munkari:
Amesema al-Hafidh Ibn Hajar katika kitabu chake Tah'dhiibul-Tah'dhiibi juzuu ya 4 ukurasa wa 562 akiitafsiri kauli ya Yahya bin Said al Qattwaan:

"ومراد القطان بالمنكر: الفرد المطلق".

''Na makusudio ya al-Qattwaan (aliposema) Munkar: ni kupwekeka mutlaki''.

Maana ya maneno ya Ibn Hajar ni kwamba:
Siyo makusudio ya Imamu al-Qattwaan aliposema "hadithi munkar" kuwa maana yake ni hadithi ya mtu dhaifu aliyepingana na mtu Thiqa kama ilivyozoeleka katika elimu ya "Mustalahul hadithi" bali makusudio ni kupwekeka mpokezi katika mapokezi yake. Na si Imamu al-Qattwaan peke yake aliye litumia neno "MUNKAR" kwa maana ya kupwekeka, bali hata Imamu Ahmad bin Hanbal anakawaida ya kulitumia neno hilo kwa maana ya kupwekeka, na kulitumia neno hili kwa maana hii halileti ile maana ya kujeruhi iliyozoeleka katika elimu ya hadithi.

Amesema Imamu Ibn Hajar katika Had'yu Saar ukurasa wa 453 kuhusu matumizi ya Imamu Ahmad juu ya tamko hili:

"وهذه اللفظة يطلقها الإمام أحمد على من يغرب على أقرانه بالحديث ...".

"Na tamko hili (MUNKAR) analitumia Imamu Ahmad kwa yule ambaye analeta hadithi ngeni kwa watu wa rika lake..".

Bado tunasisitiza kuwa, kuna muhimu mkubwa kwa mtu anayetaka kufanya utafiti wa mambo ya hadithi na riwaya, kusihi kwake na kutokusihi kuwa na utaalamu wa kutosha juu ya istilahi za maulamaa, bila ya hivyo, mtu atapoea na atawapoteza watu.

Njia ya pili:

Kuhusu kauli ya ndugu Juma al-Mazrui dhidi ya mpokezi Qais bin Abi Haazim pale aliposema:

"Na amesema Ismail bin Abi Khalid, ambaye hadithi hii imepita kwake, kuwa: "QAIS'' aliishi mpaka akavuka miaka mia na ziada nyingi juu mpaka akaharibika fahamu na kurukwa na akili".

Tazama katika kitabu chake "Hoja zenye Nguvu" ukurasa wa 254.

MAJIBU YETU

Majibu yetu ni kama ifuatavyo:

Tulishawahi kuijibu tuhuma kama hii wakati ndugu Juma alipomtuhumu nayo Hamad bin Salama na tukasema kwamba:

Mtu akichanganyikiwa mwishoni wa umri wake hazirudishwi riwaya zake zote, bali huangaliwa ni kina nani waliopokea kutoka kwake, na wakati gani wamepokea ?

Je wamepokea kabla ya kuchanganyikiwa au ni baada, rejea ufafanuzi tulioutoa hapo nyuma.

Hivyo basi tunamtaka bwana Juma atuthibitishie kwamba Ismail bin Abi Khalid amepokea kutoka kwa Qais baada ya Qais kuharibikiwa na akili.

Na kama hana ushahidi juu ya hilo basi anyamaze awaache wenye kujua waseme.

Kwa ufupi ni kwamba hadithi hii ni sahihi kwa mujibu wa misingi ya elimu ya hadithi na wala haina shaka yoyote, na bila shaka ndugu yangu msomaji utakuwa umebainikiwa na hila za ndugu Juma juu ya kutaka kuzipotosha hadithi za Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- kwa sababu ya madai yake yaliyo dhaifu tena ya uongo.

JARIBIO LAKE JINGINE

Pia ndugu Juma alifanya jaribio jingine la kutaka kumdhoofisha mpokezi mwingine ambaye ameipokea hadithi hii kutoka kwa Ismail kutoka kwa Qais, naye ni JARIR BIN ABDUL-HAMID BIN QUR'T.

Amesema Juma:
"Na mpokezi mwengine ambaye si madhubuti humu ni:
2) JARIRI BIN ABDILHUMAID BIN QART AL-RAZI naye japo kuwa wanavyuoni wengine wamemkubali lakini pia kuna tofauti juu yake.
Anasema Al-imamu Ibn Hajar Al-asqalaani kuwa "ikiwa riwaya ya Al-shadhkun ni sahihi basi Jarir alikuwa akighushi."
Na amesema Al-imamu Ahmad bin Hanbal kuwa "hakuwa mtu mwenye hifdhi nzuri ."
Na akasema Al-bayhakii kuwa "ilinasibishwa kwake kuwa alikuwa na hifadhi mbaya mwishoni mwa umri wake." Kwa hivyo hadithi hii ni dhaifu pia".
Mwisho wa kunukuu.
Tazama kitabu chake "Hoja zenye nguvu" ukurasa wa 255.

MAJIBU YETU

Majibu yetu ni kwa njia mbili:

Njia ya kwanza: ameliandika jina la mwanachuoni huyu kimakosa, sawa sawa ni: ABDUL-HAMID BIN QUR'T na siyo ABDULHUMAID BIN QART.
Lengo letu hapa ni kumuweka sawa tu, na sio kutaka kumdhalilisha ndugu yetu Juma kwa kumtia makosa kama haya, kwa sababu nimeshindwa kumvumilia maana makosa ya aina hii yamekua mengi mno tena yanakaririka, hivyo nimeona ni vyema kumtanabahisha ili atanabahi, na pia wengine wasiingie kwenye makosa aina hii.
Na watu wengi wanaoingia katika makosa haya na mfano wake utawakuta ni wale ambao wamevivamia vitabu vya elimu bila ya kuichukua kutoka kwa maulamaa waliobobea katika fani hii, ndiyo

ukamuona mtu analitaja la jina mtu vile anavyodhania yeye kwenye akili yake na si kama inavyotakiwa.

Mfano wa makosa mengine aliyoyakwaa ndugu Juma na wala hakuyaweka katika list yake ya marekebisho ni:
IBN MUIN. ukurasa wa 65 na 69 na 71, sahihi ni IBN MAI'N.
AL-AQIL. ukarasa wa 67 na sahihi ni AL-U'QAILIY.
AL-DAURI. ukurasa wa 69 Sahihi ni AL-DUURIY
GHANDAR.ukurasa wa 121 sahihi ni GHUNDAR.

Na makosa mengineyo mengi ambayo hatukuyataja, kwa sababu lengo hapa ni kutoa mfano tu na siyo kumpatiliza.
Ama kuhusu kauli ya Ibn Hajar dhidi ya Jarir, bado si hoja ya kumjeruhi Jarir na kuifanya hadithi yake kuwa ni dhaifu, kwa sababu zifuatazo;

i) Amesema Ibn Hajar; "ikiwa riwaya ya Al-Shaadhakun ni sahihi..." na wala Ibn Hajar hakusema kwamba riwaya ya Al Shaadhakun ni sahihi, kwa sababu amesema: "ikiwa" na neno hilo huonyesha hali ya kutokuwa na hakika juu ya jambo, hivyo haliwi ni hoja ya kuthibitisha madai, kwa mfano mtu akisema; "ikiwa yanayosemwa ni kweli, basi Aliy ni mtu muovu" bado maneno haya hayajakuwa ni hoja ya kumtuhumu Aliy.

Hivyo kauli ya Ibn Hajar aliposema "ikiwa riwaya ya Al Shaadhakun ni sahihi basi jarir alikuwa akighushi" si hoja ya kumtuhumu Jarir kwa tuhuma ya kughushi.

ii) Na baada ya kufanya utafiti wa kielimu imetubainikia kuwa riwaya ya Al- Shaadhakun haikusihi kwa sababu hizi zifuatazo:

a) Wanachuoni wa hadithi wamemjeruhi al-Shaadhakuni:
Amesema Imamu al-Bukhari kuhusu al-Shaadhakuni kuwa ni:

"Mtu wa kufikiriwa" (dhaifu).
Amesema Abu Hatim: al-Shaadhakuni ni "Mat'ruuk" (ni mtu wa kuwachwa).
Amesema Ibn Mai'n kuwa al-Shaadhakuni ni "Muongo".

Amesema Imamu al Nasai: Si mtu madhubuti.

Na amesema Imamu al Dhah'biy:
Inasemekana kwamba "Alikuwa (al-Shaadhakuni) ANAKUNYWA POMBE"!!!
Rejea kitabu Mizanul I'tidaal juzuu ya 2 ukurasa 205.

Pia isitoshe ndugu Juma katika kitabu chake "Hoja zenye Nguvu" ukurasa 123 amenukuu maneno ya wanavyuoni kuhusu al-Shaadhakuni akasema Juma akimnukuu Imamu Is'haq Ibn Mansour al-Kawsajiy (Juma amemuita Kuusajiy na hilo ni kosa):
"...sijapata kuona mtu bingwa wa uwongo kuliko watu wawili: SULAIMAN AL-SHADHAKUNI na MUHAMMAD BIN HUMAID".!!!
Mwisho wa kunukuu.
Tazama katika ukurasa wa 122-123 katika kitabu chake "Hoja zenye Nguvu".
Sasa vipi Juma ndugu yangu itasihi riwaya ya mtu huyo ambaye ni mlevi, bingwa la uongo?!

Njia ya pili:
Ni kuhusu kauli ya Imamu Ahmad aliposema:
"Hakuwa (Jarir) ni mtu mwenye fahamu nzuri".

Majibu yetu:
Maneno haya hayaleti maana kwamba Jarir ni dhaifu na riwaya zake pia ni dhaifu bali maulamaa huwa wanayaleta maneno haya kwa lengo la kutaka kubainisha kwamba iwapo itatokea kutofautiana mpokezi mwenye sifa hiyo na mpokezi mwengine ambaye hana sifa

hiyo basi kauli itakayo tangulizwa ni ya yule mwenye ufahamu mzuri (Dhakiyun).

Na tumesema hivi kwa sababu zifuatazo:
a) Hakuna hata mwanachuoni mmoja wa hadithi ambaye ameirudisha hadithi ya Jarir, kwa sababu ya kuwa hana fahamu nzuri.

b) Bali maulamaa wengi wamemsifia Jarir kuwa ni mtu madhubuti, kwa mfano;
Amesema Imamu Abu Haatim:
Jarir ni Hoja (katika riwaya zake).

Amesema Imamu al-Nasai:
Jarir ni Thiqa (Muadilifu mwenye hif'dhi nzuri).

Amesema Imamu al-Ijliy:
Jarir ni mtu wa (sehemu za) Kufa yeye ni Thiqa (Muadilifu mwenye hifdhi nzuri).

Amesema Ibn Hajar:
Jarir ni Thiqa (muadilifu mwenye hifdhi nzuri).
Kuhusu maelezo haya tazama vitabu vifuatavyo;
Taarikh al-Duuriy juzuu ya 2 ukurasa 81.
Taarikh al Thiqaat ukurasa wa 96.
Al-Jar'hu wat-Ta'adiil juzuu ya 2 ukurasa 505.
Mizaanul-I'tidaal juzuu 1 ukurasa 394-395.
Na al-Taqriibu ukurasa 132.

c) Na kauli ya Imamu Ahmad haileti maana kwamba Jarir alikuwa chizi (mwenda wazimu), bali maana yake ni kwamba alikuwa hawezi kusimulia kupitia hifdhi yake ni lazima asimulie kwa kuangalia kwenye kitabu chake, na jambo hilo linakubalika.
Amesema Imamu Abul-Walid:

“Niliwahi kukaa na Jarir wakati niko al-Rayyi akaandika kutoka kwangu hadithi mbili kisha nikamwambia nami nisimulie (hadithi ulizozipokea) akasema Jarir: mimi sihifadhi (kwa moyo) na vitabu vyangu havipo, lakini natarajia vitaletwa, na mimi nimeziandika (hadithi zangu) humo.

Mara siku moja akaanza kutaja hadithi, nikamwambia; nadhani vitabu vyako vimekuja?
Akasema ndiyo.
Nikamwambia Abu Daud; rafiki yetu vitabu vyake vimekuja kutoka Kufa twende tukavitazame, tukamuendea tukavitazama mimi na Abu Daud”.
Tazama kisa hicho katika Mizanul-I'tidaal juzuu 1 ukurasa wa 395.

Kwa hiyo Jarir alikuwa na kasoro hiyo ambayo si ya kumfanya mpokezi kukataliwa riwaya zake.
Ama kauli ya ndugu Juma aliposema kuhusu Jarir:

“akasema Al-Bayhakii kuwa ilinasibishwa kwake alikuwa na hifadhi mbaya mwishoni mwa umri wake” kwahivyo hadithi hii ni dhaifu pia”.
Mwisho wa kunukuu.

Jawabu kuhusu maneno haya ni kama ile iliyotangulia kuhusu wale walio changanyikiwa mwishoni mwa umri wao.
Ama kudai hadithi hii pia nayo ni dhaifu si maneno ya kweli na wala hayakujengeka juu ya misingi ya kielimu.

UFAHAMU MBAYA JUU YA HADITHI HII

Katika kuyatilia nguvu madai yake ya kwamba hadithi hii ni dhaifu ndugu Juma akaleta maneno ya ajabu kwa sababu ya ufahamu

wake mbaya juu ya hadithi hii, lakini kitambo alishasema mshairi (al-Mutanabbiy):

وكمْ مِنْ عائِبٍ قولاً صَحيحاً ... وَآفَتُهُ منَ الفَهمِ السَّقيمِ

"Ni wangapi wenye kuyatia kasoro maneno yaliyo sahihi** lakini msiba wake ni (kwa sababu ya) ufahamu mbaya"?!

Na ushahidi juu ya ufahamu mbaya wa ndugu Juma ni pale aliposema:

"La pili iwe makusudio ya kumuona Mwenyezi Mungu kama jua ni kuwa kama tunavyoliona jua kwa uwazi basi vivyo hivyo ndivyo tutakavyomuona Mwenyezi Mungu.

Lakini kama ni hivi basi mfano huu uliomo katika hadithi hii si sahihi kwa sababu hadithi inasema kuwa watu watamuona Mwenyezi Mungu kama wanavyoliona jua mchana wakati wa jua kali.

Sasa suala ni kuwa je nani anaweza akalitazama jua wakati wa mchana wa jua kali ikiwa hakuna mawingu yaliyoziba, hebu kila mmoja na ajaribu kulitazama jua saa sita mchana alau sekunde mbili. Kama hakuna, basi mfano huu si sahihi, na kama mfano huu si sahihi basi haya maneno si maneno ya Mtume (S.A.W.)."

Mwisho wa kunukuu.

Tazama kitabu chake "Hoja zenye nguvu"ukurasa wa 251.

MAJIBU YETU

Kuyaelewa maneno ya Mtume bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- inatakiwa tawfiq kutoka kwa Allah, na wala si jambo dogo, na watu wengi hawakuwafikishwa katika jambo hili la kheri kwa sababu ya nia zao mbaya. Na miongoni mwa hao ni ndugu Juma Al-Mazr'rui, naye pia haukuelewa makusudio ya maneno ya bwana Mtume Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam- katika mfano huu.

Na kuelewa semi, mifano, na methali za kiarabu ni miongoni mwa fani muhimu za lugha ya kiarabu, na kama mtu hautabarikiwa kufahamu mambo hayo, kuna hatari kubwa ya kutumbukia katika balaa la kukadhibisha maandiko kwa sababu ya uelewa mbaya.
Mara nyingi huwa mifano ndiyo inayofafanua mambo kwa uzuri zaidi na kuyaweka wazi kuliko maneno ambayo hayana mifano.
Ndiyo maana Qur'an kadhalika maneno ya bwana Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- yamejaa mifano mingi, na lengo la mifano hiyo ni kuwafanya watu wawe ni wenye kufikiria mambo kwa undani zaidi na wayapime kwa akili zao ili waweze kuufikia ukweli.

Lakini pamoja na hayo, mara nyingine hawaifahamu mifano hiyo ila wale wenye elimu za kutosha, amesema Allah:

{وَتِلْكَ الْأَمْثَالُ نَضْرِبُهَا لِلنَّاسِ وَمَا يَعْقِلُهَا إِلَّا الْعَالِمُونَ }العنكبوت43}

"Na hiyo ni mifano tunawapigia watu, na hawaifahamu ila wenye ilimu".

Suratul-A'nkabut (29) aya ya 43.

Ndugu Juma huenda -kwa sababu na yeye si katika wenye elimu, au ni kwa sababu amekusudia kupotosha- na yeye pia hakuufahamu mfano huu ndiyo akafikia kusema:

"Lakini kama ni hivi basi mfano huu uliomo katika hadithi hii si sahihi kwa sababu hadithi inasema kuwa watu watamuona Mwenyezi Mungu kama wanavyoliona jua mchana wakati wa jua kali".

Sisi tunasema lau kwamba ndugu Juma angeutazama mfano huu kwa jicho la kutaka kujua ukweli angegundua kwamba makusudio ya Mtume –swalla llahu alayhi wasallam- katika mfano huu ni tofauti na alivyofahamu yeye.

Kwa sababu makusudio ya mfano huu ni kutaka kufahamisha kwamba:

Kama vile ambavyo hakuna msongamano wala kiminyano katika kulitazama jua la mchana ambalo halikufunikwa na mawingu, basi mjue ni hivyo hivyo kwamba hakuna kiminyano wala msongamano katika kumuona mola wenu muumba huko katika Jannah (peponi).

Kwa ufupi ni kwamba:

Hakuna tabu yoyote mtakayoipata katika kumuona Allah -Tabaaraka wata'alaa- kwa namna atakavyo jihidhirisha kwenu -Sub'haanahu wata'alaa- kama vile ambavyo hamsongamani katika kulitazama jua au mwezi mpevu.

Ndiyo maana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- akawauliza maswahaba zake:

Je mnasongamana katika kuliona jua katika mchana ambao hakuna mawingu?

Maswahaba wakajibu:

Hapana !

Bali kila mwenye akili timamu akiulizwa swali kama hilo hatokua na jawabu zaidi ya kusema hapana.

Na wala Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- hakuuliza je mnataabika au mnapata taabu katika kulitazama jua katika mchana wa jua kali kwa sababu ya mwangaza wake?

Kama alivyofahamu Juma, na kama angeliuliza hivyo bila shaka jawabu lingekuwa "NDIYO " tunapata taabu. Kwa sababu hakuna anayeweza kulitazama jua kali la mchana ambao hakuna mawingu.

Kwa sababu mfano huo hauko baina ya kulitazama jua na kumtaza Allah -Sub'haanah- wala hauko katika kuweza kulitazama jua na kutokuweza kama alivyofahamu Juma, mpaka akafikia kusema: "hebu kila mmoja ajaribu kulitazama jua saa sita mchana alau sekunde mbili"!!!

Kwa ufupi ni kwamba ndugu Juma hakufahamu kitu kinachoitwa: "WAJ'HUS-SHABAHI" njia ya kufanana baina ya "MUSHABBAHUN" (chenye kufananizwa) na "MUSHABBAHUN BIHI" (chenye kufananiziwa) na huo ni mlango muhimu mno katika elimu ya "BALAGHA"(RHETORIC),

Na lau kama mtu hataufahamu vizuri mlango huu basi anaweza kuyakadhibisha maneno ya haki yasiyo na utata wowote kama alivyofanya ndugu yetu Juma al-Mazrui.

Pia balaa hili limempata ndugu Juma kutokana na uelewa wake finyu wa lugha ya kiarabu, ndiyo maana hakuweza kuleta tafsiri sahihi ya maneno haya, sasa hebu tuyaangalie maneno haya je maana yake ni kupata taabu kama alivyo tafsiri Juma au ni kusongamana kama tunavyotafsiri sisi?

Hebu tuyatazame maneno haya mawili yaliyotumika katika hadithi kupitia kamusi za lugha ya kiarabu pamoja na kauli za maulamaa wakubwa:

1-"لا تضامون" (Laa tudhaammuuna).

2- "لا تضارون" (Laa tudhaarruuna).

Yeye akatafsiri kuwa maana yake ni "hamupati tabu"na hali yakuwa maana yake ni "hamsongamani/hamtodhuriana" na kwa ushahidi zaidi angalia kauli hizo za maulamaa juu ya maana ya maneno haya:

Maana ya neno la kwanza (Laa tudhaammuuna):

قال الإمام ابن الأثير:

"معناه: لا ينضم بعضكم إلى بعض وتزدحمون وقت النظر".

Amesema Imamu Ibnul-Athir:

"Maana yake:hawatakusanyika watu pamoja wakasongamana wakati wa kutazama".

Tazam kitabu chake;al-Nihaya fiy Gharibil Hadith ukurasa wa 555. Na maudhui ya kitabu hiki kuyatafsiri maneno yote mageni na magumu ya lugha ya kiarabu ambayo yamo katika hadithi na kauli za maswahaba.

قال الإمام ابن منظور:

" أي لا ينضم بعضكم إلى بعض فيقول واحد لآخر أرنيه كما تفعلون عند النظرإلى الهلال".

لسان العرب 63/9 مادة ضمم.

Amesema Imamu Ibn Mandhuur:

“Maana yake: hawatokusanyika ikafikia kusema mmoja kumwambia mwingine nionyeshe, kama vile mnavyofanya wakati wakutazama mwezi mwandamo”.
Tazama kitabu chake Lisaanul-Arabi juzuu ya 9 ukurasa wa 63.

قال الحافظ ابن حجر:
((لا تضامون فى رؤيته)) معناه: لا تجتمعون لرؤيته فى جهة ...".
فتح الباري 526/13.

Amesema al-Hafidh Ibn Hajar:
“ ((Laa tudhaammuuna fiy ru’uyatihi)) maana yake hamtakusanyikana upande mmoja kwa ajili ya kumtazama”.
Tazama kitabu chake Fat’hul-Baari juzuu ya 13 ukurasa wa 526.

Ama kuhusu neno la pili ((Laa tudhaarruuna):

((لاتضارون)):
قال ابن الأثير:
"لا تتخالفون ولا تتجادلون فى صحة النظر إليه لوضوحه وظهوره".
النهاية فى غريب الحديث ص542 مادة ضرر.

Amesema Ibnul Athir:
“Hamtatafautiana wala hamtajadiliana kuhusu kusihi kumtazama kutokana na uwazi wake na kudhihiri kwake”.
Tazama kitabu al-Nihaaya fiy Gharibil-Hadithi ukurasa wa 542.

قال الإمام النووي:
"هل تضارون غيركم فى حالة الرؤية بزحمة أو مخالفة فى الرؤية أو غيرها لخفائه كما تفعلون أول ليلة من الشهر"؟
المنهاج شرح صحيح مسلم بن الحجاج 27/3.

Amesema Imamu Al-Nawawiy:
“(Maana yake) je mnawadhuru wengine katika hali ya kuutazama (mwezi mpevu) kwa sababu ya msongamano au kutofautiana katika kuuona au kwa jambo jingine kwa sababu ya kujificha kwake kama mnavyo fanya usiku wa mwanzo wa mwezi”?
Tazama kitabu chake al-Min’haaj, juzuu ya 3 ukurasa wa 27.

قال الإمام ابن منظور:
"أي لا يضر بعضكم بعضا...". لسان العرب 34/9.

Amesema Imamu Ibn Mandhuur:

"Maana yake: hamtodhuriana wenyewe kwa wenyewe".

Tazama katika kitabu chake Lisaanul-Arabi juzuu ya 9 ukurasa wa 34.

Bila shaka ndugu msomaji umeelewa ni kitu gani ambacho kimemsibu ndugu Juma mpaka akafikia kuyakadhibisha na kuyabatilisha maneno ya bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam-.

Mimi ninasema kwamba hakuna kitu kingine zaidi ya moja mambo mawili:

1-Ufahamu mbaya wa lugha ya kiarabu,au:

2-Anafanya makusudi ili kutimiza malengo yake mabaya ambayo ameyakusudia yeye na washirika wake, ndiyo akafikia kiwango hiki cha kuyatupilia mbali maneno ya bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- kwa urahisi tena kwa kejeli ya hali ya juu.

HADITHI YA PILI

Hadithi hii pia imepokewa kwa njia nyingi mno, lakini kwa kuhofia kurefusha tutazitaja baadhi ya njia hizo:

Njia ya kwanza:

قال الإمام ابن أبي عاصم رحمه الله تعالى:
ثنا عمرو بن عثمان ، ثنا أبي ، عن محمد بن مهاجر ، عن ابن حلبس ، عن أم الدرداء ، أن فضالة بن عبيد ، كان يقول : « اللهم إني أسألك الرضا بعد القضاء ، وبرد العيش بعد الموت ، ولذة النظر في وجهك ، والشوق إلى لقائك من غير ضراء مضرة ولا فتنة مضلة » . وزعم أنها دعوات كان يدعو بها النبي صلى الله عليه وسلم .

Amesema tena Imamu Ibn Abi A'asim: Ametusimulia Amru Ibn Uth'maan, ametusimulia baba yangu kutoka kwa Muhammad bin Muhaajir kutoka kwa IBN HALBAS kutoka kwa Ummu Dar'dai kwamba Fadhaala bin Ubaid alikuwa akisema:

“Ewe mola wangu wa haki kwa hakika mimi ninakuomba kuridhika baada ya hukumu, na ubaridi wa maisha baada ya mauti na ladha ya KUUTAZAMA USO WAKO !! na shauku ya kukutana na wewe pasi na madhara yenye kudhuru wala fitina zenye kupoteza”.
Na akadai kwamba hiyo ni dua ambayo alikuwa akiiomba Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam-.

Njia ya pili:

قال الإمام ابن حبان رحمه الله:
أخبرنا ابن خزيمة ، قال : حدثنا أحمد بن عبدة ، قال : حدثنا حماد بن زيد ، عن عطاء بن السائب ، عن أبيه ، قال : كنا جلوسا في المسجد ، فدخل عمار بن ياسر ، فصلى صلاة خففها ، فمر بنا فقيل له : يا أبا اليقظان ، خففت الصلاة ، قال : أو خفيفة رأيتموها ؟ ... ، وأسألك الرضا بعد القضاء ، وأسألك برد العيش بعد الموت ، وأسألك لذة النظر إلى وجهك ، وأسألك الشوق إلى لقائك ، في غير ضراء مضرة ، ولا فتنة مضلة ... »

Amesema Imamu Ibn Hibban:
Ametusimulia Ibn Khuzaima, amesema ametusimulia Ahmad Ibn Abdah, amesema ametusimulia Hamad Ibn Zaid, kutoka kwa Atwaa Ibn al-Saib kutoka kwa baba yake, amesema: Tulikua ni wenye kukaa msikitini, akaingiaAmmar bin Yaasir akaswali swala nyepesi, kisha akatupita, akaambiwa Ee Aba Yaq’dhani! Umeifanya nyepesi swala, akasema: mmeiona ni nyepesi ? ...akaelezea kisa kisha akasema kwamba aliomba dua hii aliyomsikia Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam-:
“Ewe mola wangu wa haki kwa hakika mimi ninakuomba kuridhika baada ya hukumu, na ubaridi wa maisha baada ya mauti na ladha ya KUUTAZAMA USO WAKO !! na shauku ya kukutana na wewe pasi na madhara yenye kudhuru wala fitina zenye kupoteza”.
Tazama kitabu “Sahihi” cha Ibn Hibbana, hadithi namba 2005.

Njia ya tatu:

قال الإمام ابن أبي عاصم رحمه الله تعالى:
ثنا أبو بكر بن أبي شيبة ، ثنا معاوية بن هشام ، عن شريك ، عن أبي هاشم ، عن أبي مجلز ، عن قيس بن عباد ، عن عمار بن ياسر ، ذكر دعاء سمعه من النبي صلى الله عليه وسلم قال :
« اللهم وأسألك لذة العيش بعد الموت ، ولذة النظر إلى وجهك ، وشوقا إلى لقاك » .

Amesema Imamu Ibn Abi A’asim:

Ametusimulia Abu Bakri bin Abi Shaibah, ametusimulia Muawiya Ibn Hisham, kutoka kwa Sharik, kutoka kwa Abu Hashim, kutoka kwa Abu Mij'laz, kutoka kwa Qais bin Abbad, kutoka kwa Ammar bin Yaasir, ameitaja dua aliyoisikia kutoka kwa Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- amesema:

"Ewe Allaah! Kwa hakika mimi ninakuomba ladha ya maisha baada ya mauti, na ladha ya KUUTAZAMA USO WAKO !! na shauku ya kukutana na wewe".

Tazama kitabu "al-Sunna" cha Imamu Ibn Abi A'asim, hadithi namba 424.

Njia ya nne:

قال الإمام الدارقطني:

157 - حدثنا محمد بن سليمان النعماني ، حدثنا أبو عتبة الحمصي ، حدثنا عثمان بن سعيد ، عن محمد بن مهاجر ، عن ابن حلبس ، عن أم الدرداء ، أن فضالة ، يعني ابن عبيد ، كان يقول : « اللهم إني أسألك الرضا بعد القضاء ، وبرد العيش بعد الموت ، ولذة النظر إلى وجهك ، والشوق إلى لقائك من غير ضراء مضرة ، ولا فتنة مضلة »

كتاب الرؤية 245/1 رقم الحديث 157.

Amesema Imamu al-Daaraqut'niy:

Ametusimulia Muhammad bin Sulaiman al-Nu'umaniy, ametusimulia Abu Ut'ba al-Himsiy, ametusimulia Uth'man bin Said, kutoka kwa Muhammad bin Muhajir, kutoka kwa Ibn Halbasa, kutoka kwa Ummul-Dardaai, kwamba Fadhala bin Ubaid alikua anasema:

"Ewe Allaah! Kwa hakika mimi ninakuomba kuridhika baada ya hukumu, na ubaridi wa maisha baada ya mauti na ladha ya KUUTAZAMA USO WAKO !! na shauku ya kukutana na wewe pasi na madhara yenye kudhuru wala fitina zenye kupoteza".

Tazama kitabu "Al-Ru'uyah" cha Imamu al-Daaraqut'niy, hadithi namba 157.

Njia ya tano:

قال الإمام ابن أبي عاصم رحمه الله تعالى:

حدثنا محمد بن عوف ، ثنا أبو المغيرة ، ثنا أبو بكر بن أبي مريم ، عن ضمرة بن حبيب ، عن أبي الدرداء ، عن زيد بن ثابت ، أن النبي صلى الله عليه وسلم علمه دعاء ، وأمره أن يتعاهده ويتعاهد به

أهله : « اللهم إني أسألك الرضا بعد القضاء ، وبرد العيش بعد الموت ، ولذة النظر في وجهك ، وشوقا إلى لقاك » .

Amesema Imamu Ibn Abi A'sim:

Ametusimulia Muhammad bin Auf, ametusimulia Abul-Mughira, ametsimulia ABU BAKAR IBN ABI MAR'YAM, kutoka kwa Dhamra bin Habib, kutoka kwa Abul-Dar'daai, kutoka kwa Zaid bin Thabit, kwamba Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- amemfundisha yeye dua, na akamuamrisha kuizoea dua hiyo na kuwazoesha watu wake, (nayo ni):

"Ewe Allaah! Kwa hakika mimi ninakuomba kuridhika baada ya hukumu, na ubaridi wa maisha baada ya mauti na ladha ya KUUTAZAMA USO WAKO !! na shauku ya kukutana na wewe".

Hizi tulizo zitaja ni baadhi ya njia za hadithi hii tukufu, na kwa ufupi ni kwamba hadithi hii imepokewa kwa njia tofauti tofauti kutoka kwa Maswahaba watatu:

1) Fadhaalah bin Ubaid, na sanadi yake ni sahihi na haina kasoro yoyote ile, kwa sababu wapokezi wake wote ni safi kabisa, kama tutakavyoona hapo mbele Inshaallah.

2) Ammar bin Yasir, na riwaya yake pia ni sahihi isipokuwa inahitaji maelezo kidogo, kwa sababu ya ATWAA BIN SAIB .

3) Zaid bin Thabit, riwaya hii ina kasoro kidogo kwa sababu ya mmoja kati ya mpokezi wake ambaye ni Abu Bakar bin Abdillahi bin Abi Mar'yam al-Ghassani ana udhaifu katika hif'dhi yake, lakini kwa mujibu wa misingi ya elimu ya uchambuzi wa hadithi, hadithi hii nayo pia inakua sahihi kwa sababu ya hadithi zilizotangulia, na hadithi hii kitaalamu inaitwa: "Hasanun-lighairihi" na inazingatiwa kuwa ni hoja kwa sababu ya "Shawaahid" (hadithi nyingine zenye kuitilia nguvu hadithi hii).

Na kwa bahati nzuri Juma pia anaukubali utaratibu huu wa kitaalamu, lakini ameshindwa kuufanyia kazi kwa sababu ya kulinda na kutetea itikadi yake. Na ushahidi wa kuukubali utaratibu huu ni pale aliposema:

"kitaalamu ikiwa hadithi imepokewa na wapokezi wengine kabisa lakini hadithi ni ile ile, basi huambiwa kuwa hadithi hio ina shahidi.".

Tazama kitabu chake "Hoja zenye Nguvu" ukurasa wa 70.

Na walilllahil-hamdu hadithi hii nayo imepokewa na wapokezi wengine kabisa, lakini hadithi ni ile ile.

Na hadithi hii inapatikana katika vitabu vifuatavyo:

"Kitabu al-Sunna" cha Imamu Ibn Abi A'asim, ukurasa wa 197 hadithi namba 427 kutoka kwa Fadhaala bin Ubaid, na hadithi namba 424 na 425 zote kutoka kwa Ammar bin Yaasir.

Na Sunan al-Nasaai hadithi namba 1305 na 1306 pia zote kutoka kwa Ammar bin Yaasir.

Ufafanuzi kuhusu njia ya kwanza ya hadithi hii kutoka kwa swahaba Fadhaala -Allah amridhie - :

Sanad ya hadithi ya kwanza, ni sahihi na haina kasoro yoyote.

Na pia maelezo yake yako wazi juu ya suala tunalolizungumzia nalo ni suala la kuonekana Allah kwa macho huko akhera.

Katika hadithi hii swahaba mtukufu Fadhaala bin Ubaid -Allah amridhie- alikuwa anatabia ya kuiomba dua hii kila mara, na anatuelezea kwamba bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- alikuwa anatabia ya kuomba dua hiyo, na ndani ya dua hiyo Mtume wetu -swalla llaahu alayhi wasallam- alikuwa akimuomba mola wake amruzuku kumpa starehe kwa kuutazama uso wa (Allah) -Jalla Jalaaluh-.

Na kitendo hicho cha Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- hakihesabiwi kuwa ni kuvuka mipaka katika maombi, kwa kuwa amemuomba Allah kitu kisichowezekana au amemuomba jambo lililo muhali.

Lakini hadithi hii ni kama hadithi nyingine zilizotangulia, haikuwafurahisha watu wa bid'a wote kuanzia Jah'miyyah, Mu'tazila, Khawaariji (Maibadhi) na wengineo.
Ndiyo maana ndugu Juma al-Mazrui akafanya jaribio la kutaka kuibatilisha na kuifanya kuwa ni miongoni mwa hadithi dhaifu na zisizokubalika kama kawaida yake!
Hebu na tulitazame jaribio lake hilo:

JARIBIO LA KWANZA LA UPOTOSHAJI

Jaribio lake la kwanza kuhusu hadithi hii amelielekeza kwenye njia ya kwanza ya hadithi hii, ambayo ni hadithi iliyopokelewa kutoka kwa Fadhaala bin Ubaid –Radhiyallahu An'hu-.
Amesema ndugu Juma katika kitabu chake "Hoja zenye Nguvu" ukurasa wa 194:
"Jawabu juu ya riwaya hii ni kuwa hii ni riwaya dhaifu kwa sababu ya ABU HALBAS ni "راو مجهول" mpokezi asiyejulikana. Tazama TAQRIB ukurasa wa 634 tarjama no. 8062. Na hukumu ya riwaya yenye mpokezi asiyejulikana huwa ni dhaifu".
Mwisho wa kunukuu.

MAJIBU YETU

Majibu yetu juu ya uongo huu ni kama ifuatavyo:
Kwanza kabisa napenda kumuusia ndugu yangu Juma al-Mazrui kwamba aache jazba na kasumba pale anapokuwa anazungumzia masuala ya kielimu, hasa hasa masuala ya elimu hii ya hadithi.
Anatakiwa awe makini, mtulivu, atulize bongo lake na asiwe na kasumba ili kuyahakiki mambo kitaalamu zaidi badala ya kutumia ubabe katika kuzihukumu hadithi zilizothibiti kutoka kwa Mtume Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam-, kwa sababu suala la kuyabatilisha mafundisho aliyoyafundisha bwana Mtume -swalla llaahu

alayhi wasallam- bila kutumia hoja za kielimu ni jambo la hatari mno kwa imani za watu.

Mtu anayefahamu uzito wa jambo hili na akawa mcha Mungu hawezi kukubali kujiingiza kwenye laana hiyo!

Hivyo ndugu yetu Juma anatakikana atahadhari, na kama nasaha zetu hizi zikimfikia, basi amtake msamaha mola wake na awabainishie watu ukweli alioupotosha, kwa usalama ya dini yake na imani za watu wengine, na pia autazame mustaqbali wake huko akhera.

Na lau kama ndugu yangu Juma angetulia akaanza kumchambua mpokezi mmoja baada ya mwingine: kwa kumtazama mpokezi huyo anapokea kutoka kwa nani na nani (masheikh zake)? Na kina nani wanapokea kutoka kwake (wanafunzi wake)? Na akazikusanya riwaya mahali pamoja kwa umakini kisha akazioanisha.

Na kisha akarekebisha baadhi ya makosa yaliyomo katika baadhi ya chapa za vitabu kwa kurejea katika vitabu vya asili badala ya kutoshelezeka na vitabu ambavyo watunzi wake wenyewe wamenakili. Lau kama angeufuata utaratibu huo basi bila shaka angegundua kuwa mtu huyu aliyemjeruhi na akaidhoofisha hadithi hii kwa sababu yake siye huyo mpokezi wa hadithi hii, angegundua kwamba mpokezi huyo haitwi ABU HALBAS bali mpokezi wa hadithi hii anaitwa IBNU HALBAS !!!

Katika kitabu "Haadil Ar'waah" cha Ibnul Qayyim hasa hasa hizi chapa za kibiashara wamemtaja kwa jina la "ABU HALBAS" na hali ya kuwa si sahihi, kwa sababu tutakazozitaja, kwahivyo bwana Juma alipoona jina la ABU HALBAS mbio akakimbilia kwenye kitabu AL-TAQRIB cha Ibn Hajar na kuanza kutoa hukumu aliyoikuta huko bila ya kuhakiki usahihi wa jambo lenyewe, na makosa haya wanayafanya watu wengi mno hasa wale wanaofuata matamanio ya nafsi zao, hawataki kuyahakiki mambo wakidhani kuwa watu wamelala, kumbe hapana! Ukisema uongo usiku, alfajiri kweupe utaambiwa usiku umesema uongo, basi tahadhari.

Kwahivyo sisi tunasema kwamba huyu mpokezi si "ABU HALBAS" bali ni "IBNU HALBAS jina lake kamili ni : YUNUS BIN MAISARAH" naye ni mpokezi "THIQATUN, A'ABID" (muadilifu mwenye hifdhi nzuri tena mcha Mungu) na tunasema hivyo kwa sababu hizi zifuatazo:

Sababu ya kwanza:

Ukivirejea vitabu vyote vya maulamaa wakubwa waliomtangulia Ibnul Qayyim utakuta kwamba mpokezi anayepokea hadithi hii kutoka kwa: IBNU HALBAS aliyefariki (132H) ni: MUHAMMAD BIN MUHAAJIR aliyefariki mwaka (170 H), kama ilivyo katika sanad hii.

Na yeye IBNU HALBAS ambaye amefariki mwaka (132H) sheikh wake ni:

UMMU AL-DAR'DAI AL-SUGH'RAA aliyefariki mwaka (81 H).

Na kwa ushahidi zaidi wa haya tuliyoyaeleza rejea vitabu hivi vifuatavyo:

Al-Sunna cha Imamu Ibn Abi A'asim ukurasa wa 197 hadithi namba 427, chapa ya mwaka 1319 H, al-Maktabul-Islami Beirut.

"Kitaabur-Ru'yat" cha Imamu Al-Daaraqut'niyu, ukurasa wa 158 chapa ya Maktabatul Qur'an-Cairo.

"Sharhu Usuuli I'tiqaadi Ahli Sunna" cha Imamu Al-Laalakai, juzuu ya 3 ukurasa 491 chapa ya mwaka 1402 H Daaru al-Taiba – Riyadh.

Sababu ya pili:

Ukivirejea vitabu vya tarjama za wapokezi, kamavile; Tah'dhibul-Tah'dhibi cha Ibn Hajar juzuu ya 6 ukurasa wa 282-283, ukiitazama tarjama ya Muhammad bin Muhaajir utakuta miongoni mwa masheikh wake ni IBN HALBAS ambaye jina lake ni YUNUS BIN MAISARAH, na si Abu Halbas.

Sababu ya tatu:

Pia ukirejea tarjama yaUmmul Dar'dai al Sugh'raa utakuta kwamba miongoni mwa wapokezi (wanafunzi) waliopokea kutoka kwake ni Yunus bin Maisarah ambaye ndiye huyo IBNU HALBAS.

Kwa faidi zaidi hebu tazama kitabu "Tah'dhiibu al-Tah'dhiibi" cha Ibn Hajar juzuu ya 6 ukurasa 625.

Sababu ya nne:

Huyo ABU HALBAS anayemsema ndugu Juma hakuwahi kupokea zaidi ya hadithi moja tu nayo ni ile iliyomo katika Sunan Ibn Maajah na mwanafunzi wake katika sanad hiyo ni Baqiyya bin al Waliid, na wala Baqiyya hajaipokea hadithi hii, na kwa sababu hiyo hakuna mwanachuoni yeyote wa hadithi aliyetaja katika kitabu chake hadithi hii kupitia kwake.

Na halikadhalika huyo ABU HALBAS hana sheikh mwingine zaidi ya Khulaid bin Abi Khulaid.

Na kwa ushahidi zaidi itazame riwaya hiyo kwenye Sunan Ibn Maajah hadithi namba 2705, pia tazama kitabu "TahdhiibuL-Tah'dhibi" cha Ibn Hajar juzuu ya 6 ukurasa wa 340.

Pia nataka ufahamu kwamba ABU HALBAS hajawahi kupokea hadithi kutoka kwa Ummul-Dar'dai hata siku moja, bali hakuwahi kumdiriki.

Na hilo ni jambo ambalo linazidi kutupa ushahidi wa kwamba kauli iliyo sahihi ni kuwa mpokezi huyo ni IBNU HALBAS na si ABU HALBAS.

Kwa mujibu wa data hizi za kielimu tulizozitoa yanakuwa madai ya ndugu Juma aliposema: "kuwa hadithi hii ni dhaifu kwa sababu ya kuwa mpokezi wake ni ABU HALBAS" ni madai dhaifu mno, ambayo hayakusimama juu ya utafiti thabiti wa kielimu, kwahiyo yanaporomoka kichwa chini miguu juu !

Na sisi tunamwambia ndugu Juma arejee vizuri na ayahakiki mambo kwa utulivu na umakini wa hali ya juu ndipo atagundua kuwa mpokezi huyo si ABU HALBAS kama alivyonukuu yeye bila ya kufanya uhakiki wa mambo kisha akaanza kutoa hukumu.

Usahihi ni kuwa mpokezi huyo ni IBNU HALBAS YUNUS IBNU MAISARAH na yeye ni mtu madhubuti kama tulivyotoa maelezo hapo nyuma. Na haya ndiyo madhara ya kuyavamia mambo bila ya elimu, kujiona unajua katika mambo ambayo hujaipata taaluma yake kutoka kwa watu waliobobea katika fani hiyo.

JARIBIO LAKE LA PILI

Jaribio lake la pili, amelifanya kwenye njia ya pili ya hadithi iliyopokelewa kutoka kwa swahaba Ammar bin Yasir.

Na jaribio hilo amelijenga juu ya madai makuu mawili dhidi ya mpokezi ATWAA BIN AL-SAIB:

Madai ya kwanza:

Amedai kwamba: ATWAA BIN AL-SAIB alichanganyikiwa sana, kwa hivyo wapokezi wote ambao wamepokea kutoka kwake baada ya kuchanganyikiwa hadithi zao si sahihi, isipokuwa Shuuba na Sufyaan al-Thawriy tu.

Na hapa ninamnukuu, amesema Juma:

"Na kwahivyo ikiwa wengine wanasema kuwa wote wamepokea hadithi kutoka kwa ATAA baada ya kuchanganyikiwa isipokuwa watu wawili Shuuba na Al-thauri na wengine wanasema HAMAD kapokea hadithi kutoka kwake kabla ya kuchanganyikiwa, basi jawabu ni kuwa haijulikani wakati gani HAMAD kapokea hadithi kutoka kwa ATAA. Na hukumu ya hadithi kama hii huwa ni yenye kuwachwa."

Mwisho wa kunukuu.Tazama kitabu chake "Hoja zenye Nguvu" ukurasa wa 192.

MAJIBU YETU

Majibu yetu dhidi ya madai yake haya ya uwongo ni kama yafuatavyo:

Kwanza, ni kuhusu msimamo wa maulamaa juu ya riwaya za Zaid kutoka kwa ATAA BIN AL-SAIB:

قال يحيى بن سعيد:

"سمع حماد بن زيد من عطاء بن السائب قبل أن يتغيّر"

Amesema Imamu Yahya bin Said:

"Hamad bin Zaid amesikia kutoka kwa ATAA kabla ya (ATAA) kubadilika."

قال الإمام البخاري:

"قال علي سماع خالد بن عبدالله من عطاء بن السائب بآخره, وسماع حماد بن زيد منه صحيح"

Amesema Imamu Al-Bukhari:

"Amesema Aliy kusikia kwa Khalid bin Abdillahi kutoka kwa ATWAA ni mwishoni mwake (baada ya kuchanganyikiwa), na kusikia kwa Hamad bin Zaid kutoka kwa ATWAA ni sahihi".

قال الإمام النسائي:

"ثقة في حديثه القديم لكنه تغير, ورواية شعبة والثوري وحماد بن زيد عنه جيدة".

Amesema Imamu Al-Nasai:

"(Hamad bin Zaid) ni Thiqa lakini alibadilika, riwaya za Shuuba, Al-Thauri, na Hamad bin Zaid ni safi".

وقال الحافظ ابن حجر:

"فيحصل لنا من مجموع كلامهم أن سفيان الثوري وشعبة وزهير أو زائدة وحماد وأيوب عنه صحيح ..

Amesema Al-Hafidh Ibn Hajar:

"Tunapata kwa mkusanyiko wa maneno yao (wanavyoni) kwamba Sufyaan Al-Thauri, Shuuba, Zuhair au Zaaida, na HAMAD BIN ZAID na Ayoub kutoka kwa ATAA ni sahihi.......".

Tazama kauli zote hizo za maulamaa katika vitabu vifuatavyo:

Mizaanul-I'tidaal juzuu ya 3 ukurasa 71.

Tah'dhibul-Tah'dhib, juzuu ya 4 ukurasa wa 132-133.

Mpaka hapo itakua imekubainikia ndugu yangu msomaji kwamba, madai ya Juma hayana ukweli wowote, na ukweli ni kwamba; Hammad Ibn Zaid ni miongoni mwa waliopokea hadithi kutoka kwa Ataa, kabla Ataa hajachanganyikiwa.

JARIBIO LAKE LA TATU

Pia amejaribu kuiangusha hadithi hii kwa kuleta madai mengine dhidi ya ATWAA, kwa kusema:

"Bali ATWAA huyu ni dhaifu hata kama hakuchanganyikiwa kwa mujibu wa maneno ya Ibn Muin kwamba "Laith bin Abi Sulaim ni dhaifu kama ATWAA BIN SAIB."

Tazama katika kitabu chake "Hoja zenye Nguvu" ukurasa wa 192.

MAJIBU YETU

Majibu yetu dhidi ya madai haya ni kama yafuatavyo:

Madai yake haya hayana ukweli wowote, na wala hayana ith'bati za kielimu, na uthibitisho wa hilo ni hizi kauli za maulamaa wa hadithi:

وقال أحمد بن حنبل: عطاء بن السائب ثقة، ثقة، رجل صالح، ومن سمع منه قديما كان صحيحا، وكان يختم كل ليلة.

ميزان الإعتدال 71/3. الجرح والتعديل 334/6

Amesema Imamu Ahmad bin Hanbal:

"Atwaa bin Saib ni Thiqa, Thiqa, ni mtu mwema, waliosikia hadthi kutoka kwake zamani (hadithi zao) ni sahihi, na alikuwa akihitimisha Qur'an kila usiku."

Tazama kitabu Mizanul-Itidali, juzuu ya 3 ukurasa wa 71.

Na Al-Jar'hu wa Ta'dil, juzuu ya 6 ukurasa wa 334.

وقال النسائي: ثقة في حديثه القديم،

Amesema Imamu al-Nasai:

"(Atwaa) ni Thiqa katika hadithi zake za zamani...".

قال حماد ابن زيد أتينا أيوب فقال اذهبوا فقد قدم عطاء بن السائب من الكوفة وهو ثقة اذهبوا إليه فاسألوه عن حديث أبيه في التسبيح.الجرح والتعديل 333/6.

Amesema Hammad Ibn Zaid:

Tulimwendea Ayoub akatwambia: nendeni kwa Atwaa Ibn Al-Saaib, kwa sababu amekuja kutoka sehemu za Kufa, naye ni Thiqa, nendeni mkamuulize kuhusiana na hadithi ya tasbihi (aliyoipokea) kutoka kwa baba yake."

Tazama kitabu Al-Jar'hu wa Ta'dil juzuu ya 6 ukurasa wa 333.

قال يحيى بن سعيد القطان ما سمعت أحدًا من الناس يقول في عطاء ابن السائب شيئا قط في حديثه القديم...
الجرح والتعديل 333/6.

Amesema Yahya Ibn Said al-Qatwan:
Sikuwahi kumsikia mtu yeyote akimsema Atwaa Ibn Al-Saaib kwa jambo lolote kuhusu hadithi zake za zamani…".
Tazama kitabu Al-Jarr'hu wa Ta'dil juzuu ya 6 ukurasa wa 333

وقال أحمد بن عبد الله العجلي: كان شيخا ثقة قديما،
تهذيب الكمال 91/20.

Amesema Ahmad Ibn Abdillahi al-I'jliy:
"Alikua (Atwaa) ni Sheikh, Thiqa, Mtu wa zamani."
Tazama kitabu Tah'dhibul-Kamali juzuu ya 20 ukurasa wa 91.

Kwa mujibu wa kauli hizi za maulamaa imebainika kwamba Atwaa ni mtu mkweli mwenye hifdhi nzuri, na hadithi zake ni sahihi.
Na ama kauli za maulamaa zinazomtia kasoro, makusudio yake ni zile riwaya za wanafunzi wake waliopokea kutoka kwake baada ya kuchanganyikiwa mwishoni mwa umri wake kwa sababu ya utuuzima, ama wale wanafunzi waliopokea kutoka kwake zamani kabla ya kuchanganyikiwa, riwaya zao zote ni sahihi na hakuna mwanachuoni yeyote aliyezitia kasoro.
Na pia imebainika kwamba Hammad Ibn Zaid ni miongoni mwa wanafunzi wake waliopokea hadithi kutoka kwa Atwaa zamani kabla ya kuchanganyikiwa.
Na mpaka hapo yatakuwa madai ya Juma al-Mazrui yameporomoka, na uwongo wake utakuwa umedhihirika.

JARIBIO LAKE LA NNE

Pia amefanya jaribio jingine kwa lengo la kutaka kuiangusha hadithi hii kwa upande wa matni yake.

Amesema Juma, na hapa ninamnukuu:
"Natumesema kabla na kutoa ushahidi kwamba neno "النظر" (al-nadharu) katika lugha ya kiarabu lina maana nyingi. Na haiwezikani bali haitakiwi useme kuwa maana kadha ndiyo iliokusudiwa ila kwa ushahidi".
Mwisho wa kunukuu.
Tazama katika kitabu chake Hoja zenye Nguvu ukurasa wa 188.

Na pia alitangulia kusema katika ukurasa wa 53 kama ifuatavyo:
"Tukitazama maana ya neno hili:" النظر" (al-nadharu) kupitia kiyoo cha Qur'an tunakuta ni:
1) Kutazama kikawaida kwa macho; NA HII NDIYO MAANA YA MSINGI YA NENO HILO...".
Mwisho wa kunukuu.

MAJIBU YETU

Majibu yetu juu ya madai haya batili ni kama yafuatavyo:
Ni kweli neno (al-Nadharu) lina maana nyingi, lakini bila shaka sote tunakubaliana kuwa maana ya asili ya neno hili ni kutazama kwa macho, kama alivyoeleza bwana Juma katika kitabu chake, na kama hivyo ndivyo, basi pia anatakiwa ndugu Juma afahamu kwamba kuna kanuni za kilugha zinazosema kuwa:

ASILI NI KUYATUMIA MANENO KATIKA ASILI YAKE, MPAKA ISHINDIKANE AU IPATIKANE DALILI YA KULITOA NENO NJE YA ASILI YAKE.

Kwahivyo tunasema kwamba; katika hadithi hii neno "al-nadharu" limetumika katika asili yake ile ile, ambayo maana yake ni "kutazama kwa macho" na hakuna hoja wala dalili yoyote inayokubalika kilugha wala kiakili ambayo imesababisha neno "al-

Nadharu” katika hadithi hii litumike nje ya maana yake ya asili, na kama ipo dalili hiyo basi anatakiwa ndugu yetu Juma na jamaa zake watuletee.

Kisha akasema tena ndugu Juma:

“Suala ni kuwa je kutazama huku kulikotajwa hapa ni kutizama nini? Kutazama wenyewe ni kutazama "وجهك" tafsiri ya neno kwa neno ni kutazama “uso wako.”Neno “uso” sote tunalijua maana yake kuwa ni sehemu ya mbele ya kichwa yenye macho pua na mdomo. Lakini je hii ndiyo maana iliyokusudiwa:

kwamba watu watautazama uso wa Mwenyezi Mungu? Jawabu natarajia iko wazi kwa kila mtu kwamba Mwenyezi Mungu hana uso. Sasa kama mwenyezi Mungu hana uso nini maana ya neno “uso wako?” Jawabu ni kuwa neno uso katika lugha ya kiarabu hutumika kwa maana nyingi:

1) Sehemu ya mbele ya kichwa yenye macho, pua na mdomo.Na hii haimuhusu Mwenyezi Mungu kinyume na Mawahabi wanavyosema kuwa Mwenyezi Mungu ana uso kweli kweli !”.

Mwisho wa kunukuu. Tazama maneno yake hayo kwenye kitabu chake “Hoja zenye Nguvu” ukurasa wa 189.

MAJIBU YETU

Majibu yetu sisi ni kama yafuatavyo:

Sisi tunaitakidi kwamba Allah aliye juu ya Ar’shi yake ambaye amekizungukia kila kitu kwa elimu yake, ana sifa nyingi mno kama vile sifa ya: Uhai, Elimu, Uwezo, Nguvu, Uoni, Usikivu, Mikono, Uso na nyinginezo ambazo ni katika sifa zake za utukufu na ukamilifu, na tunamthibitishia Allah sifa zote hizo za ukamilifu kama vile alivyojithibitishia mwenyewe-Jalla Jalaaluh- na kama vile anavyotuthibitishia mjumbe wake mtukufu katika sunna zake.

Pamoja na kuitakidi kwamba wapo viumbe ambao wana sifa kama hizo za; uhai, elimu, uwezo, nguvu, uoni, usikivu, mikono, uso, n.k. lakini sifa zao hizo si kama zile za Allah –Sub'haanah-.
Pamoja na kuwepo kwa sifa hizo na nyinginezo katika pande zote mbili: upande wa Muumba (Allah) na upande wa viumbe, lakini Allah hafanani na yeyote katika viumbe vyake si katika dhati yake wala sifa zake.
Amesema Allah:

" ليس كمثله شيئ وهو السميع البصير"الشورى11

"Hapana kitu chochote mfano wake. Na yeye ni mwenye kusikia mwenye kuona.".

Surat Shuura(42) aya ya 11.

Kwahiyo tunachotakiwa sisi waislamu ni kuthibitisha kile alichojithibitishia Allah mweyewe katika kitabu chake, na huku tukimtakasa kwamba hakufanana na viumbe, kwa kuifanyia kazi kanuni isemayo:
KUFANANA KWA MAJINA YA SIFA, SI DALILI YA KUFANANA KWA SIFA ZENYEWE.
Hivyo basi, sio sahihi kwa mtu yeyote kuanza kukimbilia kwenye kuzikanusha sifa hizo kwa madai ya kutaka kumtakasa Allah na viumbe vyake, kwa mfano:

Miongoni mwa sifa za Allah –Sub'haanahu- ni sifa ya "USIKIVU" kwa maana ya kwamba Allah "ANASIKIA"na jambo hili halina upinzani baina ya waislamu.
Na sifa hii hii ya usikivu pia wanayo viumbe vyake kama vile wanadamu.
Sasa kwa mfano ajitokeze mtu anayejifanya ni bingwa wa kumtakasa Allah aseme; Allah –Tabaaraka wata'alaa- hasikii !
Ukimuuliza kwa nini? Mbona yamekuja maandiko mengi katika Qur'an na Hadithi kuonyesha kwamba Allah anasikia?
Anajibu kwa kusema:

Kwa sababu kusikia ni kuidriki sauti kwa kupitia kiungo maalumu ambacho ni sikio kwa hiyo nikisema kuwa Allah anasikia nitakuwa nimemfananisha na kiumbe
kwa sababu sisi hatufahamu maana ya kusikia ila kwa maana hii tulioitaja.

Bila shaka kiislamu huwa mtu wa aina hii atakuwa amepotoka njia ya sawa sawa na kumfuata sheitwaani mal-u'uni.
Bali lililo la wajibu kwa muumini ni kuithibitisha sifa hii ya usikivu na nyinginezo zilizothibiti pamoja na kuitakidi kwamba KUSIKIA KWA ALLAH SIO KAMA KUSIKIA KWA VIUMBE WAKE!
Halikadhalika anatakiwa katika sifa zote afanye hivyo, kama kuitakidi kwamba:

KUONA KWA ALLAH SI KAMA KUONA KWA VIUMBE VYAKE.
UHAI WA ALLAH SI KAMA UHAI WA VIUMBE VYAKE.
UWEZO WA ALLAH SI KAMA UWEZO WA VIUMBE VYAKE.
USO WA ALLAH SI KAMA USO WA VIUMBE VYAKE.
NGUVU ZA ALLAH SI KAMA NGUVU ZA VIUMBE VYAKE.
MIKONO YA ALLAH SI KAMA MIKONO YA VIUMBE VYAKE.

Na nyinginezo katika sifa ambazo zimethibiti kuwa ni sifa zake – Sub'haanahu wata'alaa-.
Na halikadhalika haifai kumsifia Allah kwa sifa ambazo hakujisifu nazo, na kufanya hivyo ni kumzulia uwongo Allah –Jalla Jalaaluh-. Kwa sababu ya kutoufahamu msingi huu wa kwamba: "KUFANANA KWA MAJINA YA SIFA SIO DALILI YA KUFANANA KWA SIFA ZENYEWE" wamepotea watu wengi, tena pamoja na kupotea kwao huko wakajiona kwamba wao ndio waliokuwa katika haki, na haraka wakaanza kuwatuhumu watu wengine katika imani zao na kuwatia katika makosa tena kwa kutumia lugha chafu tena za kejeli.
Mara utawasikia wanawaita "MUSHABBIHA" (wenye kumfananisha Allah na viumbe) mara wanawaita "MUJASSIMA" (wenye kumfanya

Allah kuwa ana kiwiliwili) kwa madai kwamba eti wanamfananiza Allah na viumbe wake !mara Mawahabi! Basi ilimradi kuwachafua watu wasio na hatia.

Sasa hebu tumgeukie ndugu Juma na wenzake watwambie wao watasema nini kuhusu sifa hii ya kusikia kwa Allah na kusikia kwa viumbe?

Je wataikanusha kwa kusema Allah hasikii –Ma'adha llaahi- (Allah atukinge na hilo)?

Na bila shaka kuitakidi hivyo ni kufuru.

Au watakanusha kwamba mwanadamu hasikii? Na bila shaka huo utakuwa ni wendawazimu.

Na kama jawabu itakua:Allah anasikia na mwanadamu anasikia, halafu wasiutumie msingi huu tulioutaja wa kwamba kusikia kwa Allah si kama kusikia kwa viumbe "kwa sababu kufanana majina ya sifa si dalili ya kufanana sifa zenyewe" basi ni kwa msingi gani watamtakasa Allah na dhana ya "Tash'bihi" (kumfananiza na viumbe)?

Ikiwa hawana hila wala namna ila kurudi katika msingi huu wa haki kwa kusema kwamba:

Mwanadamu anasikia na Allah pia anasikia LAKINI KUSIKIA KWA ALLAH SIO KAMA KUSIKIA KWA MWANADAMU WALA KIUMBE CHOCHOTE !

Sisi tutawaambia mtakuwa mmefanya vizuri, lakini endeleeni kufanya hivyo katika sifa zote za Allah –Tabaaraka wata'alaa- na wala msibague.

Pia semeni kwamba Allah ana uso kama ilivyosema Qur'an na Sunna, lakini uso wake si kama uso wa viumbe kwa sababu hakuna kitu chochote ambacho ni mfano wa Allah.

Kwa hiyo andiko hili sahihi linatuambia kwamba bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- anamuomba mola wake amruzuku neema ya kuutazama uso wake Allah huko peponi, hapa sisi

tunachotakiwa kukifanya ni kuthibitisha kwamba miongoni mwa starehe za peponi ni watu kumuona Allah Jalla Jalaaluh.

Na pia tunatakiwa tuitakidi kwamba Allah ana Uso unaolingana na dhati yake tukufu na hana mfano wa kitu chochote.

Ama madai ya kwamba Allah -sub'haanahu- hana uso kwa dhana ya kwamba tukisema anao uso basi tutakuwa tumemfananisha na viumbe ni madai batili ambayo hayakujengwa juu ya msingi wa kielimu.

Na hiyo ndiyo njia ya watu wote wa bid'a kama Jahmiyya, Mu'utazilah na Khawaarij. Na mwanzo wa kuingia itikadi hizi batili katika safu za waislamu ni baada ya kutarjumiwa vitabu vya Falsafa za Wagiriki na Mapeshia kwa lugha ya kiarabu, na watu wakajishughulisha na vitabu hivyo na wakaiwacha njia ya wema waliotangulia katika kuamini mambo ya ghaibu.

Na huu ni muhtasari wa hoja za wenye kuthibitisha kuonekana Allah kwa macho huko akhera, hoja ziko nyingi lakini kama tulivyoeleza hapo mwanzo kwamba tutazitaja hoja chache kwa lengo la kufupisha, na kulifikia lengo, na walillaahil-hamdu lengo limetimia.

Lengo ni kuwafahamisha watu kwamba itikadi ya kuonekana Allah akhera kwa macho ni itikadi sahihi iliyothibitishwa na kitabu cha Allah (Qur'ani) na Sunna za Mtume Muhammad Swalla llaahu alaihi wasallam, na hiyo ndiyo imani na itikadi ya Maswahaba watukufu na waliowafuatia hao kwa wema, itikadi sahihi ya Ahli-Sunnati wal-Jamaa.

Sasa hebu tuzigeukie hoja za wapinzani wenye kuipinga itikadi hii

SURA YA TANO

HOJA ZA WENYE KUPINGA KUONEKANA ALLAH KWA MACHO HUKO AKHERA.

Kwa mtu yeyote aliyekuwa na itikadi ambayo imesalimika na kutakasika na nongo za bid'a atakuwa si rahisi kwake kuyapuuza na kuyatupilia mbali maandiko ya Qur'an na mafundisho ambayo yamethibiti kutoka kwa Mtume Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam-.

Kwa sababu mambo ambayo yamethibiti kuwa yanatoka kwenye kinywa cha Mtume Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam- ni "WAH'YI" utokao kwa Allah, kwa kuwa mjumbe huyo hazungumzi kwa matashi yake, wala kwa matamanio ya nafsi yake.

Kama tulivyoeleza katika sehemu iliyotangulia kwamba kuna aya za Qur'an na kadhalika hadithi sahihi zinazothibitisha kuonekana kwa Allah kwa macho huko akhera, tena hadithi hizo zimepokewa kwa wingi na Maswahaba wengi, mpaka wataalamu wa hadithi wamefikia kusema kwamba hadithi hizo zimefikia kiwango cha kuwa ni "MUTAWAATIR" (hadithi ambazo zimekuja kwa wingi ambao kikawaida inakuwa ni muhali kuwa wapokezi wake wameafikiana juu ya kutunga uwongo).

Pamoja na maandiko yote hayo sahihi, lakini bado kuna baadhi ya watu wa batili wameyafumbia macho mafundisho hayo, bali wanawataka watu wengine pia nao wayafumbie macho na kuyapuuza.

Katika sehemu hii tutazitaja baadhi ya hoja zao ambazo wanazitegemea watu hao katika kuyapotosha maandiko sahihi, kama alivyozitaja ndugu Juma M. Al-Mazrui kwenye kitabu chake "Hoja zenye Nguvu".

Na katika hoja zao hizo kuna hoja za aina mbili:

i) Kuna hoja alizoziita za kiakili.

ii) Na kuna hoja za kimaandishi.

Hapa tunaanza na hizo hoja zao za kiakili;

Amesema ndugu Juma:

"Baada ya kuzijadili hoja ambazo wamezitegemea wale wenye itikadi ya kumuona Mwenyezi Mungu na kuzibainisha udhaifu wake, sasa natugeukie upande wa pili na kujadili hoja za kundi jengine nalo ni kundi la wenye kukataa itikadi hiyo.Na wao pia wana hoja za namna mbili.

Hoja za kwanza ni hoja za kiakili na za pili ni hoja za kimaandishi.Na hoja hizi ziko nyingi sana kazitaja baadhi yake Al-imamu Badrudin Sheikh Al-Mufasirin Al-Khalili katika kitabu AL-HAQ AL-DAMIGH ukurasa wa 67.

Miongoni mwa hoja hizi ni kuwa kuona kwa macho ambako tunakujua ni kuingia sura ya chenye kuonekana katika mboni ya macho ya mtazamaji kwa nguvu za mionzi yenye kuvuta sura hio. Nayo ina shuruti:

1) Moja ni kuwa chenye kuonekana kiwe ni kitu ambacho kinajuzu kuonekana. Hii inavitoa vitu kama roho, akili, upepo, sauti na mengineyo ambayo hayaonekani.

2) La pili ni kuwa mwenye kuona akielekee anachokiona au kidhihiri katika kitu kama kiyoo kisha ndiyo akitazame.

3) Jambo la tatu ni kuwa chenye kuonekana kisiwe kidogo sana kama bektiria.

4) Jambo jengine ni kuwa chenye kuonekena kisiwe karibu sana na macho ya mtazamaji kama mtu akiweka mkono wake kwenye macho mpaka macho yasiwezekufumbuka.
5) Jambo la tano ni kuwa chenye kuonekana kisiwe mbali sana. Katika hali hii mtazamaji anakuwa hakioni, na ndiyo maana kuna vitu vingi anga za juu ambavyo hatuvioni pamoja na kuwa vitu hivyo ni vikubwa sana katika umbo lake lakini umbali baina yetu na baina yake umetuzuia tusivione. Hizi ni baadhi ya hoja za kiakili tu kuhusiana na shuruti baina ya chenye kuonekana na chenye kuona.
Lakini cha msingi zaidi ni hoja za kimaandishi".
Mwisho wa kunukuu.
Tazama kitabu "Hoja zenye Nguvu" ukurasa wa 271-272.

MAJIBU YETU

Majibu yetu juu ya hoja hizi ni kwa njia tatu:
1) Hakuna katika maneno haya yote tuliyoyanukuu kutoka kwa ndugu Juma ushahidi wa kutoonekana Allah kwa macho huko akhera, na wala hapo hakuna akili iliyotumika katika kuyathibitisha madai hayo batili.

2) Maelezo yote yaliyotolewa yanahusiana na hali ya hapa duniani, ama huko akhera mambo yatakuwa tofauti kabisa na hapa duniani, kuna mambo ambayo ni muhali kufanyika hapa duniani, lakini huko akhera yatafanyika. Kwa mujibu wa maandiko sahihi ya dini yetu

mambo ya huko akhera yako tofauti kabisa na mambo ya hapa duniani.

Kwamfano, tunaambiwa kwamba huko akhera vitu kama mikono, miguu, ngozi ya mwili, ardhi na vinginevyo vyote hivyo vitatamka na kutoa ushahidi dhidi ya mwanadamu, hata vile visivyo na uhai kama vile mawe vyote hivyo vitasema !

Siku hiyo kubwa na ya kutisha watakuwepo watu ambao watatembea kwa nyuso zao badala ya miguu yao!!! Na mtu atayaona ya mbali yake kama anavyoyaona yaliyo karibu yake!

Na huko peponi hakuna kushiba wala kwenda haja kama duniani, na kutakuwa na mambo mengi ya ajabu ambayo ni tofauti na mambo yalivyo hii leo hapa duniani.

Kwa hiyo, si sahihi kabisa, kulifananisha suala hili la kuona hapa duniani na kuona huko akhera.

Pia si sahihi kuitakidi kuwa lile lisilowezekana hapa duniani, kuwa hata huko akhera haliwezekani, bali kufanya hivyo ni hila ya kutaka kuyapinga maandiko sahihi yanayotuelezea habari za ghaibu, na mwenye kufanya hivyo atakuwa ni mpungufu wa imani, au hana imani kabisa, na wala hakuitumia akili yake vizuri katika kuzitafakari aya za Qur'an na Hadithi sahihi za Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam-.

Sisi maudhui yetu hapa ni kuhusu suala la je, Allah ataonekana kwa macho huko akhera au hatoonekana? Na wala hautuzungumzii suala la kuonekana Allah hapa duniani.

3) Mambo ya huko Akhera hufaamika kwa maandiko ya Wah'yi na sio kwa akili za watu, lile ambalo limethibiti kwa maandiko ya kisheria hilo ndilo la haki, hata kama linapingana na akili zetu, na tunatakiwa tuliamini hivyo hivyo lilivyoelezwa, bila ya kupinga wala kutia shaka na kufanya hivyo ndiyo ukamilifu wa kuamini mambo ya ghaibu.

Kwa hiyo ninathubutu kusema kuwa; hizi hoja alizo zinukuu Juma kutoka kwa sheikh wake al-Khalili, ambazo wameziita kuwa ni hoja

za kiakili; haikutumika akili hata chembe katika kuzithibitisha bali akili iko mbali na hoja hizi.
Ukiwa ndugu msomaji umeufahamu upeo wa akili zao katika kuzithibitisha hoja hizo, hebu sasa natuzitazame hoja zao walizoziita za kimaandishi:

HOJA YAO YA KWANZA

Amesema Juma M. Al-Mazrui:
"Ushahidi wa kwanza walioutegemea wale wenye kusema kuwa Mwenyezi Mungu haonekani katika Qur'ani Tukufu ni aya ya 103 ya sura ya 6 inayosema kwamba;

" لا تدركه الأبصار وهو يدرك الأبصار وهو اللطيف الخبير".

"Macho hayamdiriki (hayamfikii) Naye ni mwenye kuyadiriki (kuyafikia) Naye ni Mjuzi wa yasiyo dhahiri na ni Mjuzi wa yaliyo dhahiri".

Sura ya 6 aya ya 103".

Akasema tena Juma:
"Aya hii inatoa dalili ya uwazi juu ya kukataa kuonekana kwa Mwenyezi Mungu....Na hoja ambayo imo katika aya hii ni kwamba Mwenyezi Mungu anasema kuwa "macho hayamdiriki yaani hayamfikii" na kufikia kwa macho ni kuona, na kwa maana hio macho hayamuoni".
Akaendelea kusema Juma:
"Na hii ni sifa ambayo Mwenyezi Mungu anaisifu nafsi yake kwa sifa hio, kwahivyo haijuzu kuthibitisha kinyume chake.
Halikadhalika hii ni habari kutoka kwake, na maneno yake hayabadiliki".

Kisha akaendelea kusema tena:

"Hii ndiyo hoja ya wale wanaosema kuwa Mwenyezi Mungu haonekani:

Kwamba hapa Mwenyezi Mungu anajisifu hivyo kuwa yeye hafikiwi na jicho na sifa za Mwenyezi Mungu ni zile zile: hazijabadilika tangu enzi na azal na hazibadiliki wala hazitobadilika huko akhera, kwa sababu Mwenyezi Mungu Yeye amekamilika katika Dhati Yake na katika sifa Zake: hahitaji sifa za ziada ili azidi kuwa mkamilifu zaidi: hivyo hivyo alivyo sasa ndivyo alivyokuwa kabla na ndivyo atakavyokuwa huko akhera na milele".

Mwisho wa kunukuu.

Tazama maneno yote haya katika ukurasa wa 272 wa kitabu chake "Hoja zenye Nguvu".

MAJIBU YETU

Majibu yetu hapa yatakuwa kwa njia tatu:

Njia ya kwanza:

Ni kumkumbusha ndugu yetu Juma M. Al-Mazrui kwamba hana haja yeye ya kujikakamua katika kuzifafanua aya za Qur'an. Kwa sababu kazi hii ya kufafanua ni ya bwana Mtume Muhammad –swalla llaahu alayhi wasallam- yeye ndiye aliyetumwa na Mola wake –Tabaaraka Wata'alaa- kwa ajili ya kazi hiyo, bila shaka mjumbe huyo mtukufu ameitekeleza kazi yake kwa ufanisi wa hali ya juu kabisa, hasa hasa katika yale mambo ambayo wanayahitajia watu kuhusu Mola wao Mtukufu, bila ya shaka mambo hayo ameyafafanua kwa kiasi cha kutosha.

Kwa sababu haiwezekani kuwa mjumbe huyo ametufafanulia kila kitu mpaka adabu za kukidhi haja kisha katika suala linalofungamana na kumjua Mola wetu akatuacha hivi hivi bila ya ufafanuzi wowote!

Sidhani kwamba yuko mtu yeyote katika waislamu mwenye kudai kwamba Mtume Muhammad –swalla llaahu alayhi wasallam- kuna mambo ameyaficha, au kwa lugha nyingine amefanya khiyana katika kazi yake ya kufikisha ujumbe.

Na kama sote tunakubaliana kwamba Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- ametubainishia kila kitu na kutufafanulia, bila shaka miongoni mwa hayo aliyotubainishia na kutufafanulia ni suala zima la kuonekana na kutokuonekana Allah.
Kama hivyo ndivyo, je yeye amesemaje ? Na je aya hizi amezibainisha vipi?

Ndugu Juma na washirika wake hawakuzitaka hadithi za Mtume – swalla llaahu alayhi wasallam- ndiyo maana wakazijengea mazingira ya shaka kwa madai ya kwamba eti ni hadithi dhaifu! Tena kwa kutumia uwongo na hadaa!.

Na mimi nina matumaini makubwa kuwa ndugu yangu msomaji umebainikiwa kwa kiasi kikubwa na uwongo wao, hasa kwa ufafanuzi wa kielimu tulioutoa hapo nyuma kuhusu usahihi wa hadithi hizo za Mtume Muhammad –swalla llaahu alayhi wasallam- .

Amesema Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- alipokuwa akiifafanua aya ya 26 ya surat Yunus:

"..Basi litaondolewa pazia na watamtazama yeye Allah na HAWAJAWAHI KUPEWA KITU WANACHO KIPENDA MNO KULIKO HUKO KUMTAZAMA YEYE (ALLAH) NA HIYO NDIYO ZIADA" !!!
Tazama sahihul muslim hadithi namba 449.

Na amesema tena Bwana Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam-:
"Kwa hakika nyinyi MTAMUONA MOLA WENU kama mnavyouona huu mwezi, hamsongamani katika kuuona…".
Tazama Sahihul-Bukhari hadithi namba 7434.

Na imepokewa kutoka kwa Ummu Dardai kwamba swahaba mtukufu Fadhaala bin Ubaid alikuwa akisema:

“Ewe Allah ! Kwa hakika mimi ninakuomba wewe kuridhika baada ya hukumu, na ubaridi wa maisha baada ya mauti na LADHA YA KUUTAZAMA USO WAKO !!
Na shauku ya kukutana na wewe pasi na madhara yenye kudhuru wala fitina zenye kupoteza”.
Na akasema kwamba hiyo ni dua ambayo alikuwa akiiomba Mtume Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam-.

Tazama kitabu al-Sunna cha Imamu Ibn Abi A’asim ukurasa wa 197 hadithi namba 427 kutoka kwa Fadhaala bin Ubaid.
Na 424 na 425 zote kutoka kwa Ammar bin Yaasir.
Na Sunanul-Nasaai hadithi namba 1305 na 1306 pia zote kutoka kwa Ammar bin Yaasir.

Njia ya pili:
Ni kuhusu kauli yake aliposema:
“Na hii ni sifa ambayo Mwenyezi Mungu anaisifu nafsi yake kwa sifa hio, kwahivyo haijuzu kuthibitisha kinyume chake.
Halikadhalika hii ni habari kutoka kwake,na maneno yake hayabadiliki”.
Mwisho wa kunukuu.

Labda kwanza tuanze kumjibu kwa njia ya swali, kisha ndiyo tutaleta maelezo sahihi juu ya suala hili, na swali lenyewe ni hili:
Miongoni mwa sifa za Allah ni rah’ma (huruma) sifa hii ya Allah hapa duniani imewaenea viumbe wake wote majini na watu, wema na waovu, vilivyo na uhai na visivyo na uhai.
Je sifa hiyo, hivyo ilivyokuwa hapo azal (kale) na ilivyo sasa hapa duniani ndivyo itakavyo kuwa mpaka huko akhera?
Je makafiri nao watapata rehma za Allah huko akhera? Au watakua mbali na rehma hiyo na watakuwa katika ghadhabu zake za milele na laana?

Na kama hawataipata huruma hiyo ambayo ni sifa yake Allah iliyoenea kwenye kila kitu, je itakuwa sifa hiyo imebadilika?

Na je maneno ya Allah aliposema:

وَرَحْمَتِي وَسِعَتْ كُلَّ شَيْءٍ الأعراف156}

"Na rehema yangu imekienea kila kitu.."

katika sura ya 7 aya 156.

Na aliposema:

"ربنا وسعت كل شيئ رحمة وعلما"

"Ewe Mola wetu! Umekienea kila kitu kwa rehema na ujuzi".

Katika sura ya 40 aya ya 7,

yatakuwa nayo yamebadilika?

Majibu ya maswali haya ndiyo majibu yetu ya; kwanini Allah asionekane hapa duniani, lakini huko akhera aonekane.

Njia ya tatu:

Sisi tunasema kwamba: Allah –Sub'haanahu Wata'alaa- hufanya analolitaka, kwa namna anayotaka, kwa wakati anaotaka, na hakuna wa kumuuliza kwanini amefanya hivyo.

Ameshatueleza Allah kupitia Qur'an, na kadhalika Sunna za Mtume wake –swalla llaahu alayhi wasallam- pia zimetueleza kuwa hakuna atakayemuona yeye kwa macho yake hapa duniani.

Ama huko Akhera Allah kwa ih'sani zake na fadhila zake atawakirimu waja wake wema kwa kuwaondoshea pazia na watamuona Mola wao mkarimu kwa macho yao.

Na yeye huyo huyo ndiye aliyetuelezea kupitia Qur'an na Sunna za Mjumbe wake mtukufu kwamba huruma yake hapa duniani imewaenea waja wake wote wema na waovu, lakini huko akhera mambo yatakuwa tofauti, huruma yake itawahusu watu wema tu, na wale waliomkufuru hawataipata huruma yake abadan, bali wataishi katika ghadhabu zake na laana milele na milele -Allah atukinge na ghadhabu zake na laana zake-.

Na sisi tunapokuwa tunaitakidi hivi hatusemi kuwa kauli ya Allah imebadilika kama anavyodai ndugu Juma na Sheikh wake Al-Khalil, bali huo ni ufahamu wao finyu wa maandiko sahihi, na hayo ndiyo madhara ya kufuata hawaa za nafsi, lau kama wangeridhika na ubainifu wa Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- wasingepata taabu yote hii, lakini hiyo ndiyo jazaa na malipo ya kuyapuuza mafundisho sahihi ya Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- na kutanguliza akili zao mbele ya maandiko sahihi, na hiyo ndiyo kawaida ya watu wa bid'a wote.

Sisi tunasema kwamba zote hizo ni hukumu zake Allah, na yeye anafanya anachokitaka na anahukumu anavyopenda.

Miongoni mwa juhudi za Juma M. Al-Mazrui za kuyapuuza mafundisho ya Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- ni pale aliposema;

"Lakini hata kama kuna andiko jengine lenye kutoa ushahidi wa kuonekana Mwenyezi Mungu <u>basi ni lazima lifasiriwe kwani</u> aya hii tunayoijadili hapa inakataa na <u>kwa sababu hii ni sifa ya Mwenyezi Mungu haiwezekani ikawa kutoonekana huko ni kwa baadhi ya watu tu.</u>

Lakini hata hivyo tunasema kwamba hakuna ushahidi mwengine sahihi kwamba Mwenyezi Mungu ataonekana.

Ama dalili zao walizozitegemea katika hadithi tumebainisha kuwa zote ni batili wapokezi wake ni madhaifu na waongo watupu". !!!

Mwisho wa kunukuu.

Tazama ukurasa wa 292 wa kitabu chake "Hoja zenye Nguvu".

Zingatia ndugu msomaji:

Juma anasema kuwa "..hata kama kuna andiko jingine lazima lifasiriwe" !!!

Akiwa anakusudia kwamba, hata kama imekuja aya au hadithi sahihi inayoelezea kwa uwazi kabisa; kwamba watu wema watamuona Mola wao huko akhera, basi lazima maandiko hayo yatafutiwe maana nyingine, lakini isiwe maana ya kuonekana Allah ! Yaani hata

zingekuja aya arobaini au sabini na hadithi mia tano zinazosema wazi wazi kwamba waumini watamuona Allah huko akhera kwa macho yao, Juma anasema lazima maandiko yote hayo hayatasaidia kitu, bali lazima yatafutiwe maana nyingine ili mradi maana hiyo isiwe kuona !!

Swali, kwanini kuwe na ulazima wa kufasiriwa maandiko yanayothibitisha kuonekana Allah ?

Kwanini yasifasiriwe maandiko mengine mnayodai kuwa yanakanusha kuonekana Allah huko akhera kwa macho?

Lakini Juma alipojua kuwa kuna maandiko mengine yaliyo sahihi yanayopingana na fikra zake potofu, na hana uwezo wa kuyajibu ndiyo akaamua kuitumia lugha hii ya kuifunika haki !

Sisi kama kawaida yetu tunayaamini na kuyakubali maandiko yote yaliyomo kwenye kitabu cha Mola wetu, na maandiko yote sahihi yaliyothibiti kutoka kwa Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam-.

Ndiyo maana maulamaa wakubwa wa Ahli Sunna wakaitumia kanuni ya upatanisho wa maandiko ambayo dhahiri yake yanaonekana kugongana wakasema kuwa; kilichokataliwa na aya hii ni kumuona Allah kwa kumdhibiti na wala si suala la kumuona.

Njia ya nne:

Ni kuhusu pale aliposema:

"..na kwa sababu hii ni sifa ya Mwenyezi Mungu haiwezekani ikawa kutoonekana huko ni kwa baadhi ya watu tu".

Tukimuuliza Juma, kwanini haiwezekani kuwa Allah hatoonekana na baadhi ya watu?

Je haiwezekani kwanani ? Na kwanini ?

Hata kama Allah na Mtume wake wamesema kuwa jambo hilo linawezekana?

Je utajibu nini kuhusu suala la rehma ya Allah?

Je nayo haiwezekani kutowapata baadhi ya watu kwa sababu ni sifa ya Allah?

Amesema tena ndugu Juma:

"Lakini hata hivyo tunasema kwamba hakuna ushahidi mwengine sahihi kwamba Mwenyezi Mungu ataonekana.

Ama dalili zao walizozitegemea katika hadithi tumebainisha kuwa zote ni batili wapokezi wake ni madhaifu na waongo watupu" !!!

Mwisho wa kunukuu.

Tazama ukurasa wa 292 wa kitabu chake "Hoja zenye Nguvu".

Jawabu yetu:

Ama madai ya ndugu Juma kuwa dalili zote tulizozitegemea ni batili na wapokezi wake ni madhaifu na waongo watupu, madai hayo si ya kweli, bali tunasema kwamba madai yake hayo ni batili na tena ni dhaifu na yeye ndiye mwongo mkubwa.

Kwanini tunasema hivyo?

Naam, yeye ameidhoofisha hadithi ya Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- pale aliposema kuhusiana na kauli ya Allah:

"Wale waliofanya mema watapata wema na ziada".

Akasema Mtume swalla llaahu alayhi wasallam;

Watakapoingia watu wa peponi katika pepo atanadi mwenye kunadi: hakika nyinyi mna ahadi mbele ya Allah anataka kukutekelezeeni.

Watasema kwani hukuzing'arisha nyuso zetu? Na hukutuokoa na moto na ukatuingiza peponi?

Akasema (Mtume swalla llaahu alayhi wasallam);

Basi ataondoa pazia, (na watamtazama Allah), naapa kwa Allah: HAWAJAWAHI KUPEWA KITU WANACHOKIPENDA ZAIDI KULIKO KUMTAZAMA YEYE (Allah subhaanahu wata'alaa).

Na katika riwaya ya Abdulrahamaan Ibn Abi Layla kutoka kwa Suhaib kwamba Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- aliisoma aya hiyo kisha akasema;

‘‘..Basi litaondolewa pazia na watamtazama yeye Allah na hawajawahi kupewa kitu wanachokipenda mno kuliko huko kumtazama yeye NA HIYO NDIYO ZIADA”.
Tazama sahihul muslim hadithi namba 449.
Ndugu Juma yeye akasema katika kitabu chake ‘‘Hoja zenye nguvu ’’ katika ukuasa 111:

‘‘..na hapa nitakunakilia namna mbili tu katika maneno ya AL IMAMU SAID BIN MABRUK AL- QANNUBI IMAMU WA HADITHI ,FIQHI NA USULI uone jawabu yake juu ya hadithi hii...anasema Al imamu Al qannubi:
‘‘Na hadithi hii ni batili na ubainifu wa haya ni kwa njia mbili:
Ni kuwa katika sanad yake yumo HAMAD BIN SALAMA,naye japo kuwa ni mkweli katika nafsi yake lakini
HIFDHI YAKE NI MBOVU:
ANASAHAU na
KUKOSEA na
AMECHANGANYIKIWA na KUBADILIKA MWISHONI MWA UMRI WAKE; kwahivyo yeye hafai kuwa hoja’’.
Mwisho wa kunukuu.
Sisi tukamjibu kama ifuatavyo:
Madai yake kwamba Hamad bin Salama hifdhi yake ni mbovu, anasahau, anakosea na amechanganyikiwa na kubadilika mwishoni mwa umri wake.
Madai haya si kweli na mwenye kudai hilo anatakikana alete ushahidi juu ya hilo.
1-Amesema Imamu Ahmad bin Hambali:
‘‘Mtu madhubuti kuliko wote (waliopokea kutoka kwa) Thabit ni Hamad bin Salama’’.
Na hadithi hii Hamad bin Salama ameipokea kutoka kwa Thabit.
Na amesema tena kuhusu Hamad bin Salama kuwa ni:
(mtu) madhubuti’’.

2-Amesema Imamu Yahya bin Mai'n:
''Yeyote atakayetofautiana na Hamad bin Salama kuhusu (mapokezi kutoka) kwa Thabit kauli (ya kuchukuliwa) ni kauli ya Hamad''.
Pia amesema tena:
(Hamad bin Salama) ni ''Thiqa'' (muadilifu mwenye hifdhi nzuri).

3-Amesema Al Imamu al Saajiy:
''Alikuwa (Hamad bin Salama) mwenye kuhifadhi tena ni ''Thiqa'' (muadilifu) na ni mwenyekuaminiwa''.

4-Amesema Al-Imamu Ibn Sa'ad:
''Na alikuwa (Hamad) ni mtu thiqa (muadilifu mwenye hifdhi nzuri) mwenye hadithi nyingi, lakini ni mara chache anasimulia hadithi Munkar''.
Hapo limetumika neno la kiarabu ''Rubba maa'' nalo huleta maana ya uchache.

5-Amesema Al-Imamu Al-I'jliy:
(Hamad) ni: ''Thiqa (muadilifu mwenye hifdhi nzuri) mtu mwema mwenye hadithi nzuri''.

6-Amesema Al Haafidh Ibn Hajar katika kitabu chake al Taq'ribu uk 195:
Hamad bin Salama bin Dinar al Basriy Abu Salama ni Thiqa (muadilifu mwenye hifdhi nzuri) mcha Mungu na ni mtu madhubuti (miongoni mwa waliopokea kutoka) kwa Thabit,na hifdhi yake ilibadilika mwishoni mwa umri wake''.

7-Amesema Al-Imamu Aliy bin Abdillahi bin al Madiniy sheikh wake Imamu al Bukhariy:
''Ukimsikia mtu anamsema kwa ubaya Hamad bin Salama basi mtuhumu (mtu huyo)''.

Tazama vitabu vifutavyo:
Al-Thiqaat cha Ibn Hibbaan juzuu ya 6 ukurasa 216.
Twabaqaat cha Ibn Sa'ad juzuu ya 7 ukurasa 282.
Taarikhu Thiqaat cha Al-I'jliy ukurasa 131.
Tah'dhiibu Tah'dhiib juzuu ya 1 ukurasa10-13.
Taqribul Tah'dhiib Tar'jama namba 1636.

Hivi unadhani Juma kwa kutumia uwongo dhidi ya mpokezi huyo wa hadithi unadhani kuwa hoja zako zitakuwa sahihi na zetu ndiyo batili?
Hapana, ukweli utabaki kuwa ni ukweli tu, mpaka siku ya Qiyama, na uwongo utaendelea kuwa ni uwongo.
Kwa kweli ndugu Juma amefanya majaribio mengi dhidi ya hadithi nyingi za Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- lakini –Al-Hamdu lillaahi- hakufaulu, na ukirejea majibu na maelezo yetu hapo nyuma juu ya upotoshaji wake utalibaini hilo.

Na amefanya hivyo kwa makusudi ili akifika katika aya kama hizi zinazohitajia ufafanuzi wa bwana Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- aseme kama alivyosema katika ukurasa wa 296:

"Ama hadithi tumezibainisha kwa mizani ya elimu ya hadithi kuwa hakuna hata moja katika hadithi zao hizo ilio sahihi.
Kwahivyo madai haya ya kuwa kuna maandiko mengine yenye kusema kuwa Mwenyezi Mungu ataonekana, si madai sahihi wala hayana maana yoyote"!
Mwisho wa kunukuu.

Nadhani ndugu msomaji utakuwa umeshafahamu kuwa ndugu Juma hayuko sahihi na yeye ndiye asiye na maana yoyote.

Njia ya tano:
Jawabu yetu hapa pia itakuwa kwa njia ya maswali:

Katika misingi ya sheria ya kiislamu, kama maana ya kilugha ikitofautiana na maana ya kisheria ni ipi itakayotangulizwa na kufanyiwa kazi?

Bila shaka jawabu itakuwa: maana itakayo tangulizwa ni maana ya kisheria, na sheria ya kiislamu inapitishwa kupitia Qur'an na Sunna, na Qur'an na Sunna zinatuelezea kuwa waumini watamuona Mola wao huko akhera.

Na hapa duniani hakuna mtu yeyote aliyemuona wala atakaemuona Allah –Jalla Jalaahu-.

Kwa hiyo maandiko yote: aya za Qur'an na Sunna sahihi za Mtume yanatakiwa kufanyiwa kazi bila ya kuyabagua wala kuyafanyia kazi baadhi na kuyatupa baadhi.

HOJA YAO YA PILI

Amesema ndugu Juma M. Al-Mazrui katika kitabu chake "Hoja zenye Nguvu" ukurasa wa 301:

"Dalili ya pili ambayo wanaitegemea wale wenye kusema kuwa Mwenyezi Mungu haonekani, ni jawabu ya Mwenyezi Mungu kwa Nabii Musa alipomwambia:

"لن تراني"

"Hutoniona"

Sura ya 7 aya 143.

Hakika jawabu hii haijahusishwa na wakati maalumu : Mwenyezi Mungu anamkatalia Mussa kuwa hatamuona na hii inamaanisha kuwa "hutoniona" sasa hivi wala baadae kwa sababu herufi hii "لن" (Lan) wataalamu wa lugha ya kiarabu wanaita kuwa:

"حرف نفي ونصب واستقبال وهو يفيد التأكيد أو التأبيد"

"Herufi ya kukataa na kukitia fat'ha ! kitendo na kuonesha wakati unaokuja nayo inamaanisha kutilia mkazo au kuonesha umilele kwa hicho kitu kilichotajwa".

Majibu yetu kuhusu madai haya yatakuwa katika nukta tatu muhimu:

Nukta ya kwanza:

Ni kuhusu kauli yake aliposema:

".. kwa sababu herufi hii "لن" (Lan) wataalamu wa lugha ya kiarabu wanaita kuwa:

"حرف نفي ونصب واستقبال وهو يفيد التأكيد أو التأبيد"

"Herufi ya kukataa na kukitia fat'ha ! kitendo na kuonesha wakati unaokuja nayo inamaanisha kutilia mkazo au kuonesha umilele kwa hicho kitu kilichotajwa".

Mwisho wa kunukuu.

Kwanza kabisa maneno hayo si ya kweli, bali huo ni msimamo wa Zamakh'shariy na wengineo katika watu wa bid'a, ama msimamo wa maulamaa wa haki ni kuwa neno "Lan" peke yake halileti maana ya umilele, mtiririko wa maneno ndiyo ambao unaainisha maana, na kuifanya iwe inaleta maana ya umilele au maana ya muda maalumu. Amesema Imamu Ibn Malik:

من رآ النفيَ بلن مؤبداً *** فقوله اردد وسواه فاعضُدا

Na mwenye kuona kukanusha kwa "Lan" ni kwa milele, basi kauli yake irudishe na ipe nguvu kauli (nyingine) isiokuwa hiyo.

Kwa mujibu wa utafiti wa kielimu ni kwamba herufi "Lan" ikiwa katika mtiririko wa maneno inafanya kazi kuu nne:

1) Kukana/Kukataa.

2) Kunasibisha "Mudhari'u" (Kitendo kilichokuwa na maana ya sasa au baadaye)-Ndugu Juma yeye amesema kutia fat'ha, na hivyo si sahihi kwa sababu fat'ha ni alama tu katika alama za Nasbu, kitendo kinaweza kutiwa fat'ha na ikawa si nasbu, na pia kinaweza kunasibishwa bila ya kutiwa fat'ha, na mifano katika hilo ni mingi haidhibitiki-.

3) Kuonesha wakati ujao.

4） i） KUTILIA MKAZO. ii） AU KUONESHA UMILELE, ukiwa mtiririko wa maneno umeanisha hivyo.

Na ukiyatazama kwa makini maneno ya Juma kuanzia 307-310 katika kitabu chake utaona namna anavyojizonga mwenyewe, na mwisho wa yote anathibitisha kwamba "Lan" haina maana moja, bali pia ina maana ya KUTILIA MKAZO.

Kama kweli Juma anakubali kuwa "Lan" ina maana zaidi ya moja, basi kwanini yeye ameing'ang'ania maana moja tu katika aya hii （maana ya umilele） ? Na kwanini asiitumie maana hiyo ya pili （ya kutilia mkazo） ?

Kitu kibaya zaidi ni pale alipofikia kudai kwamba kuitafsiri aya hiyo kwa maana ya pili ya "Lan" （KUTILIA MKAZO） ni kwenda kinyume na aya！

Amesema Juma:

"Na kama tutadai kuwa Mwenyezi Mungu ataonekana basi itakuwa kinyume na aya hii ambayo inakataa MILELE"！！！

Mwisho wa kunukuu.

Sisi tunasema aya hii haijakataa milele, kwa sababu "Lan" hapa haina maana ya MILELE, bali ina maana ya "KUTILIA MKAZO" kama alivyo tunakilia kauli kutoka kwa wataalamu wa lugha ya kiarabu！

Pia amesema Ibn Malik:

من رأى النفيَ بلَن مُؤبَّداً * فقولَه اردُد وسِواه فاعضُدا

Mwenye kuona kukanusha kwa Lan ni kwa milele kauli yake irudishe （usiikubali） na ipe nguvu kauli nyingine

Kama Juma analo andiko jingine la kuyatilia nguvu madai yake hayo, ili iwe herufi "Lan" hapa haikutumika kwa maana nyingine isipokuwa umilele tu basi na alilete.

Na kwa hakika hasa, hana andiko lolote zaidi ya kutumia akili yake kwenye kuzipindisha aya za Allah.

Na kwa bahati nzuri na sisi pia tunao uwezo wa kuzitumia akili zetu vizuri sana katika kuzitafsiri aya.
Nyinyi mkisema kuwa Allah hataonekana kwa macho kisha mkazitumia akili zenu katika kuyatafsiri maandiko yaliyobeba zaidi ya maana moja.
Na sisi tukasema hapana, Allah ataonekana kwa macho huko akhera kisha tukazitumia akili zetu katika kuyatafsiri maandiko hayo hayo, bila shaka hapo zitakuwa akili zetu zimetofautiana.

Swali, je ni akili ya nani itakayo kuwa hakimu kati ya akili za pande hizi mbili zilizotofautiana? Tena ikawa akili hiyo ni lazima kutiiwa katika hukumu iliyoitoa?
Au mambo yataachwa hivi hivi tu, na kila mtu atakuwa yuko huru kufuata upande anaoutaka?
Kama jawabu litakuwa ndiyo, je dini ya Allah itabakia? Au zitakazobakia ni akili za watu?

Na kama jawabu ni hapana, je ni nani huyo hakimu wa kuutatua mgogoro huu wa ufahamu juu ya aya hizi tata? Je ni hizi akili tete?

Bila shaka hakimu bora ni yule aliyechaguliwa na Mola mwenye kitabu hicho, kwa ajili ya kufanya kazi ya kututafsiria na kutubainishia kitabu cha Mola wetu, na hakuna mwingine zaidi ya Mtume wetu Muhammad –swalla llaahu alayhi wasllam-.

Nukta ya pili:
Sisi tunasema "Lan" hapa haina maana ya milele, kwa hiyo watu wema watamuona Mola wao kwa macho yao huko akhera.

Ndugu Juma na kaumu yake wao wanasema kwamba; hapana! "Lan" hapa ina maana ya umilele, kwa hiyo hakuna atakayemuona Allah kwa macho si hapa duniani wala huko akhera.

Kwa kuwa neno hili limebeba zaidi ya maana moja "haiwezekani kusema kwamba maana fulani ndiyo iliyokusudiwa ila kwa dalili na ushahidi, kama inavyosema kanuni (principle) ya misingi ya sheria ya kiislamu "Fundamentals of Islamic Jurisprundence) kwamba:
"Dalili ikiwa na maana nyingi, basi ushahidi huanguka"!

Haya ni maneno ya ndugu Juma katika kitabu "Hoja zenye Nguvu" ukurasa wa 51-52 alipokuwa akiipinga maana ya neno (Nadharu) kwa maana ya kuona.

Kwa hiyo aya hii si hoja ya kukataa kuonekana Allah kwa macho huko akhera, bali inahitajika dalili ya kuiainisha maana hiyo na kuipa nguvu.

MAJIBU YETU

Swali, je Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- anasemaje?
Swali hili litajibiwa katika nukta ifuatayo:
Nukta ya tatu:

Amesema Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam-:
وعن أبي أمامة رضي الله عنه قال خطبنا رسول الله صلى الله عليه وسلم فكان أكثر خطبته يحدثنا عن الدجال ويحذرنا منه وإنه يبدأ فيقول أنا نبي ولا نبي بعدي. ثم يثني فيقول: أنا ربكم. ولن تروا ربكم حتى تموتوا...الحديث"

"Imepokewa kutoka kwa Abu Umamah –Radhia llahu An'hu- amesema:
"Ametuhutubia Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- ikiwa sehemu kubwa ya hotuba yake anatusimulia kuhusu Al-Dajjaal na akawa anatutahadharisha naye.
(Dajjaal) Ataanza kwa kusema mimi ni Nabii, na hakuna Mtume baada yangu.
Kisha atasema: Mimi ni Mola wenu, na HAMTOMUONA MOLA WENU MPAKA MTAKAPOKUFA....".

Haditihi hi ni sahihi ameipokea Al-Imamu Ibn Abi A'sim kwenye kitabu chake Al-Sunna ukurasa wa 198 hadithi namba 429.
Kwa sanad hii ifuatayo,amesema:

"Ametusimulia Abu Umayr, amesema: Ametusimulia Dhamrah, kutoka kwa Al-Saybaaniy kutoka kwa Amri Ibn Abdillahi Al-Hadh'ramiy, kutoka kwa Swahaba Abu Umamah –Radhiya llaahu An'hu-".
Hebu sasa tuanze kuwachambua wapokezi wa hadithi hii, je wanadosari zozote?
Kwanza tuanze na mtunzi wa kitabu, naye ni:
Al-Imamu Al-Hafidh Abu Bakri Amru Ibn Abi A'sim Al-Dhahaak Ibn Makh'lad Al-Shaybaniy ambaye amefariki mwaka 286 H.

Je wanachuoni wa kiislamu wanasemaje kuhusu yeye?
1) Amesema Imamu Al-Dhah'biy kuhusu mwanachuoni huyu:
Ni hafidh mkubwa, Imamu aliyebobea, mwenye kufuata Aathaar (Sunna) mtunzi wa vitabu vingi.
2) Amesema Imamu Abu Bakri Ibn Mar'dawayhi:
"(Ibn Abi A'asim) ni Hafidh mwenye hadithi nyingi..".
3) Amesema Imamu Abul-Abbas Al-Nasawiy:
Abu Bakri Ibn Abi A'asim...Alikuwa Thiqa (muadilifu Mwenye hifdhi nzuri) mwerevu alipewa umri mrefu".

Tazama habari zake katika vitabu vifuatavyo:
Al-Jar'hu wat-Ta'adil juzuu ya 2 ukura 67.
Siyaru A'alaamin-Nubalai juzuu ya 13 ukurasa 430-439.
Lisanul-Mizan juzuu ya 6 ukurasa 349.

Mpokezi wapili ni Abu Umayr, naye jina lake ni: Muhammad bin Issa bin Is'haq Al-Ramliy, amefariki mwaka 256 H.

Je wanachuoni wanasema nini kuhusu yeye?

1) Amesema Al-Imamu Abu Zur'a: (Abu Umayr) ni Thiqa (mwadilifu mwenye hifdhi nzuri).
2) Amesema Imamu Al-Nasaiy: "Thiqa" (mwadilifu mwenye hifdhi nzuri).
3) Amesema Imamu Abu Hatim: Alikuwa (Abu Umayr) ni miongoni mwa wacha Mungu wa kiislamu.
4) Aliulizwa Imamu yah'ya Ibn Mai'n kuhusu Abu Umayr akasema: "Thiqa ni katika watu waliozihifadhi vizuri hadithi za Dhamrah".

Tazama vitabu vya marejeo vifuatavyo:
Al-Jar'hu wat Ta'adil juzuu ya 6 ukurasa 286.
Tah'dhibul-Tahdhibi juzuu ya 4 ukurasa 461.
Al-Taq'ribu Tar'jama namba 5984.
Mpokezi wa tatu ni Dhamrah, naye jina lake ni Dhamrah bin Rabi'a Al-Filistiiniy Abu Abdillahi, asili yake ni Damascus.

Kauli za maulamaa kuhusu Dhamrah:
1) Amesema Imamu Al-Nasaiy: "Thiqa" (mwadilifu mwenye hifdhi nzuri).
2) Amesema Abu Hatimi: "Alikuwa ni mtu mzuri".
3) Amesema Ibn Sa'd: "Alikuwa Thiqa".
4) Imamu Ibn Hibbana amemtaja miongoni mwa watu waadilifu wenye kuhifadhi.

Tazama maelezo hayo katika vitabu vifuatavyo:
Al-Jar'hu wat-Ta'dil juzuu ya 4 ukurasa 467.
Tabaqaat Ibn Sa'd juzuu 7 ukurasa 471.
Al-Thiqaat cha Ibn Hibbaana juzuu ya 7 ukurasa 324.
Tah'dhiibul-Kamaal juzuu ya 13 ukurasa 317.

Mpokezi wa nne, ni Al-Saybaaniy naye jina lake kamili ni Yah'ya Ibn Abi Amri Al-Saybaaniy Al-Himsiy, Abu Zur'a. Amefariki mwaka 148 H.

Mtazamo wa maulamaa kuhusu yeye:

1) Amesema Imamu Ah'mad Ibn Hanbal: "yeye ni Thiqa tena Thiqa" !
2) Amesema Imamu Abu Aliy Al-Naysaaburiy: (Al-Saybaaniy) ni mmoja miongoni mwa watu waadilifu wenye kuhifadhi (al-Thiqaat) tena katika hadithi zake zote.
3) Na Imamu Ibn Hibbaan amemtaja katika orodha ya watu waadilifu wenye kuhifadhi vizuri.

Kwa maelezo zaidi tazama vitabu vifuatavyo;

Al I'Lal juzuu ya 1 ukurasa 379.

Al-Thiqaat juzuu ya 7 ukurasa 609.

Al-Tah'dhibu juzuu ya 6 ukurasa 166,Tarjama namba 8791.

Al-Taq'ribu Tarjama namba 8581.

Mpokezi wa tano ni Amru bin Abdillahi Al-Shaybaaniy Abu Abdil-Jabbaar Al-Hadh'ramiy.

Kauli za maulamaa kuhusu yeye:

1) Imamu Ibn Hibbaan amemtaja katika orodha ya watu waadilifu na kuhifadhi vizuri.
2) Amesema Imamu Al-I'jliy: "Huyo ni mtu wa Sham, ni katika wanafunzi wa maswahaba, ni Thiqa.
3) Amesema Ibn Hajar : "Maq'boul" (ni mtu wa kukubaliwa)".

Tazama vitabu vifuatavyo:

Al-Thiqaat juzuu ya 5 ukurasa 179.

Taarikhul Thiqaat ukurasa wa 365.

Al-Taq'ribu Tarjama namba 5701.

Mpokezi wa sita ni Swahaba Abu Umamah ambaye jina lake ni Sudayi bin A'jlaan Al-Baahiliy –radhia llaahu an'hu- aliyefariki mwaka 86 H.

Pia kuna hadithi nyingine kama hii tena kwa sanad iliyosafi kabisa imesimuliwa kutoka kwa Amru bin Thabit Al-Ansaariy kwamba

amesimuliwa na baadhi ya Maswahaba wa Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam-
Tazama kitabu Al-Sunna cha Ibn Abi A'sim ukurasa 199 Hadithi namba 430.

JARIBIO LAKE JINGINE LA UPOTOSHAJI

Ndugu Juma katika kuipinga mat'ni ya hadithi hii na nyinginezo amesema:
"Zingatia katika hadithi hii maneno yanayosema kwamba tusije tukababaika bure tutapomuona Al-Masihi Al-dajal tukadhani kuwa ndio Mwenyezi Mungu kweli, kwa sababu Al-masihi Al-dajal ana chongo.
Hii ndio tofauti baina yao. Ni vigumu kukubali kuwa haya maneno ni maneno ya Nabii.
Kama Mtume ndiye aliyeyasema haya basi angesema kuwa:

"asikudanganyeni kwa sababu Mwenyezi Mungu (S.W) (hana mfano wa kitu chochote) lakini kuifanya chongo ya Al-masihi Al-dajal kuwa ndio alama itakayomtofautisha baina yake na Mwenyezi Mungu ni jambo lisilokubaliana na akili, kwa sababu kila asiyekuwa Mwenyezi Mungu ni tofauti na Mwenyezi Mungu: na hakuna haja ya kulihusisha chongo au kitu kimoja dhidi ya chengine". Mwisho wa kunukuu. Tazama katika kitabu chake "Hoja zenye Nguvu" ukurasa wa 207-208.

MAJIBU YETU

Sisi tunasema kwamba kila ambacho kimetuthibitikia kwa mapokezi sahihi kutoka kwa Mtume wetu -swalla llaahu alayhi wasallam- tunakiamini kuwa ni wah'yi, mpaka tutakapobainikiwa kwamba ni dhidi ya hivyo.

Na Mtume –swalla Ilaahu alayhi wasallam- yeye ameletwa kwa watu waliokuwa katika zama zake na watakaokuja baada yao hadi siku ya Qiyamah; waarabu na wasio waarabu, na ana wajibu wa kuwabainishia watu wa tabaka zote kwa kadiri ya akili zao na tofauti za viwango vyao vya kielimu.
Imethibiti katika maandiko mengi kwamba Masihul Dajjal atakuja katika zama za mwisho (Akhirul Zaman) wakati ambao utakithiri ujinga kwa kiwango kikubwa na elimu ya dini itatoweka.
Na fit'na za Masihul Dajjal zitawakumba watu wengi na katika fitna zake atadai Utume, kisha Uungu na ataonesha mambo ya miujiza chungu nzima na watu wengi watahadaika kwa hilo, kwa sababu ya ujinga wao, hivyo bwana Mtume –swalla Ilaahu alayhi wasallam- kwa kuizingatia hali hiyo akamuelezea Masihi huyo wa uwongo kwa uwazi wazi na mpaka kufikia kutaja tofauti kama hizo kwa mujibu wa akili na hali za wakati huo.

Ni watu wangapi leo hii wamehadaliwa na Utume wa uwongo wa Mirzai na hana lolote la ajabu alilokuja nalo?!
Na maandiko ya wazi wazi yenye kukana kuendelea kwa Utume yanavunjwa vunjwa, na watu kwa sababu ya ujinga wao wakawa wanasadiki na kuyaona kuwa ni haki, bali wakajitokeza watu wenye kudai elimu kama Juma Mayunga wakaja wakazitetea hoja hizo dhaifu tena kwenye tafsiri ya kitabu cha Allah?!
Kwa hiyo Juma asishangae Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam kuyatamka hayo, kwa sababu yuko katika kuuelimisha umma na kuupa tahadhari dhidi ya upotoshaji wa Masihi wa uwongo.
Kwa hiyo mpaka hapo ndugu msomaji utakuwa umebainikiwa kwamba muda wakuwa watu wako hai hapa duniani hawatomuona Allah mpaka watakapokufa, kama alivyotuelezea bwana Mtume –swalla Ilaahu alayhi wasallam-.

HOJA YAO YA TATU

Amesema ndugu Juma katika ukurasa wa 311-312:
"Na dalili ya tatu ambayo imeonesha kuwa Mwenyezi Mungu haonekani ni aya isemayo:

"وما كان لبشر أن يكلمه الله إلاّ وحياً أو من وراء حجاب"

"Na haiwi kwa mtu (yeyote yule) kuwa Mwenyezi Mungu azungumze naye ila kwa (njia ya) wahyi au nyuma ya pazia (bila ya kuonana).
Sura ya 42 aya ya 51.

Aya hii ameitolea ushahidi Mama wa Waumini Bibi Aaisha (R.A) kuwa Mwenyezi Mungu haonekani alipoulizwa na Mas'ruq kuhusu Mtume (S.A.W.) kuwa kamuona Mwenyezi Mungu alipokwenda mbinguni. Na imekuja riwaya kutoka kwake aliyoipokea Al-imamu Muslimu. Nayo ni hoja ya wazi kabisa tunavyoisoma kuwa Mwenyezi Mungu hazungumzi na kiumbe ila kuwe kuna pazia (bila ya kuonana)."
Mwisho wa kunukuu.

MAJIBU YETU

Majibu yetu katika hoja hii ni kwa njia tatu:

Njia ya kwanza:
Kama utaisoma kwa umakini aya iliyotumiwa kuwa ndiyo hoja ya kutokuonekana Allah —Azza wajalla- utagundua kwamba haina ushahidi wowote katika suala hili ambalo tunalizungumzia.
Aya inazungumzia suala la kuwa haiwezekani kuzungumza na Allah ana kwa ana ila kwa njia mbili tu: kwa wah'yi au nyuma ya pazia. Na wala haizungumzii suala tunalolijadili hapa la kumona Allah kwa macho huko akhera.

Njia ya pili:

Suala analolikanusha Bibi Aisha –Radhiyallaahu An'haa- ni madai ya baadhi ya watu kwamba bwana Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- amemuona Mola wake usiku alipokwenda mbinguni, na wala hazungumzii suala la kuonekana Allah huko akhera au kutokuonekana.

Njia ya tatu:

Tujaalie kwamba huo ni ufahamu wa Bibi Aisha kwamba Allah hataonekana kwa macho huko akhera –na hali ya kuwa huo si msimamo wake- utakua ufahamu wake huo unapingana na ufahamu wa maswahaba wenzake, bali unapingana na mafundisho sahihi ya Mtume swalla llaahu alayhi wasallam pale aliposema:

"إنكم سترون ربكم كما ترون هذا القمر لا تضامون فى رأيته ...الحديث"
انظر صحيح البخاري كتاب التوحيد باب رقم24 رقم الحديث 7434.

"Hakika nyinyi MTAMUONA MOLA WENU kama mnavyo uona huu mwezi, wala hamsongamani katika kuuona…".

Tazama Hadithi hii katika Sahihul-Bukhari, KitabulTawheed, Mlango namba 24, hadithi namba 7434.

Kwa hiyo hoja yao hii nayo pia imeanguka chini.

HOJA YAO YA NNE

Hoja yao ya nne, ni hadithi ya Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam-, amesema Juma Al-Mazrui:

"Hadithi wamezitolea ushahidi wale wenye kukataa kuonekana kwa Mwenyezi Mungu, ziko kama tatu, lakini inatosha hapa kunukuu moja tu, kwani Qur'an ndio msingi wa itikadi na tumethibitisha kwa aya za Qur'an kuwa Mwenyezi Mungu haonekani.

Ama hadithi kwa mujibu wa Jumhuri ya umma huwa haichukuliwi katika mambo ya itikadi ila ikiwa ni mutawatir.

Kwa hivyo ikiwa umelifahamu hili, utakuwa umefahamu kwamba kutoa kwetu ushahidi kwa hadithi katika maudhui hii ni kwa sababu hadithi

hizi au hadithi hii ahadi imekubaliana na Qur'an, kwahivyo katika hali hii inapata nguvu za Qur'an.
Mwisho wa kunukuu.
Tazama ukurasa wa 319 wa kitabu chake "Hoja zenye Nguvu".

MAJIBU YETU

Hapa kuna nukta mbili za kuzijadili:

Nukta ya kwanza:

Ni kuhusu kauli yake aliposema: "kwani Qur'an ndio msingi wa itikadi..".

Sisi tunasema: hata Sunna pia ni msingi wa itikadi kama vile Qur'an, amesema:

"وما آتاكم الرسول فخذوه وما نهاكم عنه فانتهوا"

"Na anachokupeni Mtume chukueni, na anacho kukatazeni jiepusheni nacho",

Suratul Hash'ri (59) aya 7.

Na miongoni mwa aliyotupa bwana Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- ni mambo ya itikadi na sheria ya dini.
Na yote hayo tunatakiwa kuyakubali na kuyafanyia kazi bila ya kukidharau chochote katika mafundisho yake.

Nukta ya pili:

Ni kuhusu kauli yake: "Ama hadithi kwa mujibu wa Jumhuri ya umma huwa haichukuliwi katika mambo ya itikadi ila ikiwa ni mutawatir."
Maneno haya, hayana ukweli hata kidogo, na wala hayakujengwa juu ya msingi wa kielimu, bali ni maneno porojo yaliyojaa ubabaishaji ndani yake.
Ushahidi wa hilo ni huu:

Kwanza ndugu Juma anataka kutuambia kwamba kauli ya maulamaa wengi ni kuwa katika mambo ya itikadi hawazikubali ila hadithi mutawatir.

Na hali yakuwa mambo ni kinyume chake, na sijui aliposema Jumhuri ya uma alikuwa anawakusudia kina nani?

Kama makusudio yake ni wanavyuoni wengi wa hadithi ambao ndiyo wataalamu wa fani hii, maneno hayo si kweli.

Na kama ni mkweli basi atuthibitishie hilo kwa data za kielimu na si kwa maneno matupu.

Na kama makusudio yake aliposema "Jumhuri" ni mpaka wajinga ambao hawana utaalamu wowote katika fani hii, hilo pia si kweli, na hata kama ni kweli msimamo na ufahamu wao si hoja katika mambo ya kielimu.

Pili, ni kuhusu maana ya mutawatir, Je anakusudia mutawatir kwa istilahi ya wanavyuoni wa hadithi ambao ndiyo wataalamu wa fani hii? au anakusudia hadithi mutawatir kwa istilahi yake yeye na kaumu yake? Kama ni mutawatir kwa istilahi ya kitaalamu katika elimu ya hadithi, basi hebu sikiliza kauli za wataalamu wa fani ya mambo ya hadithi wanavyosema:

Amesema Imamu Al-Tahaawiy:

وأما الأحاديث عن النبي صلى الله عليه وسلم وأصحابه الدالة على الرؤية فمتواترة...".
شرح العقيدة الطحاية 1/189- 193.

"Na ama hadithi (zilizopokelewa) kutoka kwa Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- na maswahaba zake zenye kuelezea kuonekana (Allah) ni Mutawatir".

Tazama Shar'hul-Aqidati Tahaawiyah ukurasa wa 189-193

Amesema Imamu Ibn Kathir:

"وقد ثبتت رؤية المؤمنين لله – عز وجل – فى الدار الآخرة فى الآحاديث الصحاح من طرق متواترة عند أئمة الحديث لا يمكن دفعها ولا منعها...".
تفسير القرآن العظيم لإبن كثير 3670/8.

Amesema Imamu Ibn Kathir:

“Na limethibiti (suala la) waumini kumuona Allah –Azza Wajalla- huko akhera kwa hadithi sahihi kwa njia zilizo mutawatir (kwa njia nyingi ambazo ni muhali kuwa wapokezi wake wameafikiana kutunga uwongo) mbele za watu wa hadithi na haiwezekani kuzizuia wala kuzikataa”.
Tazama Tafsiri ya Ibn Kathir juzuu ya 8 ukurasa 367.chapa ya Daaru Ibn hazmi, Beirut-Lebanon.

1) Na kama lengo lake ni kwa maana ya kitaalamu, swali kwani mutawatir ni watu wangapi? na atajibu nini kuhusu riwaya zote hizi zilizo sahihi? Na isitoshe wengi katika wataalamu wa fani hii wanaelezea kuwa hadithi hizi zimekuja kwa wingi mno mpaka kufikia daraja hiyo ya mutawatir, na bila shaka kauli za wataalamu wanapo lizungumzia jambo linalohusu fani zao hupewa uzito wa aina yake, na wao ndiyo wanaotuambia kuwa hadithi za kuthibitisha kuonekana Allah kwa macho ni mutawatir.

2) Hata hali halisi nayo pia inaiunga mkono rai hii kwa sababu hadithi hizo zimepokewa kutoka kwa maswahaba hawa wafuatao:

1)Abu Bakar Siddiq.2)Aliy Ibn Abi Twalib.3)Ibn Mas’oud.4) Muadh Ibnu Jabal. 5) Abu Musa Al -Ash’ariy. 6) Ibnu Abbaas.7) Ibnu Umar.8) Abu Umaamah. 9) Muawiyah. 10) Abu Hurayrah. 11) Jaabir. 12) Hudhaifah. 13) Anas Ibn Maalik.14) Ammaar Ibn Yaasir. 15) Zayd Ibn Thabit. 16) Fadhala Ibn Ubayd.
Na wengineo katika Maswahaba wa bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam –Allah awe radhi nao wote-.
Na pia zimepokelewa kauli nyingi kutoka kwa Tabiina wengi (wanafunzi wa maswahaba) kama vile:

17) Said Ibn al Musayyib. 18) Twaaus. 19) Mujaahid. 20) Ikrimah. 21) Muhammad Ibn ka'b al-Quradhiy. 22) Abul Aaliyah. 23) Hasan al Basriy. 24) Abdul-Rahmaan Ibn Abi Layla. 25) Qataadah Al-Saduusiy. 26) Abu Is'haq al-Sabi'y. 27) Dhahaak Ibn Muzahim, na wengineo.
Na ama katika maimamu wakubwa ni hawa wafuatao:

28) Imamu Malik Ibn Anas. 29) Al-Layth Ibn Sa'ad. 30) Al-Awzaiy. 31) Sufyan al-Thawriy. 32) Sufyan Ibn Uyaina. 33) Jarir Ibn Abdil Hamid. 34) Abdullahi Ibn Mubarak. 35) Waki'i. 36) Yazid Ibn Haroun. 37) Imamu Shaafiy. 38) Abu Nuaym.
39) Sulaiman Ibn Harbi. 40) Abdullahi Ibn Wahbi. 41) Imamu Ahmad Ibn Hanbal. 42) Ibn Jarir al Twabariy. 43) Imamu Abdul-Qadir al-Jaylaaniy.
Na wengineo wengi ambao hatukuwataja kwa kuchelea kurefusha.

HADITHI WANAYOITEGEMEA

Amesema ndugu Juma Mazrui:
"Hadithi hii inasema:
"ما بين القوم وبين أن ينظروا إلى ربهم إلاّ رداء الكبرياء على وجهه فى جنة عدن".

"Hakuna kitakachozuia baina ya watu na baina ya kumtazama Mola wao katika pepo ya Aden (ya kukaa milele) isipokuwa vazi la kibri (ukuu na utukufu) lilopo katika Dhati Yake."
Na maana ya maneno haya ni kuwa lau kama si utukufu wa Mwenyezi Mungu basi watu wa peponi wangemuona Mwenyezi Mungu kwa jinsi alivyowaridhia, lakini utukufu wake ndio uliozuia wasimone".
Mwisho wa kunukuu.
Tazama ukurasa wa 325 katika kitabu chake "Hoja zenye Nguvu".

MAJIBU YETU

Hadithi hii ni kama zilivyo dalili zao nyingine zilizotangulia, si hoja ya kukataa kuonekana Allah huko akhera kwa macho.

Bali hadithi hii inazungumzia kwamba baina ya waja na Mola wao kuna pazia na kizuizi ambacho kinawazuia wao kumuona yeye hapa duniani.

Lakini zimethibiti hadithi nyingi za bwana Mtume —swalla llaahu alayhi wasallam- kwamba kizuizi hicho kitaondolewa siku ya Qiyama kwa waumini na watamuona Mola wao katika uwanja wa hisabu, kadhalika huko peponi.

Amesema Mtume —swalla llaahu alayhi wasallam-:

"...فيكشف الحجاب, قال: فوالله لم يعطوا شيئا أحب إليهم من النظر إليه".

"...BASI ATAONDOA PAZIA -naapa kwa Allah-! Hawajawahi kupewa kitu wanacho kipenda zaidi kuliko kumtazama yeye (Allah subhaanahu wata'alaa)".

Kwahiyo kizuizi hicho ambacho kilikuwa kikiwazuia watu duniani kumuona Mola wao, Mtume —swalla llaahu alayhi wasallam- anatwambia kuwa Allah atakiondoa kizuizi hicho huko akhera ili awakirimu waja wake waliowema kwa kumuona.

Sisi tunayaamini na kuyasadiki maneno yote ya Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam-, na hatulipingi jambo lolote lililothibiti kutoka kwake -swalla llaahu alayhi wasallam- na tuko mbali kabisa na mwenendo wa watu wa bid'a, kwa sababu wao wanayaamini na kuyasadiki yale yanayoafikiana na mapenzi ya nafsi zao, ama yale yaliyo kinyume na mapenzi yao wanayakataa.

Na pia tunasema kwamba Allah anafanya atakalo na wala hakuna wa kumpinga hukumu yake.

Na Allah kufanya hilo sio kwenda kinyume na utukufu wake, bali huo ni katika ukamilifu wa utukufu wake: kuwa yeye anafanya atakalo na hakuna wakumuuliza kwanini?

Na ama kauli ya Juma kwamba: “Lakini utukufu wake ndio uliozuia watu wasimuone”.

Kauli hiyo si kauli ya kweli, na wala hakuna hadithi hata moja inayosema hivyo.

Bali ukizisoma hadithi kwa umakini utazikuta zimetaja maneno haya: iliyozuia ni “Nuru” au “Hijaab” au “Ridaaul Kibriyai” na maneno yote haya makusudio yake ni kitu kimoja, kwa sababu hijabu yake ni Nuru na ndiyo hiyo Ridaul-Kibriyai, na bwana Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- anasema Allah ataiondosha hijabu hiyo na watu watamuona yeye –Jalla Jalaaluh-.

Kwa hiyo hadithi hiyo si hoja wala ushahidi wa kupinga kuonekana Allah huko akhera kwa macho.

SURA YA SITA

KAULI ZA BAADHI YA MAIMAMU JUU YA SUALA HILI.

1- Amesema Imamu Malik:

"الناس ينظرون إلى الله يوم القيامة بأعينهم".

“Watu watamtazama Allah siku ya Qiyama kwa macho yao”.

Tazama kitabu al-Shari’a cha Imamu al Ajurriy juzuu 2 ukurasa 8.

Shar’hu Usuuli I’itiqaad juzuu 1 ukurasa 318.

2- Amesema Imamu Shaafiy:

Amesema mwanafunzi wa Imamu Shaafiy al-Rabi’i bin Sulayman nilihudhuria kwa Muhammad bin Idrisa al-Shaafiy, ikamjia karatasi yenye swali kutoka nje ya mji (aliulizwa hivi):

“Unasemaje kuhusu kauli ya Allah:

"كلا إنهم عن ربهم يومئذ لمحجوبون". سورة المطففين الآية 15.

“Hapana sivyo hivyo kwa hakika wao siku hiyo watazuiliwa (kumuona) Mola wao”.

Suratul Mutaffifiina aya ya 15.

Akasema Imamu Shaafiy:
"Walipozuiwa hawa (makafiri kumuona Mola wao) kwa sababu ya kuchukiwa, hiyo ni dalili juu ya kwamba wao (waumini) watamuona yeye kwa sababu ya radhi (za Allah)...".
Tazama Shar'hu Usuuli I'tiqaadi Ah'li Sunna cha Imamu al-Laalakai juzuu 1 ukurasa 321.

JARIBIO LA KUIPOTOSHA KAULI HII

Amesema Juma:
"Riwaya hii ambayo imenasibishwa kwa Al-imamu Al-shafi pia si sahihi kwa sababu imesimuliwa na IBN HARIM AL-QURASHI naye ni dhaifu bali wengine wanasema hajulikani kamwe".
Mwisho wa kunukuu. Tazama ukurasa wa 171 katika kitabu chake.

MAJIBU YETU

Sisi tunasema kwamba kauli ya Imamu Shaafiy ni kauli sahihi na imepokewa kwa mapokezi sahihi, lau kama ndugu Juma alikuwa na nia ya kuufikia ukweli angefuatilia kwa kina, na kama angefanya hivyo angezipa riwaya sahihi na miongoni mwa hizo ni hii:

قال الإمام الحاكم حدثنا الأصم حدثنا الربيع بن سليمان قال حضرت محمد بن إدريس الشافعي...الخ

"Amesema Imamu al-Hakim, ametusimulia al-Asam, ametusimulia al-Rabii bin Sulaiman amesema nilihudhuria kwa Muhammad bin Idrisa al-Shaafiy....".
1- Al-Asam ni Muhammad bin Ya'qub bin Yusuf bin Ma'qil bin Sinan.
Amesema Imamu al-Dhah'biy al-Asam ni Imamu Muhadith katika zama zake
Tazama Siyaru a'laamin Nubalai juzuu ya 15 ukurasa wa 452-460.
2- Al-Rabi' bin Sulaiman bin Abdil-Jabbar al-Muradiy mwanafunzi mkubwa wa Imamu Shaafiy.

Amesema Imamu Abu Said Ibn Yunus na wengineo kuwa Al-Rabi' ni "THIQA".
Tazama kitabu Siyarul-A'laami juzuu ya 12 ukurasa wa 587-591.

Kwahivyo sanad hii ni sahihi kutoka kwa Imamu Shaafiy na hayo ni maneno yake, na huo ndiyo msimamo wake, lakini sijui ni kwa mantiki gani Juma ameiacha riwaya hii sahihi kutoka kwa Imamu Shaafiy inayoelezea msimamo wake, na akaamua kuitaja riwaya hii ambayo anasema kuwa ni dhaifu ? Kisha akakata hukumu moja kwa moja bila ya woga wala haya!

3- Amesema Imamu Ah'mad bin Hanbal:

"من قال: إن الله تعالى لا يرى فهو كافر".

"Mwenye kusema kwamba Allah hatoonekana (huko Akhera) basi yeye ni kafiri".

Al Shari'a juzuu 2 ukurasa 10.

4- Amesema Imamu Abdul-Qadir al-Jaylaaniy:

"وينظر أهل الجنة إلى وجهه ويرونه لا يضامون فى رؤيته
قال تعالى:
((للذين أحسنوا الحسنى وزيادة)) قيل الحسنى: هي الجنة, والزيادة: النظر إلى وجهه الكريم,
وقال تعالى:
((وجوه يومئذ ناضرة* إلى ربها ناظرة)).
انظر كتابه الغنية 55/1.

"Na watu wa peponi watautazama uso wake –Jalla Jalaaluh- na watamuona na wala hawatotaabika katika kumuona, amesema Allah:

"للذين أحسنوا الحسنى وزيادة

'Wale waliofanya mema watapata wema na ziada''.

Surat Yunus (10) aya ya 26.

Imesemwa kuwa "Hus'na" ni pepo, na "Ziada" ni kuutazama uso wake (Allah) uliomtukufu.
Na amesema Allah:

"وجوه يومئذ ناضرة*إلى ربها ناظرة".**

"Zipo nyuso siku hiyo ni zenye kung'ara Ni zenye kumwangalia (kumuona) Mola wake".*

Surat al-Qiyamah aya 22-23."

Mwisho wa kunukuu.

Tazama katika kitabu chake Al-Ghun'ya juzuu ya 1 ukurasa wa 55.

Amesema Imamu al-Twahaawiy:

"والرؤية حق لأهل الجنة بغير إحاطة ولا كيفية كما نطق به كتاب ربنا..".
العقيدة الطحاوية ص 10.

“Na kuonekana Allah ni kweli kwa watu wa peponi, pasi na kumdhibiti na bila kuwepo namna, kama kilivyotamka kitabu cha Mola...”.

Tazama kitabu chake al-Aqidatu al-twahaawiyah uk 10.

Amesema Imamu Ibn Abil-Izzi al-Hanafiy:

قال الإمام ابن أبي العز الحنفي:
"المخالف فى الرؤية الجهمية والمعتزلة ومن تبعهم من الخوارج والإمامية. وقولهم باطل مردود بالكتاب والسنة. وقد قال بثبوت الرؤية الصحابة والتابعون وأئمة الإسلام المعروفون بالإمامة فى الدين, وأهل الحديث.....
وأما الأحاديث عن النبي صلى الله عليه وسلم وأصحابه الدالة على الرؤية فمتواترة...".
شرح العقيدة الطحاوية 189/1- 193.

“Wenye kupinga kuonekana (Allah) ni Jah'miyah na Mu'tazila na waliowafuata hao katika Makhawarij (Maibadhi) na (Shia) Imaamiya.

Na kauli zao ni batili, zenye kurudishwa kwa Qur'an na Sunna. Na waliosema kuthibiti kuonekana Allah ni maswahaba na wafuasi wao na maimamu wa kiislamu waliokua maarufu kwa uimamu katika dini na watu wa hadithi....

Na ama hadithi (zilizopokelewa) kutoka kwa Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam- na maswahaba zake zenye kufahamisha kuonekana (Allah) ni MUTAWATIR”.

Mwisho wa kunukuu.

Tazama Shar'hul-Aqidati Tahaawiyah ukurasa wa 189-193.

وقال الإمام ابن جرير الطبري:
"وأولى الأقوال فى ذلك بالصواب أن يقال : إن الله تبارك وتعالى وعد المحسنين من عباده على إحسانهم الحسنى أن يجزيهم على طاعتهم إياه الجنة....ومن الزيادة على إدخالهم الجنة أن يكرمهم بالنظر إليه..".جامع البيان 126/11.

Amesema Imamu Ibn Jarir al-Twabariy:

"Na kauli iliyobora katika suala hilo (la kuonekana Allah) ni kusemwa kuwa: Allah –Tabaaraka wata'alaa- amewaahidi watu wema katika waja wake kuwapa wema kwa sababu ya wema wao na kuwalipa pepo kwa sababu ya utiifu wao...na ziada yakuingizwa peponi ni kumtazama yeye (Allah)".

Tazama Tafsiru Tabariy 11/126.

قال الإمام النووي رحمه الله:

"اعلم أن مذهب أهل السنة بأجمعهم : أن رؤية الله تعالى ممكنة غير مستحيلة عقلاً وأجمعوا وأن المؤمنين يرون الله تعالى دون الكافرين...وقد تظاهرت أيضاً على وقوعها فى الآخرة, أدلة الكتاب واالسنة وإجماع الصحابة فمن بعدهم من سلف الأمة على إثبات رؤية الله تعالى فى الآخرة للمؤمنين ورواها نحو من عشرين صحابياعن رسول الله صلى الله عليه وسلم..."

المنهاج بشرح صحيح مسلم ابن الحجاج 21/4.

Amesema Imamu al-Nawawiy:

"Fahamu kwamba madhehebu ya Ah'li Sunna wote ni kwamba: kuonekana Allah ni (jambo) lenye kuwezekana na si muhali kiakili na wakapatana vile vile kutokea (jambo hilo) huko akhera, na kwamba waumini watamuona Allah kinyume na makafiri.... Na zimekuja kwa wingi dalili za kitabu (Qur'an) na Sunna na maafikiano ya maswahaba na waliokuja baada yao miongoni mwa waliotangulia katika umma huu juu ya kuthibitisha kuwa waumini watamuona Allah akhera na wakazipokea (hadithi hizo) zaidi ya maswahaba ishirini kutoka kwa Mtume –swalla llaahu alayhi wasallam-".

Tazama kitabu Al-Min'haj Shar'hu Sahihi Muslim 4/21.

قال الإمام ابن كثير رحمه الله:

"وقد ثبتت رؤية المؤمنين لله – عز وجل – فى الدار الآخرة فى الآحاديث الصحاح من طرق متواترة عند أئمة الحديث لا يمكن دفعها ولا منعها...".

تفسير القرآن العظيم لإبن كثير 3670/8.

Amesema Imamu Ibn Kathir:

"Na limethibiti (suala la) waumini kumuona Allah –Azza Wajalla- huko akhera kwa hadithi sahihi kwa njia zilizo mutawatir (kwa njia nyingi ambazo ni muhali kuwa wapokezi wameafikiana kutunga uwongo) mbele za watu wa hadithi na haiwezekani kuzizuia wala kuzikataa".

Tazama Tafsiri ya Ibn Kathir juzuu ya 8 ukurasa 367.chapa ya Daaru Ibn hazmi, Beirut-Lebanon.

Hizi ni kauli chache za baadhi ya wanavyuoni wa kiislamu juu ya suala hili la kuonekana Allah –Jalla Jalaaluh- huko akhera.

HATIMA

Mwisho ninapenda kukikhitimisha kitabu hiki kwa muh'tasari huu ufuatao:

1- Tumebainisha katika kitabu hiki kwamba, chanzo na chimbuko kubwa la watu kutumbukia katika itikadi za batili ni kuiacha njia sahihi aliyotuwekea bwana Mtume Muhammad swalla llaahu alayhi wasallam, njia ya Qur'an na Sunna kwa ufahamu wa wema waliotangulia (maswahaba na wafuasi wao na maimamu waliokuja baada yao). Na si kama alivyodai mwandishi wa kiibadhi Juma Al-Mazrui, kwamba chanzo cha upotevu ni kupinga kuwepo kwa Majazi katika Qur'an.

2- Watu wema watamuona Mola wao -Jalla Jalaaluh- katika viwanja vya hisabu huko akhera na halikadhalika watakapoingia peponi. Ama wanafiki na makafiri watazuiliwa kumuona.

3- Itikadi ya kuonekana Allah ni itikadi sahihi kwa mujibu wa hoja na dalili za Qur'an na Sunna sahihi za Mtume Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam- na kauli za maulamaa wakubwa wa kiislamu.
4- Hadithi zilizokuja kuielezea itikadi hii kuna miongoni mwa hizo zilizokuwa sahihi, pia zipo ambazo ni dhaifu. Na hizo hadithi sahihi zimefikia kiwango cha kuwa ni Mutawatir (ni hadithi zilizopokewa kwa wingi mno, kiasi ambacho haiwezekani kuwa wapokezi wake wameafikiana kutunga uwongo).
5- Na hiyo ndiyo itikadi ya Maswahaba wa Mtume Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam- na hiyo ndiyo itikadi ya Taabi'ina (wanafunzi wa maswahaba) na waliofuatia baada yao miongoni mwa maimamu wakubwa wa kiislamu kama vile: Abu Hanifa, Malik, Shaafiy, Ahmad bin Hanbal, al-Awzai'y, Abdullahi Ibn Mubarak, Sufyan al-Thauriy, Sufyan Ibn Uyaina, Abdul-Rahman Ibn Mah'di, Hammad Ibn Salama, Hammad Ibn Zaid, Shu'uba Ibn al-Hajjaaj, Abdullahi Ibn Wah'bi al-Masriy, Wakii Ibn Jarraah, al-Bukhari, Muslimu Ibn Hajjaaj, Abu Daud al-Sijistaniy, Abu Isa Tirmidhiy, an-Nasai, Ibn Majah al-Qazwiniy, al-Daaramiy, Ibn Khuzima, Ibn Hibbana, al-Baihaqiy, Ibn Jariri al-Twabariy, al-Tabaraaniy, Abu Abdillahi al-Hakim, al-Daaraqutniy, Said Ibn Mansour, al-Khatib al-Bagh'dadi, Ibn Abdil-Barri, Ibn Taymiyyah, Ibn al-Qayyim, Ibn Kathir, Al-Dhah'biy, al-Nawawiy, Ibn Hajar al-As'qalaaniy, Ibn Rajab al-Hanbaliy, al-Suyutiy, Muhammad Ibn Abdil-Wahab, al-San'aniy, al-Shawkaaniy, Siddiq Hasan Khani, na wengine wengi ambao hatukuwataja kwa kuhofia kurefusha, wote hao itikadi yao ni kwamba watu wema watamuona Mola wao huko akhera kwa macho.
6- Makundi yote ya bid'a kama vile: Jah'miyyah, Mu'utazila, Khawarij (Ibadhi) Shia Ith'naasharia wameipinga itikadi hii, kwa sababu ya kufuata matamanio ya nafsi zao, wakazitafsiri

aya za Qur'an kwa rai zao na wakazikadhibisha hadithi sahihi za bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- kwa madai yasiyo na msingi wowote, kama ulivyojionea mwenyewe katika kitabu chetu hiki.

KIMEKAMILIKA KITABU HIKI MNAMO SIKU YA JUMANNE TAREHE 25/SHAABAN/1428 H = 26/08/08.

كتبتُهُ

مصلياً ومسلماً على نبينا محمد وعلى آله وصحبه والتابعين لهم بإحسان إلى يوم الدين.
الراجي لرحمة ربه الكريم :

أبو الفضل قاسم بن مفوتا قاسم غفرالله له ولوالديه وللمسلمين.